

**7 NOVEMBA, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 7 Novemba, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu jana Jumapili, tarehe 6 Novemba, 2022, majira ya saa mbili asubuhi, kulitokea ajali ya ndege inayomilikiwa na Shirika la Ndege la *Precision Air* ambayo ilitua kwenye Ziwa Victoria, umbali wa takribani mita mia moja kutoka uwanja wa ndege wa Bukoba, Mkoani Kagera.

Waheshimiwa Wabunge ndege hiyo iliyopata ajali ilitokea Jiji Dar es Salaam kuelekea Bukoba, ikiwa na watu 43 ambapo miongoni mwao abiria ni 39 marubani wawili, wahudumu wa ndege wawili.

Waheshimiwa Wabunge mara baada ya taarifa ya ajali hiyo kutolewa, juhudi mbalimbali za kuokoa maisha ya wahanga wa ajali hii ilianza ambapo napenda kutambua kazi iliyofanywa na wadau mbalimbali walioshiriki katika zoezi la uokoaji wakiwemo wananchi

## **7 NOVEMBA, 2022**

waliokuwa jirani na eneo la ajali, uongozi wa Mkoa wa Kagera, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, taasisi mbalimbali kwa mwitikio wa haraka, ushirikiano na juhudi kubwa zilizofanyika katika kuokoa maisha ya abiria na kuivuta ndege hiyo kutoka ziwani.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa rasmi tuliyonayo mpaka sasa kuhusu ajali hii inaonesha kuwa abiria 26 wameokolewa na wanaendelea kupatiwa matibabu. Kwa upande mwingine abiria waliofariki katika ajali hiyo ni 19. Kwa niaba ya Bunge napenda kutumia nafasi hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa marafiki na Watanzania wote kwa kuwapoteza ndugu zao katika ajali hiyo.

Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina. Vilevile nawatakia majeruhi wote afueni na uponyaji wa haraka ili warejee kwenye haraka za ujenzi wa Taifa letu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa Serikali imewakilishwa kwenye tukio hili la ajali ambapo tumeshuhudia Mheshimiwa Waziri na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wakifika eneo la tukio na kuwafaraji majeruhi na wafiwa, nimeona ni vema na sisi Bunge tutume wawakilishi wetu watatu ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria yenye dhamana ya masuala ya maafa wafike eneo la tukio ili kuona hali halisi ya ajali na zoezi la uokoaji.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea kuomboleza vifo vilivyosababishwa na ajali hii na kuwaomba majeruhi afya njema, napenda kutoa rai kwa mamlaka zinazohusika kuendelea na uchunguzi wa chanzo cha ajali ili matokeo yake yasaidie kuepusha majanga kama haya wakati mwingine.

**7 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, poleni sana sana na tukio hili.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PATROBAS P KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, pamoja na wewe Mheshimiwa Spika, kwa kutoa pole tena kwa ajali kubwa iliyolikumba Taifa letu hapo jana, Mwenyezi Mungu aendeele kutunusuru katika majanga haya.

Taarifa za Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 37 la tarehe 16 Septemba, 2022;
2. Toleo Na. 38 la tarehe 23 Septemba, 2022;
3. Toleo Na. 39 la tarehe 30 Septemba, 2022;
4. Toleo Na. 40 la tarehe 07 Oktoba, 2022;
5. Toleo Na. 41 la tarehe 14 Oktoba, 2022;
6. Toleo Na. 42 la tarehe 21 Oktoba, 2022; na
7. Toleo Na. 43 la tarehe 28 Oktoba, 2022.

**7 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MHE. MARIAM N. NYOKA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Kutofuata Maelekezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Conchesta Leonce

**7 NOVEMBA, 2022**

Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 66

**Nafasi za Uwakilishi kwa Wazee Bungeni**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, ni lini Wazee watapata nafasi ya uwakilishi Bungeni kama ilivyo kwa Vijana na Wanawake ili waweze kusikilizwa na kutoa ushauri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PATROBAS P KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 66(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, imeweka sharti la aina sita za Wabunge ambao ni Wabunge wa kuchaguliwa kuwakilisha Majimbo ya Uchaguzi, Wabunge Wanawake wasiopungua asilimia thelathini ya Wabunge wote, Wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi, Mwanasheria Mkuu pamoja na Wabunge wasiozidi 10 wa kuteuliwa na Rais na Spika iwapo hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Ibara ya 67(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeainisha moja ya sifa ya mtu kuwa Mbunge ni lazima awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa. Hivyo tunatoa wito kwa Vyama vya Siasa nchini kutenga nafasi za uwakilishi wa wazee kama ilivyo kwa watu wenye ulemavu na vijana ili waweze kupata nafasi ya uwakilishi Bungeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchester Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu aliyoyatoa Naibu Waziri, ukitazama Viti Maalum vina utaratibu maalum ambao umeshushwa na Tume mpaka kwenye vyama vya siasa. Je, haiwezekani sasa kuhakikisha kwamba utaratibu huu unashushwa ndani ya vyama vya siasa ili vyama hivi viwajibike kuwateua wazee ili na wenyewe waweze kupata nafasi ndani ya Bunge?

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchester Rwamlaza hebu tusaidie, hilo kundi la wazee, unataka kundi la wazee kwa ujumla au kundi la wazee wanawake?

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, kundi la wazee kwa ujumla wao bila kujali wanawake au wanaume.

**SPIKA:** Sasa watateuliwa kwa kile kifungu cha ile asilimia 30? Maana ile ni mahususi kwa ajili ya wanawake. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**7 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WWENYE ULEMAVU (MHE. PATROBAS P KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Katiba yetu imeainisha vizuri katika vifungu hivyo, lakini pia ipo katika kifungu cha 36, 37 na 61 ambavyo vinatoa haki ya uwakilishi, lakini pia Ibara ya 21 ya Katiba, nayo pia inatoa haki ya kushiriki kwenye majukumu moja kwa moja ama kupitia uwakilishi. Zaidi kwenye Ibara ya 3 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaeleza Tanzania ni Nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi ya kidemokrasia, kijamaa isiyofungamana na dini au isiyofuata misingi ya dini na ina mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Spika, sasa katika vyama vingi vya siasa kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1992, vyama vya siasa vinapewa haki ya kupata wawakilishi kwenye vyombo mbalimbali vya maamuzi, ikiwemo vyama hivi vya upinzani. Kwa mfano mzuri tu ambapo moja ya chama ambacho kinafanya hapa nchini vizuri kuna jumuiya ya vyama ambazo zinakuwa na wawakilishi wake, kuna moja ya chama kina umoja wa vijana UVCCM, lakini pili chama hicho kinao umoja wa wanawake, lakini pia kuna umoja wa wazazi na wawakilishi hao wote wameendelea kuwemo humo.

Mheshimiwa Spika, pengine hata Mheshimiwa naye atanikubalia, naye ni mmoja wa wawakilishi katika chama chake kwa sababu ni bibi yangu na ni mama, Mheshimiwa Conchester, kwa hiyo, nafasi hiyo inatolewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naona umeshajua hakuna maswali mengine, haya ahsante sana, hakuna Mbunge mwingine amesimama. Nakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 67

**Hitaji la Uzio na Uwanja wa Michezo Sekondari ya Asharose Migiro**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga uzio na uwanja wa michezo katika Shule Maalum ya Watoto wa kike Asharose migiro iliyopo Wilayani Mwanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa michezo na utamaduni katika ukuaji na maendeleo ya wanafunzi na kutazama michezo na sanaa kwa mlengo wa ajira na stadi muhimu zinazochangia ukuaji wa



**7 NOVEMBA, 2022**

kiuchumi na kijamii, Serikali imedhamiria kuboresha miundombinu ya michezo katika Shule teule 56 nchini ikiwa ni wastani wa shule mbili kwa kila mkoa.

Mhesahimiwa spika, Shule ya Sekondari Asharose Migiro haipo kwenye mpango wa shule za sekondari zilizochaguliwa kuwa za michezo hivyo, inashauriwa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kutenga fedha kwenye Bajeti yake ya mapato ya ndani ili kuanza ujenzi wa uzio katika viwanja hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Mwanga haina mapato ya kutosha, je, Serikali haioni umuhimu wa kuisaidia halmashauri hii ili kujenga uzio katika shule hii muhimu ya wasichana ambayo inapata adha kubwa sana kutokana kutokuwa na uzio, usumbufu, changamoto ya wanyama pamoja na miti kuharibika wakati ambapo ndiyo inaoteshwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeielekeza Halmashauri ya Mwanga na natambua kwamba Mheshimiwa

**7 NOVEMBA, 2022**

Mbunge anajua, sawa kiwango chao bado sio kizuri sana. Sasa hivi sisi kama Serikali tumekuwa na mipango mingi ikiwemo kumaliza miundombinu ili wanafunzi wetu waweze kukaa katika maeneo salama ambayo yatawasaidia wao waweze kuwa na ufaulu mzuri katika masomo yao. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tulipokee kwa mipango ya baadaye ili tuweze kuja kulifanyia kazi baada ya kumaliza hili jukumu la kwanza ambalo tumejipangia kama Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti, sasa aulize swali lake.

Na. 68

**Fedha kwa Ajili ya Kuboresha na Kujenga Uwezo katika  
Huduma za Afya - Serengeti**

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kusaidia Hospitali ya Wilaya ya Serengeti na Nyerere *DHH* kwa kujijengea uwezo wa kutoa huduma bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde kumbe umeshamaliza, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA  
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 mpaka 2021/2022, imepeleka fedha Shilingi bilioni 2.36 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kwa ajili ya kuboresha huduma zinazotolewa kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti. Fedha hizo zimetumika kujenga majengo saba (7) ya kutolea huduma ambapo majengo sita yamekamilika na yanatoa huduma na jengo moja la Wodi ya Mama na Mtoto lipo kwenye hatua ya ukamilishaji. Aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022, imepeleka katika hospitali hiyo watumishi 16 na vifaa na vifaatiba mbalimbali vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Hospitali Teule ya Nyerere (Nyerere DDH) katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepokea vifaa tiba mbalimbali vya kutolea huduma za afya ikiwemo *haematology machine*, *biochemistry machine* na *urine analyser*. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Hospitali hii imetengewa bajeti ya kuajiri watumishi saba (7) wa kada mbalimbali za afya.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Pamoja na hayo niombe kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika bilioni 2.36 ambazo

**7 NOVEMBA, 2022**

zilipelekwa Hospitali ya Wilaya, zilichukuliwa milioni 400 ambazo zilikuwa kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Iramba katika Jimbo langu la Serengeti na hali ya afya kule ni mbaya, ni kituo cha muda mrefu kimechakaa na kinahudumia watu wengi. Je, ni lini Serikali itapeleka tena hizo fedha milioni 400?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hospitali ya Nyerere DDH inahudumia zaidi ya wakazi 100,000 katika Jimbo langu na idadi ya watumishi Saba iliyopelekwa bado kuna upungufu wa Madaktari 22, Wauguzi Wasaidizi 28 na Wauguzi wa kawaida 37.

Je, ni lini Serikali itatusaidia kuhakikisha tuna Madaktari wa kutosha na Wauguzi wengine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Jimbo la Serengeti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilipeleka Shilingi Bilioni 2.36 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Serengeti, kati ya fedha hizo, Shilingi Milioni 400 ilipelekwa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Iramba. Sasa kwa sababu Halmashauri walitumia fedha ile kujenga majengo ya hospitali ya Wilaya, kwanza naomba nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Serengeti kuhakikisha wanazingatia maelekezo ya Serikali. Fedha inapopelekwa kwa ajili ya kujenga vituo vya afya ijenge vituo vya afya kama ni

**7 NOVEMBA, 2022**

zahanati ijenge zahanati, kama ni hospitali ijenge hospitali badala ya kuhamisha matumizi bila kibali maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa maelekezo katika mapato yao ndani watenge kwa awamu Shilingi Milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Iramba.

Mheshimiwa Spika, kuhusina na Hospitali ya Nyerere DDH, ni kweli kwamba ina upungufu wa watumishi lakini Serikali imeendelea kupeleka watumishi, katika mwaka huu wafedha imetengewa ajira Saba kwa ajili ya kuonesha kwamba tunaendelea kupunguza upungufu wa watumishi katika hospitali hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba kuuliza Serikali ni lini italetwa fedha za awamu ya pili kuwezesha ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Ngara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisamba, Mbunge wa Jimbo la Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya ya Ngara ilipelekewa shilingi Milioni 500 mwaka wa fedha uliopita

**7 NOVEMBA, 2022**

na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunajenga hospitali zetu hizi kwa awamu, sasa tunakwenda awamu ya pili ambapo katika mwaka wa fedha huu hospitali hii pia imetengewa Shilingi Milioni 500 na zitakwenda wakati wowote ndani ya mwaka huu wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Sabu, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa tiba ikiwemo mtambo wa kuzalisha oxygen katika hospitali ya Wilaya Meatu katika jengo la mahututi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka huu wa fedha imetenga Shilingi Bilioni 69.95 kwa ajili ya kununua vifaa tiba na kuvipeleka katika vituo na hospitali zetu kote nchini. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza bajeti ya vifaatiba katika hospitali ya Wilaya ya Meatu tayari ipo, lakini tutakwenda kufanya tathmini kuona uwezekano wa kuwa na mtambo wa kuzalisha oxygen kulingana na mahitaji ili tuweze kuona namna ya kutekeleza wazo hilo.

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Justine Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hospitali ya *DDH* ya Ilula, bado inategemewa sana wananchi wa Tarafa ya Mazombe na Tarafa ya Mahenge. Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea kuipelekea fedha hospitali ili iweze kutoa huduma bora kama ilivyokuwa ikitoa mwanzo ilivyokuwa *DDH* kabla ya kujengwa hospitali ya Wilaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Justine Nyamoga, Mbunge wa Jimbo la Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha inawezesha hospitali zetu hizi za *DDH* kuendelea kutoa huduma kwa wananchi katika maeneo hayo. Kwanza kwa kuhakikisha kwamba fedha za mfuko wa pamoja *health center basket fund* zinaendelea kupelekwa, Hospitali hii ni moja ya hospitali zinazoendelea kupewa fedha hizo ili kuziwezesha kujiendesha na kutoa huduma bora, lakini pia kuangalia uwezekano wa kuendelea kuwapatia watumishi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuiunga mkono hospitali hii ili iendelee kutoa huduma kwa wananchi wa Mazombe na Tarafa zingine za karibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako sasa aulize swali lake.

**7 NOVEMBA, 2022**

Na. 69

**Madiwani wa Makambako Kuongezewa Posho**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Makambako wataongezewa posho kama ilivyo katika Halmashauri nyingine nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga Mbunge wa Jimbo la Makambako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiwalipa Madiwani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo Halmashauri ya Mji Makambako posho kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura 287 na 288 na kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2019 Halmashauri ya Mji Makambako imekuwa ikilipa posho ya vikao ya Shilingi 50,000 ikiwa ni Shilingi 10,000 zaidi ya kiwango kilichopendekezwa. Aidha, hivi sasa viwango vya posho za safari kwa Halmashauri hiyo vinalipwa kwa kuzingatia waraka wa zamani kwa sababu viwango vya posho mpya havikutengewa bajeti ya mwaka 2022/2023,



## 7 NOVEMBA, 2022

kwa kuwa wakati maelekezo ya mabadiliko ya posho hizo yanatoka tayari Bajeti ya Halmashauri ilikuwa imeandaliwa na kupitishwa kwenye vikao vya Kisheria vya Maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Makambako inashauriwa kufanya mapitio ya bajeti au izingatie maelekezo ya Waraka Na. 1 wa Utumishi wa Umma wenye Kumb. Na. CAC.17/228/01/A/176 wa Tarehe 10 Juni, 2022 kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Serikali swali lina maelezo madogo.

Kwa kuwa, fedha nyingi zinapelekwa za maendeleo katika Halmashauri zetu nchini zikiwepo za afya, barabara, maji, elimu. Na kwa kuwa hivi karibuni Rais wetu mpendwa mama Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha nyingi za kujenga madarasa katika sekondari zetu Mabilioni kwa Mabilioni. Sasa Madiwani hawa hawasimamii kwenye *force account* hawamo, na hawa ndiyo wanaowaeleza wananchi tumepata fedha kiasi gani.

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka Madiwani hawa wawemo ili kusudi maana ndiyo wanaowaambia wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa vilevile kama nilivyosema ndiyo wanaosimamia...

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, swali lako la pili lisiwe na maelezo marefu.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, halina maelezo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa hawa ndiyo wanaosimamia na Serikali posho za mwezi tulizungumza kwenye bajeti hapa tunaomba waongezewe. Je, madiwani wote nchini, bajeti ya 2023/2024 Serikali imejipangaje kuwaongezea posho za mwezi madiwani hawa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hospitali ya Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan imeleta fedha nyingi sana katika Halmashauri zetu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Lakini nimhakikishie kwamba kwa mfumo wa *force account*, kwa kuwa Waheshimiwa Madiwani ni viongozi wasimamizi wa miradi hiyo, mwongozo wa haukuwaweka Madiwani kuwa sehemu ya Kamati zile kwa sababu wanahitaji kuhoji zile Kamati. Kwa hiyo, kama Diwani atakuwa sehemu ya Kamati ile atashindwa kujihoji mwenyewe lakini atashindwa kusimamia wananchi katika maeneo yale katika kutekeleza miradi ile.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamuombe Mheshimiwa Mbunge aamini kwamba dhamira ya Serikali ni nzuri kwamba Waheshimiwa Madiwani wabaki na nguvu zao za kusimamia na kuhoji Kamati ili miradi iweze kutekelezwa kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na posho za Waheshimiwa Madiwani, kwanza niwahakikishie kwamba Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anathamini na anajali sana kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Madiwani na ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha amechukua jukumu la Serikali Kuu kulipa posho za Madiwani kama Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba Serikali inafanya tathmini ya kuona uwezekano na uwezo wa Serikali kuongeza posho hizo ili muda ukifika posho hizo ziongezeke kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda sasa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe, sasa aulize swali lake.

Na. 70

**Ushiriki wa Mbunge katika Miradi inayoibuliwa na TASAF**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA** aliuliza: -

Je, ni kwa kiwango gani Mbunge anashirikishwa katika miradi inayoibuliwa na wananchi katika Jimbo lake kupitia TASAF?

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mheshimiwa Deo Ndejembu majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uibuaji wa miradi ya jamii inayochangiwa na *TASAF* hufanyika kwenye mikutano ya jamii ambayo huendeshwa na wataalam chini ya usimamizi wa viongozi wa maeneo hayo. Mbunge au Mwakilishi wa eneo husika kama anakuwepo wakati zoezi la kuibua miradi likifanyika hazuiwi kushiriki kwa kuwa hakuna mwongozo unaomtaka Mbunge asiwepo wakati wa zoezi la kuibua miradi.

Mheshimiwa Spika, wananchi huibua miradi ambayo inatatua kero walizonazo katika jamii kutokana na kukosekana kwa huduma stahiki. Ikiwa wananchi wote kwenye mkutano wameridhia mradi fulani kutekelezwa, basi moja kwa moja huo unakuwa ni chaguo lao. Lakini kama kuna miradi miwili au mitatu iliyopendekezwa, jamii hupiga kura na mradi utakaopata kura nyingi ndio unapewa kipaumbele cha kuanza kutekelezwa. Jamii ikishaamua mradi wa kutekeleza, timu ya Wataalam hufanya bajeti ya mradi huo na kurudi tena kwa wananchi kukubaliana kuhusu mchango wa jamii kabla bajeti hiyo haijawasilishwa *TASAF* kwa hatua nyingine.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naomba kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza, niruhusu nitoe shukrani zangu za dhati sana kwa ofisi ya Rais kupitia *TASAF* kwa mradi mkubwa ambao wamenipelekea katika shule yangu ya *Peak*, kukarabati na ujenzi wa uzio shule ambayo Baba wa Mheshimiwa wetu Mzee Suluhu Hassan alifundisha, hivyo wamepeleka fedha nyingi pale nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza niliuliza Wabunge wanashirikishwaje? Nashukuru kwa majibu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati baada ya miradi ile ambayo imeibuliwa na wananchi Wabunge nao wakapata taarifa ili kuwa karibu na ile miradi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa mradi mkubwa huu uliopheleka katika skuli ya *Peak* Jimbo langu la Mtambwe kukarabati madarasa na uzio kuna baadhi ya maeneo bado hayajakamilika. Je, Serikali haioni ni wakati mzuri sasa hivi wa kuweza kupeleka fedha pale ili kukamilisha baadhi ya maeneo ambayo hayajakamilika? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa

## 7 NOVEMBA, 2022

Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalifa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu Je, sasa Serikali haioni umuhimu wa kuwapa taarifa Waheshimiwa Wabunge, naomba nitumie nafasi hii mbele ya Bunge lako hili kuelekeza ma-TMO wote ambao ni wasimamizi wa miradi hii ya TASAF katika Wilaya husika kuwa wanawapa taarifa Waheshimiwa Wabunge kwa miradi yote ambayo wananchi wameibua kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa tunafahamu Wabunge ndio wawakilishi wa wale wananchi wa yale maeneo husika hivyo ni muhimu sana kuweza kuwapa taarifa, nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge, kwamba miradi mingine itakayoanza kuibuliwa ndani ya Majimbo husika basi Wabunge wataanza kupewa taarifa ile.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kuhusu mradi wa Peak, bahati nzuri nimefika mpaka pale, hatua ya kwanza iliyoanza kwenye shule ile ilikuwa ni kujenga madarasa ambayo yalikuwa yamechakaa sana. Baada ya kumaliza ujenzi ule wa madarasa yale, wananchi wale wa eneo lile pia waliibua mradi mwingine ambao ni hitaji lao lilikuwa ni uzio katika shule ile. Kwa sababu ilikuwa ni njia ya wakazi wa pale kukatiza katikati ya skuli ile katika eneo la Peak. Baada ya kutambua hilo fedha ikatolewa na mradi wa TASAF baada ya kuibuliwa mradi na baada ya hapo ni uzio ule umejengwa.

Mheshimiwa Spika, kama kuna hitaji jingine wananchi wanaweza wakaibua na TASAF watafanyia kazi. *(Makofi)*

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, sasa aulize swali lake.

Na. 71

**Vikao Kujadili Changamoto za Muungano**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza:-

Je, vikao vinavyopokea na kujadili changamoto za Muungano bado vipo na lini vilikaa mara ya mwisho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Khamis Hamza Hamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji Mbunge wa Mwera kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kuwa vikao vya kupokea na kujadili changamoto za Muungano bado vipo na vitaendelea kuwepo kutokana na umuhimu wake kwa mustakabali wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kulitaarifu Bunge kuwa, kwa mwaka 2021/2022 vikao hivyo vilifanyika kwa

**7 NOVEMBA, 2022**

mujibu wa mwongozo huo ambapo kikao cha Kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia Masuala ya Muungano kilifanyika Tarehe 24 Agosti, 2021. Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, swali la nyongeza.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ambayo yamesema kikao chamwisho kilifanyika Agosti, 2021 na katika kikao hicho changamoto 11 kati ya 18 zilipatiwa ufumbuzi.

(a) Je, Serikali inaweza kulitaarifu Bunge sasa mambo hayo ni yapi?

(b) Ni lini Serikali italeti Muswada ili mambo haya sasa yatambulike kisheria kwamba yapo nje ya changamoto zetu na kila mtu afanye ya kwake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) swali la nyongeza la kwanza ni mahususi, kama huna ile orodha utampelekea Mheshimiwa Mbunge ili ayajue hayo mambo, lakini swali la pili liko wazi. Kama unayo orodha msomee kama huna utampatia orodha.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Jimbo la Mwera, kama iifuatavyo:-



## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika changamoto 25, jumla ya changamoto 28 zimeshapatiwa ufumbuzi, miongoni mwa hizo kama ambavyo umenishauri nitampelekea kwa maandishi ili aweze kuziona. Zipo changamoto kwa mfano kulikuwa kuna hoja ya uvuvi katika Bahari Kuu hii ilishapatiwa ufumbuzi, kulikuwa kuna hoja ya mgawanyo wa mapato ilishapatiwa ufumbuzi. Kulikuwa kuna hoja ya mapato yanayotokana na uhamiaji, hii ilishapatiwa ufumbuzi kwa upande wa Zanzibar, kulikuwa kuna hoja ya ucheleweshaji wa miradi ya maendeleo, kusainiwa kwa mikataba ya miradi ya maendeleo Zanzibar hili limeshapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kusainiwa kwa mkataba ujenzi wa Hospitali ya Mbiguni Zanzibar, ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, ujenzi wa barabar ya kutokea Chake, Machomanne, Meli Tano kuelekea kwa Binti Abeid kueleka Wete, yote haya na mengine yalishapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mengine kama ulivyoshauri nitampelekea kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuwa jambo hili la Muungano ni jambo ambalo hati zake zimesainiwa zipo na zina nguvu kisheria. Kwa hiyo, nimuambie tu Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu ni jambo ambalo linahitaji ridhaa ya pande zote mbili, wacha tukakae tutakapoona kuna haja ya kuleta kama Muswada basi tutalileta hapa. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Toufiq Salim Turkey, Mbunge wa Mpandae sasa aulize swali lake.

**7 NOVEMBA, 2022**

Na. 72

**Kuiwezesha TASAC Kuhudumia Meli Nyingi**

**MHE. AMINA ALI MZEE K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuiwezesha TASAC iweze kuhudumia meli nyingi?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq Salim Turkey, Mbunge wa Mpendae, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kuiwezesha TASAC kuhudumia meli nyingi, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza watumishi wa ukaguzi wa meli kutoka watumishi 23 hadi watumishi 34. Watumishi walioongezwa wamepelekwa mikoa yote yenye kuungana na bahari na maziwa. Aidha, katika kuboresha uwezo wa wakaguzi, TASAC imepata mkaguzi wa michoro na ujengaji wa meli (*naval architect*) na

**7 NOVEMBA, 2022**

imepeleka mkaguzi mmoja kwenda kusomea uchoraji na ujengaji wa meli nchini Uingereza.

Mheshimiwa Spika, TASAC pia imeingia makubaliano na Chuo cha *International Maritime Safety, Security and Environment Academy* kilichopo Nchini Italia ili kupatiwa mafunzo ya ukaguzi kwa meli za ndani na meli za nje (*Flag State Inspection and Port State Inspection*). Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Usalama wa vyombo vya majini ni lazima kwa maisha ya watu na mali zao. Je, Serikali inafanyaje kila baada ya muda kuvifanyia ukarabati kisheria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba usalama ni jambo la msingi na ni lazima lifanyike. Kwa sheria yetu tunafanya ukaguzi kila mwaka kwa vyombo vyote vya majini na kwenye maziwa makuu, na huwa tunatoa cheti

**7 NOVEMBA, 2022**

kinachoitwa *seaworthiness certificate*. Hata hivyo, hatulazimiki tu kwa mwaka, tunaweza tukafanya pia kwa wakati wowote inapobidi shirika lijiridhishe na vyombo hivyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 73

### **Ujenzi wa Uwanja wa Ndege – Simiyu**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Simiyu utaanza baada ya kukamilika zoezi la uthamini wa eneo la Uwanja utakapojengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako, sasa nimuite Mheshimiwa Naibu Waziri mwingine wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Simiyu kilifanyiwa Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa

**7 NOVEMBA, 2022**

ufadhili wa Benki ya Dunia mwaka 2017 kupitia Mradi wa *Transport Sector Support Project (TSSP)*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imekamilisha uthamini kwa maeneo na mali zitakazoathiriwa na utekelezaji wa mradi na kuandaa jedwali la uthamini ambalo tayari limeidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuendelea na taratibu za malipo.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya taratibu za kulipa fidia kukamilika, mipango ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Simiyu itaanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, swali nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa majibu yanaendelea kutolewa haya haya kila tukiuliza swali; je, nini kauli ya Serikali kuhusu lini uwanja huu utaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba Serikali imeshakwenda hatua kubwa mbele, tayari tumeshathamini na tayari maandalizi ya malipo ya watakaopisha mradi huu yako

**7 NOVEMBA, 2022**

yanafanyiwa kazi na tumeahidi kama Serikali kwamba baada ya kukamilisha suala hilo, ujenzi wa Uwanja wa Simiyu utaanza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 74

### **Serikali Kufanyia Kazi Hoja za Wamachinga**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali kuwasikiliza na kufanyia kazi hoja za wamachinga, hasa baada ya zoezi la kuwapanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo: -

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanyia kazi hoja za wamachinga, hasa baada ya zoezi la kuwapanga kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ambapo Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hukukutana nao mara kwa mara kwenye vikao na kujadiliana nao kupitia viongozi wao kwa lengo la kushughulikia hoja na kero zao.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Taifa, Serikali inasikiliza hoja zao kupitia viongozi wa Shirikisho la Umoja wa Machinga (SHIUMA) Taifa. Kutokana na vikao vinavyofanyika, Serikali imeweza kuwajengea uwezo katika masuala ya uongozi na utatuzi wa changamoto zao. Pia watendaji wa kata sehemu mbalimbali nchini ikiwemo kwenye masoko wamekuwa na mchango mkubwa katika kuwasikiliza na kufanyia kazi hoja na kero zao kwa kadri zinavyojitokeza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Je, kuna katazo lolote la watu hawa (wamachinga) kupangwa katika maeneo ya wazi katika halmashauri na maeneo ya taasisi?

Pili; je, Serikali inaweza kutoa ruhusa kwa ajili ya wamachinga, hasa waliokuwa wanauza mananasi, kuweza kujipanga eneo la *Railway* na wale wa samaki kurudi eneo la Manyema? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

**7 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inawajali sana wananchi wake, hasa wafanyabiashara wadogowadogo. Rais ametoa shilingi milioni 10 kwa kila mkoa kwa ajili ya kujengwa ofisi za wafanyabiashara wadogowadogo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tayari imeshachora michoro hiyo kwa ajili ya ujenzi huo. Wafanyabiashara hawaruhusiwi kufanya biashara zao katika maeneo ya wazi na ya taasisi. Wafuate maelekezo ya viongozi wao wafanye biashara katika maeneo waliyopangiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, eneo la wazi la Manyema, Moshi limetengwa kwa ajili ya shughuli za reli. Wafanyabiashara hawaruhusiwi kufanya biashara kwa ajili ya usalama wao, lakini pia kuzuia shughuli za shirika la reli hiyo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Moshi tayari imeshawatengea wafanyabiashara hao walioondoshwa katika eneo la Reli la Manyema kufanya biashara zao katika maeneo mengine. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.



**7 NOVEMBA, 2022**

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani, sasa aulize swali lake.

Na. 75

**Hitaji la Ukarabati Kituo cha Polisi Chaani Lungalunga – Zanzibar**

**MHE. JUMA USONGE HAMAD** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati wa Kituo kidogo cha Polisi cha Chaani Lungalunga.?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kituo kidogo cha Polisi cha Chaani, Lungalunga kilichopo Wilaya ya Kaskazini A ni kituo kilichojengwa kwa kushirikisha jitihada na nguvu za wananchi. Jengo la kituo hiki ni chakavu na haliwezi kufanyiwa ukarabati kwa sababu kuta zake zimeweka nyufa nyingi na kingo za jengo zimebomoka.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Kamisheni ya Zanzibar imeshaandaa mchoro na makadirio kwa ajili ya kujenga Kituo kipa cha Daraja C katika eneo hilo. Kiasi

**7 NOVEMBA, 2022**

cha fedha, shilingi 82,530,960 kinahitajika kwa ajili ya ujenzi huo, na zitaingizwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 kulingana na upatikanaji wa fedha. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nishukuru sana Serikali kwa *commitment* ya kutaka kukijenga Kituo hicho cha Lungalunga. Sasa naomba niulize swali langu la nyongeza.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atapanga ziara ya kuja kutembelea kwenye eneo hilo ili wananchi wale wawe na matumaini makubwa kwamba kweli Serikali ina *commitment* ya kutaka kujenga kituo hiki cha polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kabla ujenzi wa kituo hicho haujafanyika, nampa ahadi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kutembelea eneo hilo tukiwa pamoja naye ili kuweza kujiridhisha kwamba kazi itafanyika. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**7 NOVEMBA, 2022**

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 76

**Uhaba wa Madaktari Bingwa Hospitali ya Rufaa  
Mkoa wa Iringa**

**MHE. NANCY H. NYALUSI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya uhaba wa madaktari bingwa katika Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Iringa?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa hadi sasa ina jumla ya madaktari bingwa kumi na moja. Madaktari bingwa wa afya ya akina mama na uzazi wanne, madaktari bingwa wa upasuaji wawili, daktari bingwa wa magonjwa ya ndani mmoja, madaktari bingwa wa watoto wawili, daktari bingwa wa macho mmoja na daktari bingwa wa mionzi mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza idadi ya madaktari bingwa, Wizara imepeleka kusoma jumla ya madaktari kumi na mbili kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa, ambapo madaktari wawili wanasomea

**7 NOVEMBA, 2022**

kinywa, sikio na koo, madaktari bingwa wa mifupa wawili, daktari wa magonjwa ya dharura mmoja, madaktari bingwa wa watoto wawili, madaktari bingwa wa magonjwa ya ndani wawili, daktari bingwa wa meno mmoja, daktari bingwa wa usingizi mmoja na daktari bingwa mbobezi wa masuala ya watoto mmoja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali, lakini hali bado ni mbaya.

Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kutatua changamoto hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Afya alieleza juzi hapa Bungeni, ni kwamba tunaendelea kuangalia sasa ikama ya madaktari kwenye hospitali zote za mikoa kwenye nchi yetu na kuwaangalia mabingwa kote waliko, tukiona na kuangalia hali ilivyo pale Hospitali ya Mkoa wa Iringa ili kuweza kuwahamisha maeneo mengine ambayo yamezidi na kupeleka kule Iringa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna masomo yanayoendelea miezi mitatu mitatu kwa ajili ya *super specialists* kwa hiyo tutawaondoa nao kwenye eneo hili na kuwasomesha kwa muda mfupi na kuwarudisha kwenye eneo hilo.

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo katika Hospitali ya Mkoa wa Iringa inafanana kabisa na changamoto iliyopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara. Je, ni lini Serikali itakwenda kutatua changamoto hii ya uhaba wa madaktari, hasa kwa magonjwa ya wanawake na watoto katika hospitali hiyo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia mambo ya mkoa wake, na nakumbuka alikuja Wizarani kwa ajili ya hilo. Ninamuomba Mheshimiwa Mbunge tukutane wakati wa haya mapitio ya kuwahamisha tuone tunaweza kufanya nini kwenye eneo la mkoa wake.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 77

**Wanawake Kuwa Wachimbaji wa Madini Nchini**

**7 NOVEMBA, 2022**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wanawake wanakuwa wachimbaji wa madini nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *STAMICO* ina jukumu la kuwasadia wachimbaji wadogo wa madini wa makundi mbalimbali nchini wakiwemo wanawake. Aidha, *STAMICO* imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali kuhakikisha wanawake pia wanakuwa wachimbaji madini nchini.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo inahusisha, pamoja na mambo mengine, kutoa mafunzo mbalimbali ya nadharia na vitendo kwa wachimbaji wadogo wakiwemo wanawake kupitia vituo vya mfano tulivyonavyo katika maeneo ya Katente (Bukombe), Lwamgasa (Geita) na Itumbi (Mbeya); kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata taarifa sahihi za mashapo kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST*) ambapo kwa sasa *STAMICO* imeagiza mitambo mitano ya uchorongaji maalumu kwa ajili ya wachimbaji wadogo nchini ili kuwasaidia kufanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni kuwaunganisha wachimbaji na Taasisi za kifedha

## 7 NOVEMBA, 2022

zikiwemo Benki za CRDB, NMB na KCB kwa lengo la taasisi hizo kuweza kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo nchini wakiwemo wanawake. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanawake ni kundi maalum ambalo linatakiwa kuwezesha na kutambuliwa kisheria katika sheria zetu mbalimbali, je, ni nini mkakati wa Wizara kuhakikisha wanawake wanaingia kisheria kwenye hii Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Spika, pili, Songwe pia ni moja ya mikoa maarufu sana kwa uzalishaji wa madini; je, ni lini Serikali itakuja kuwapatia wanawake wa Mkoa wa Songwe mafunzo juu ya uchimbaji wa madini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la kwanza, Serikali inawatambua wanawake kipekee kabisa, siyo kama kundi maalum bali kama wadau muhimu katika sekta hii ya uchimbaji madini, na ndiyo maana tumeendelea kuwashirikisha wanawake katika mafunzo mbalimbali. Wizara imeendelea kuwafundisha faida za kushiriki katika uchimbaji wa madini, na imewahamasisha wajiunge kwenye vikundi ambavyo mpaka sasa hivi Tanzania tuna zaidi ya vikundi 20 vya wachimbaji wanawake na hata

**7 NOVEMBA, 2022**

kule Songwe pia tumeendelea kuhamasisha na wapo wachimbaji wanawake wasiopungua 15.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, Wizara ina mkakati maalum wa kutoa mafunzo nchi nzima na baada ya Bunge hili taasisi zetu za GST, Tume ya Madini na STAMICO, wamepanga kwenda kutoa mafunzo katika Mkoa wa Songwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 78

### **Nyavu Haramu**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kuzuia nyavu haramu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa Mkakati wa Kusimamia Rasilimali za Uvuvi ambao unajumuisha mbinu



**7 NOVEMBA, 2022**

mbalimbali za kudhibiti utengenezaji, uagizaji, matumizi na biashara ya nyavu haramu za uvuvi. Utekelezaji wa mkakati huo unahusisha wadau mbalimbali ikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama, sheria, watendaji wa taasisi zilizopo mipakani, bandarini na viwanja vya ndege; Viongozi wa Mikoa na Wilaya, wavuvi pamoja na watendaji wa Wizara kupitia vituo vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi. Aidha, elimu kwa wadau kuhusu matumizi ya nyavu sahihi, uvuvi endelevu na wenye tija inaendelea kutolewa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba niwe na maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza: Kwa kuwa nyavu nyingi zinaagizwa kutoka nje ya nchi na kuingizwa ndani ya nchi, lakini mwisho wa siku, mvuvi ndio amekuwa mhanga mkubwa wa hizi nyavu: Je, Serikali imewahi kuwawajibisha watendaji wengine kama ilivyowataja kwenye swali la msingi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wavuvi kupata vifaa vya kisasa ili waondokane na zana za uvuvi zilizopitwa na wakati?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**7 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Eng. Stella Simon Fiyao, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali kuhusu je, wapo ambao wamewahi kuwajibishwa kutokana na kwamba nyavu hizi huwa zinaagizwa kutoka nje au zinazalishwa na watu, wapo? Zipo kesi kadhaa ambazo zimewahusisha waagizaji na zilizowahusisha watengenezaji na kesi hizi zote tulipokwenda Mahakamani Serikali ilifaulu kwa kushinda kesi zile. Zipo kesi nyingine ambazo hata sasa bado zinaendelea. Wako watendaji ambao walichukuliwa hatua mbalimbali na wengine kesi zao bado ziko Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, swali la pili alitaka kujua juu ya uwezesaji wa makundi ya wavuvi kwa kupata vifaa vya kisasa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Serikali yetu ya Awamu ya Sita. Tunayo *program* kubwa ambayo inaendelea hivi sasa ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kukopesha boti za kisasa takribani 150 hadi 160 kwa wavuvi wote nchini, wale watakaokidhi vigezo. Boti hizi zitakuwa na vifaa kama vile *fish finder* kwa maana ya kile kifaa cha kujua Samaki walipo, vilevile eneo la kuhifadhia samaki takribani tani moja hadi tani moja na nusu, *GPS* na zitakuwa zimeunganishwa katika Satelite ili mvuvi kabla hajatoka kwenda katika uvuvi awe tayari na picha ya kujua mahali walipo samaki. Ahsante.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Constantine

**7 NOVEMBA, 2022**

John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Ujenzi wa Uwanja wa Kisasa wa Michezo - Geita Mjini**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Je, ni upi mchango wa Serikali Kuu katika ujenzi wa Uwanja wa Kisasa wa Michezo wa Halmashauri ya Mji wa Geita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Taifa ya mwaka 1995 Ibara ya 7(1) mpaka (7), jukumu la ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya michezo ni jukumu la Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na watu binafsi. Hata hivyo, tunaipongeza Halmashauri ya Geita Mji kwa ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu ambao umefikia asilimia 75. Hivyo napenda kutoa wito kwa halmashauri zote nchini kuiga mfano wa Halmashauri ya Geita Mji kwa kujenga fedha kutoka mapato yao ya ndani kwa ajili ya kujenga na kukarabati miundombinu ya michezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ipo tayari kutoa mchango wa ushauri wa

**7 NOVEMBA, 2022**

kitaalamu katika ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo unaojengwa katika Halmshauri ya Geita Mji, pale itakapohitajika kama ilivyofanya katika halmashauri kadhaa nchini ikiwemo Halmashauri ya Chalinze, Tunduma, Ruangwa na Taasisi kama vile Bandari na Gymkhana. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Michezo Nchini. Sasa nataka kufahamu tu kwamba majukumu makubwa ya fungu hilo ilikuwa ni pamoja na kuunga mkono juhudi zinazoendelea mikoani za ujenzi wa viwanja: Je, ni Shilingi ngapi ambazo Wizara inaweza kuipatia Halmashauri ya Mji wa Geita?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa Tanzania imekuwa haipati matokeo yanayoridhisha inapokwenda kwenye michezo mbalimbali nje ya nchi; na hii inasababishwa na kukosekana kwa mpango na mkakati unaopimika wa kuendeleza michezo nchini: Ni upi mpango wa haraka ambao wizara inao ili kuweza kujikwamua kwenye eneo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba sasa nijibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza Mheshimiwa Kanyasu anapenda kufahamu ni kwamba Bunge hili lilitupitishia fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Michezo na hadi sasa ni shilingi ngapi zimetumika lakini pia kama tunaweza kuwasidia Geita Mji katika ujenzi wa uwanja ule.

Mheshimiwa Spika, tushukuru Bunge hili Tukufu na Mheshimiwa Rais kwa kutupatia fedha hizi, ambazo zimetusaidia sana kwenye Timu za Taifa ambapo mmeona kwa kiasi kikubwa sana wameletea heshima Taifa letu. Sisi kama Wizara tulivyoomba fedha hizi, lengo kubwa lilikuwa ni kujenga viwanja vya kitaifa ambavyo vitasaidia vijana wetu ambao wametoka kwenye ngazi za chini kuweza kucheza kwenye viwanja vizuri. Jukumu hilo tumeanza, lakini na Halmashauri ya Geita hatujaiacha, tumewapa maelekezo mbalimbali ili waandae uwanja huu vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba fedha hizi zitakapokuwa zinatoshwa baada ya timu za Taifa kuhudumiwa, tuko tayari kuendelea ku- *support* jitihada hizi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Kanyasu anapenda kufahamu ni mkakati gani Wizara yetu tumeandaa kwa ajili ya kuhakikisha tunapata wachezaji wazuri kwa ajili ya kuendeleza michezo katika Taifa letu? Kwanza Bunge hili Tukufu mlitupatia Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya Chuo cha Malya ambacho kinatoa mafunzo kwa Makocha wetu. Pia Bunge hili Tukufu mlitupitishia fedha zaidi ya Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya *Academy* 56 nchi nzima ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu amejibu hapa na fedha hizi sisi tumetenga.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaendelea kukarabati viwanja saba vya zaidi ya Shilingi bilioni 10 ambavyo tulivitaja hapa vikiwemo vya Mbeya, Dodoma, Arusha na maeneo mengine kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu na tunawapata wataalam kupitia fedha hizi ambazo mnatutengea.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima sasa aulize swali lake.

Na. 80

### **Hitaji la Kituo cha Askari Wanyamapori Itilima**

**MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Askari Wanyamapori katika Wilaya ya Itilima na maeneo yanayozunguka Pori la Akiba Maswa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Jimbo la Itilima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha ujenzi wa Kituo cha Askari Wanyamapori katika Wilaya ya Itilima

## 7 NOVEMBA, 2022

mwezi Oktoba, 2022. Kituo hicho kipo katika Kijiji cha Longalombogo ambapo kitakuwa na Askari wa Jeshi la Uhifadhi na Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) na kitahudumia zaidi ya vijiji tisa vikiwemo Longalombogo, Nding'ho, Lung'wa, Nyantugutu, Mbogo, Shishani, Pijulu, Ng'walali na Mwamakili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, swali la nyongeza.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawashukuru Wizara kwa majibu mazuri ambayo umeyatoa kulikana na utekelezaji wa kazi waliyoifanya. Nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jukumu kubwa la Wizara ni kuhakikisha wanatoa elimu kwenye maeneo yanayopakana na kandokando ya hifadhi kama vijiji alivyovitaja, lakini kupitia taasisi yake, TAWA aliweza kutoa fedha kwa ajili ya kuanzisha Shule ya Sekondari katika Kijiji cha Nkuyu, Kata ya Nkuyu kwa kushirikiana na wananachi. Sasa Wizara iko tayari kukamilisha ile Sekondari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Njalu Silanga, Mbunge wa Itilima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuliwahi kuweka mradi kwenye shule hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge na tukajenga madarasa manne; nimwahidi tu Mheshimiwa

**7 NOVEMBA, 2022**

Mbunge kwamba tutaenda kumaliza yale maeneo ambayo yamebaki ili shule hii iweze kufanya kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, sasa aulize swali lake.

Na. 81

### **Programu ya kuunda na kurusha Satelaiti Angani**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza programu ya kuunda na kurusha setilaiti?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu Mheshimiwa Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa nchi kuwa na Setilaiti, hivyo, mwaka huu wa fedha Serikali imeanza utaratibu wa awali utakaowezesha kuunda na kurusha setilaiti angani. Ili kuwezesha kufikia azma hiyo, Serikali tayari imeandaa andiko dhana na kuunda timu ya wataalam watakaoshauri aina ya setilaiti



tutakayorusha angani itakayoendana na mahitaji halisi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio kuwa timu hiyo itakamilisha kazi ya uchambuzi kisha kuwasilisha mapendekezo yake Serikalini kwa hatua za kimaamuzi ndani ya mwaka huu wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nina swali dogo la nyongeza kwamba nchi ya Uganda, siku ya jana tarehe 6 imekuwa ni nchi ya 12 katika Afrika kurusha Setilaiti yake angani. Setilaiti ile imeundwa kwa kupitia vijana *ma-engineer* wa Uganda wakishirikiana na nchi ya Japan na Kituo cha Anga cha Marekani: Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha *program* hii ya kuanza kufundisha vijana wetu kwa kushirikiana kama ilivyofanyika Uganda ili tuweze kupata setilaiti ambayo itaundwa na Watanzania halisi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi za Afrika mpaka sasa tuna setilaiti 41 na kuanzia mwaka 2016 ni setilaiti takribani 20 ambazo tayari zimekuwa angani. Katika hizo setilaiti 41 ni tisa tu ambazo zimekuwa *designed, manufactured* na baadaye kupelekwa angani ambazo zina asili ya Kiafrika.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, bado tuna maeneo mengi ya kuendelea kujifunza, lakini kama nilivyojibu katika swali la msingi, Mheshimiwa Rais siku ya tarehe 8 Februari wakati akiwa na kikao kazi na Wakuu wa Mikoa, alielekeza Wizara yetu ili tuone umuhimu sasa wa kuwa na setilaiti yetu. Tayari Wizara yetu imeshaunda timu ya wataalam ambao watakuja kuishauri Serikali aina ya setilaiti itakayoendana na mahitaji ya Watanzania. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Uwekezaji, Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma Mbunge wa Muheza, sasa aulize swali lake.

Na. 82

### **Upatikanaji wa Soko la Machungwa**

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha upatikanaji wa soko la machungwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Jimbo la Muheza, kama ifuatavyo:-

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika ya machungwa ambayo huzalishwa kwa wingi katika Mkoa wa Tanga hususan Wilaya ya Muheza, Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*TanTrade*) imeendelea kutafuta masoko katika nchi mbalimbali, ambapo mwaka 2021/2022 liliweza kupatikana soko la machungwa katika nchi za falme za Kiarabu. Vile vile, Serikali inaendelea kutoa elimu ya ufungashaji na usindikaji wa matunda ya aina zote kwa wazalishaji ili kuyaongezea thamani na kuweza kunufaika na fursa hiyo ndani ya nchi ambayo itaongeza soko kwa matunda yakiwemo machungwa. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pia nashukuru kwa majibu ya Serikali kupitia kwa Naibu Waziri ambayo yananipeleka kwenye maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, wakati huu ambao taratibu mbalimbali zinaendelea za kutafuta masoko kwa ajili ya machungwa, lakini pia kutafuta uwekezaji kwa ajili ya kutengeneza viwanda cha kuchakata matunda: Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kutengeneza vituo vya ukusanyaji, uhifadhi na uuzaji wa machungwa ili kuwapa uhakika wa sehemu ya kuuzia machungwa yao wananchi wa Wilaya ya Muheza na pia kuepusha idadi kubwa ya machungwa yanayoharibika kila mwaka kwa kukosa uhifadhi mzuri?

Mheshimiwa Spika, la pili,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwinjuma, umeshauliza maswali mawili katika moja. Kwa hiyo, hilo litakuwa ni la tatu sasa.

**7 NOVEMBA, 2022**

Naibu Waziri, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana kuhusiana na soko la machungwa katika Mkoa wa Tanga Wilayani Muheza. Niseme kweli, machungwa ya Muheza ni ya aina yake kwa maana ya ladha; ni matamu kuliko; kwa hiyo, unaweza ukayatenganisha kuliko ya maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeanza mpango wa kujenga maghala ambayo yatakuwa kama vituo vya kukusanyia matunda ili kuhakikisha matunda hayapotei. Siyo maghala tu, yatakuwa ni maghala ambayo yatakuwa na vyumba vya ubaridi (*cold rooms*) ambavyo vitawasaidia wakulima kutunza mazao yao, yakae kwa muda mrefu wakati wanatafuta masoko.

Mheshimiwa Spika, moja ya jitihada kama nilivyosema ni kujenga viwanda vya kuchakata matunda ya machungwa, lakini tunavutia viwanda vidogo na vikubwa. Tumeshianza kujenga viwanda vidogo kupitia vikundi vidogo vidogo ambavyo vitaongeza thamani. Pia tumeshianza kuongea na wawekezaji wakubwa ambao wataenda kuwekeza kwenye eneo la Muheza kwa kuwapa vivutio maalum maana wengi wanataka kuwekeza mjini badala ya mashambani ambako ndiko kwenye machungwa. Kwa hiyo, tutaweka mkakati

**7 NOVEMBA, 2022**

maalum wa kuwavutia ili wapate vivutio vya kuwekeza katika Mkoa wa Tanga hususan Muheza. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na 83

### **Hitaji la Mahakama ya Wilaya Korogwe**

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, ni lini Mahakama ya Wilaya ya Korogwe itajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania inaendelea kutekeleza mpango wake wa miaka mitano wa Ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali. Kutokana na mpango huo wa Mahakama, jengo la Mahakama ya Wilaya ya Korogwe, limepangwa kujengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Mahakama ya Tanzania ipo katika mpango wake wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama zake hapa nchini. Hivyo basi, ujenzi wa Mahakama za Makao Makuu ya Tarafa zote nchini utakamilika ifikapo 2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini kwa sasa hivi hatuna Mahakama ya Wilaya na shughuli za Mahakama ya Wilaya zinafanyika kwenye Mahakama yetu mojawapo ya Mwanzo ambayo haikidhi mahitaji ya Mahakama ya Wilaya: Huoni kuna haja sasa ya Serikali kuharakisha ujenzi wa Mahakama yetu ya Wilaya ya Korogwe? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza shughuli za Mahakama ya Wilaya ambazo zilitakiwa zifanywe na Mahakama ya Wilaya katika Wilaya ya Korogwe, mwanzo zilikuwa zinafanyika katika ofisi ndogo sana ya Mkuu wa Wilaya ya Korogwe. Kwa sasa tumeweza kukarabati jengo ambalo tumepewa na Halmashauri ya Korogwe ambalo kimsingi linakidhi mahitaji ya Mahakama hiyo. Hivyo basi, kama tulivyokwisha toa maelezo ya msingi kwenye jibu la msingi kwamba, ifikapo kipindi kijacho cha fedha, tunakwenda

**7 NOVEMBA, 2022**

kuanzisha ujenzi wa Mahakama ambayo sasa itakuwa ni ya Wilaya ya Korogwe. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Boniphance Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 84

**Hitaji la Masoko ya Mtama na Uwele**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawatafutia wakulima wa Kishapu Masoko ya Mazao ya Mtama na Uwele?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la mahitaji ya zao la mtama na uwele kwa ajili ya matumizi ya viwanda vya ndani ya nje ya nchi. Kutokana na ongezeko la mahitaji hayo, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali kuhakikisha wakulima wa mazao hayo wanapata masoko ya uhakika.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo ni pamoja na kuzalisha mbegu bora zinazokidhi mahitaji ya soko, kuwaunganisha wakulima na wanunuzi wa ndani kama TBL ambao wameanza kununua mazao haya katika Mikoa ya Dodoma na Manyara na kufungua Vituo vya Mauzo katika Mji wa Juba, Sudan Kusini na Lubumbashi Nchini Congo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; changamoto bado ni kubwa sana hususani soko la ndani kwa wakulima wa zao la mtama na uwele. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba yenyewe inashughulika kununua mazao haya kupitia NFRA ili mradi kupunguza tatizo la changamoto ya soko la ndani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna tatizo kubwa la ndege aina ya kwelea kwelea ambao wamekuwa wakishambulia sana mazao haya ya mtama pamoja na uwele na Serikali yetu ina tatizo la kutokuwa na ndege ambayo ni maalum kwa ajili ya kushughulikia ndege hawa waharibifu wa mazao haya. Je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha kwamba inanunua ndege yake ili mradi iweze kushughulika kwa karibu na ndege hawa waharibifu ambao wanashambulia mazao haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya



## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Nyangindu Boniphace Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akiwapambania na kuwasemea wakulima wa mtama pamoja na uwele kutoka Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhakika wa soko la ndani, maelekezo tayari *NFRA* wanayo ya kununua mazao hayo ikiwemo mtama pamoja na uwele. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba *NFRA* anaendelea na zoezi la kununua mtama hivyo wakulima wa Shinyanga ni sehemu ya wanufaika wa soko hili la ndani kupitia *NFRA*.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kuhusiana na ndege. Katika bajeti yetu ya mwaka huu tumetenga Shilingi bilioni tatu ya kununua ndege mpya kwa ajili ya kunyunyizia wadudu kwenye sehemu ya kukuza kilimo anga. Ninavyozungumza hivi sasa tuko katika *due diligence*, tunazo kampuni tatu, mbili kutoka Marekani na moja kutoka Afrika ya Kusini ambako baadaye sasa tutafanya maamuzi ni wapi tununue ndege hiyo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tunayo ndege yetu pia ya *survey* ambayo iko Nairobi Kenya, imekamilishwa matengenezo yake na yenyewe pia itakuja kuungana kuimarisha kilimo anga ili kuondokana na changamoto hii ya wadudu waharibifu.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kasalali Mageni.

**7 NOVEMBA, 2022**

Na. 85

**Kuhakikisha Upatikanaji Bora wa Mbegu za Alizeti**

**MHE. KASALALI E. MAGENI K.n.y. MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za alizeti kwa wakulima ili kuzalisha mafuta ya kula?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbuge wa Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa, nchi yetu inazalisha alizeti itakayo changia kwa kiasi kikubwa katika kuzalisha mafuta ya kula na kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta ya kula, Serikali imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti kwa kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 1,500 zilizokuwepo awali hadi tani 5,000 kwa lengo la kuongeza eneo kubwa zaidi la uzalishaji wa alizeti ili kuweza kufikia malengo; Kuendelea kutekeleza mkakati wa uandaaji wa mashamba makubwa zikiwemo *block farms* ambayo kwa asilimia kubwa yatatumiwa na wakulima kwa kilimo cha alizeti; na Wakala wa Mbegu (ASA) tayari ameanza usambazaji wa mbegu bora ya alizeti aina ya *record* ambayo imethibitishwa ubora na inauzwa kwa bei ya ruzuku ili kuhakikisha kwamba inamletea tija mkulima.

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; Serikali imekiri kwamba imeanza mchakato na inagawa mbegu bora za kilimo cha alizeti kwa wakulima. Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha mbegu hizi zinafika kwenye Jimbo la Sumve kwenye Kata za Lyoma na Malya ambazo zimeonyesha uwezo mkubwa wa kuzalisha alizeti kuliko maeneo mengi ya nchi hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; uzalishaji wa mazao haya ya alizeti na upelekaji wa mbegu bora unategemea pia upatikanaji wa mbolea. Katika Jimbo la Sumve mbolea ya ruzuku ambayo tunaitegemea sana kwa mazao haya mpaka sasa haipatikani. Je, ni nini tamko la Serikali juu ya upatikanaji wa mbolea hii ya ruzuku ambayo imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa wakulima wetu?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa unampa nani taarifa? Yeye ameuliza swali lake kwa Waziri. Unataka kumsaidia Waziri kujibu?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kwenye maelezo yake ndiyo nataka nimpe taarifa.

**SPIKA:** Hapana hairuhusiwi. Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**7 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kuhusu mbegu bora za alizeti kuwafikia wakulima wake, nikitoka hapa nakwenda kumpigia simu na kumwelekeza Mtendaji Mkuu wa ASA ahakikishe wakulima wa Sumve na wenyewe wanapata mbegu bora hii ya alizeti.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu mbolea, ni kweli kumekuwepo na changamoto katika mfumo wa usambazaji, lakini tumeshatoa maelekezo kwa ndugu zetu wa CPB ambao wanashirikiana na wadau wengine kuhakikisha kwamba mbolea hii inawafikia wakulima kwa wakati. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, zilikuwepo changamoto, tumeendelea kuzifanyia kazi na muda sio mrefu CPB pamoja na mawakala wengine watasaidia ufikishaji wa mbolea kwa wakulima pasipo na usumbufu wowote kwa wakulima wetu wa Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali fupi.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa nini sasa Serikali isipeleke mbegu bure kabisa kwa wakulima wa alizeti ili waweze kuzalisha alizeti kwa wingi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya mafuta hapa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuona tunaongeza uzalishaji wa zao la alizeti, kila jambo linakwenda kwa hatua. Hatua ya kwanza tumeanza na ruzuku ya kuuza mbegu ya kilo moja kwa Sh.5,000 ambayo katika hali ya kawaida mkulima angepata kwa Sh.35,000 mpaka Sh.40,000. Kwa hiyo kwa hatua hii, ni hatua nzuri ambayo Serikali imeianza na huko mbeleni tutalifikiria ombi la Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba sasa aulize swali lake.

Na. 86

**Mpango wa pembejeo za korosho kupatikana kwa wakati**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha pembejeo za korosho kwa msimu wa mwaka 2022/2023 zinapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya pembejeo za zao la korosho katika msimu wa 2023/2024 ni tani 70,000 za salfa ya unga na lita 3,400,000 za viuatilifu vya maji, mabomba

## 7 NOVEMBA, 2022

10,000 na magunia 6,200,000. Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania inasimamia upatikanaji wa pembejeo za korosho kabla ya msimu kuanza. Tarehe 15 Oktoba, 2022, Kamati ya Ununuzi wa Pembejeo kwa pamoja ilisaini mikataba na kampuni 14 kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea kuratibu zoezi hilo ili kuhakikisha kuwa pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati na bei itakayopangwa kulingana na mahitaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa miaka miwili mfululizo Serikali imekuwa ikiahidi, lakini kiasi kinachotolewa kwa ajili ya usambazaji huwa hakiendani na kile ilichoahidi, hivyo kusababisha upungufu wa pembejeo kwa wakulima. Je, Serikali inatoa kauli gani kwamba ahadi hii ya leo ya pembejeo ya unga na dawa za maji kwamba zote zitapatikana kwa wakati na zote zitafika kwa wakulima?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni ongezeko la pembejeo. Tunatarajia kwamba kutakuwa na ongezeko la uzalishaji wa korosho na tumeona pia kwenye soko la korosho bei inazidi kuporomoka. Je, Serikali ina mkakati gani kwamba ongezeko hili la uzalishaji litaendana na bei nzuri ambayo ina tija kwa mkulima wa korosho? Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**7 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kauli ya Serikali bahati nzuri kwenye kikao cha wadau wa korosho ambacho mimi nilikuwa sehemu ya washiriki na Waheshimiwa Wabunge walikuwepo mle ndani, tumekubaliana kwamba viutilifu vyote na pembejeo zote ziwafikie kabla ya msimu na kwa idadi ambayo Vyama vya Msingi vitakuwa vimewasilisha katika Kamati ile ya Pembejeo. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge na kwamba Serikali itasimamia kuhakikisha viutilifu hivi vinawafikia wakulima kwa wakati ili kuondokana na changamoto ambazo zilikuwa zinawakumba wakulima katika misimu iliyopita.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu namna ambavyo uzalishaji utaongezeka na Serikali imejipangaje katika kuhakikisha kwamba soko linakuwepo? Moja ya mkakati tulionao mkubwa ni kuhakikisha tunawawezesha wabanguaji wadogo ili kuongeza ubanguaji wa korosho ghafi na kutengeneza masoko ya uhakika ya korosho ambayo imechakatwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tumeendelea kutafuta masoko nje ya nchi na wiki iliyopita mimi mwenyewe nimekwenda uwanja wa ndege kusindikiza kontena la korosho iliyobanguliwa ambayo tumepata soko Marekani na kilo moja kule inauzwa 90,000/= ambayo ni uhakika mkubwa kwa mkulima wa korosho. Hivyo mkakati wa Serikali ni kuhakikisha tunawawezesha wabanguaji wadogo na kuwajengea uwezo ili tuachane kuhangaika

## 7 NOVEMBA, 2022

na soko hili la Vietnam na India ambalo limekuwa na changamoto kubwa sana ya bei.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Mniwie radhi wote mliokuwa mmeomba maswali ya nyongeza hapa. Leo hatukuweza kufanya hivyo kwa sababu wageni leo ni wengi sana na tulishakubaliana wageni watangazwe humu ndani. Kwa hiyo hatuwezi kupata vyote viwili kwa wakati mmoja. Kwa hiyo matangazo yatakuwa marefu kidogo leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni 16 wa Bunge kutoka Bunge la Msumbiji ambao ni Wabunge na watumishi wa Bunge hilo waliokuja kwenye ziara ya mafunzo. *(Makofi)*

Sasa hapa itabidi nisome tangazo lao kwa Kiingereza ili yule anayetafsiri aweze kutafsiri kwa urahisi. So, we have Honorable Muanarera Abdallah, *(Member of the Plan and Budget Committee and Head of Delegation)*. Thank you so much. *(Applause)*

We also have Honorable Abdul Gaful Mamade Hossene Issufo, *Member of the Plan and Budget Committee*; Honorable Muanaiamo Pinto Massua, *Member of the Plan and Budget Committee*; Honorable Mirna Isabel Chibuko Valige, *Member of the Plan and Budget Committee*; Honorable Amilcar José Ussene, *Member of the Committee on Agriculture, Economic Activities and Services*; Honorable Gloria Salvador,



**7 NOVEMBA, 2022**

*Member of Agriculture, Economic Activities and Services; Honorable Faruk Osman, Member of the Committee on Agriculture, Economic Activities and Services; and Honorable Afonso Lopes Nipero (Member of the Committee on Constitutional Affairs, Human Right and Legality. Thank you so much. (Applause)*

*We also have Mr. Eduardo Augusto Namburete, Deputy Rapporteur of the Committee on Constitution Affairs and Legality; Mr Carlos Manuel, Deputy Rapporteur on Committee of the Plan and Budget; Mr. Flávio Manuel Martins, Assistants; Mr. Abilio Daquene Siteo, Interpreter; Mr. Dércio Alfazema, Program Director of IMD; Mr. Fidalia Maculuve, IMD Project Manager; Mr. Mohamed Khan, Official from Mozambique Embassy in Tanzania; and Mr. Frank Mwega, Foreign Service Officer from the Ministry of Foreign Affairs and East African Cooperation in Tanzania. Thank you so much. (Applause)*

Haya, sasa tunaanza ya Kiswahili. Tunao pia wageni nane kutoka Bunge la Zambia ambao ni watumishi wa Bunge hilo, waliokuja kwenye ziara ya mafunzo Bungeni wakiongozwa na Ndugu Margaret Mtine, Afisa Utawala Mkuu, Ndugu Doreen Manyoni, Karen Chisenga, Sara Mwale, Anjela Anna Sinkwaya, Carol Ndoti, Cristabela Ntonga na Mundia Kilembe. Hao ndio wageni wetu kutoka Bunge la Zambia na hao ni Watumishi wa Bunge. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali wa kwenu Waheshimiwa Wabunge.

Kwanza Tunao wageni 56 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbalo Waziri wa Katiba na Sheria, ambao ni wanafunzi na Walimu kutoka Shule ya Mtakatifu Joseph

## 7 NOVEMBA, 2022

*Millennium Primary School* ya Jijini Dar es salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 14 wa Mheshimiwa Festo Dugange, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao ni Maafisa Elimu Kata kutoka Wilaya ya Wanging'ombe, Mkoa wa Njombe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni mdogo wake na mtoto wake kutoka Unguja Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 56 wa Mheshimiwa Ritta Kabati, ambayo ni kwaya kuu ya KKKT Luganga Ilula kutoka Kilolo, Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Mchungaji Huruma Bimbiga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 32 wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambao ni Wanakwaya wa Usharika wa Masama Kati KKKT kutoka Hai, Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Diwani Mheshimiwa Jublatue Ndossi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Noah Saputu ambao ni wapiga kura wake kutoka Arumeru Magharibi Jijini Arusha. Karibuni sana. Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni viongozi wa UVCCM kutoka Kilolo Mkoa wa Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunae mgeni wa Mheshimiwa Abbas Tarimba ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

## 7 NOVEMBA, 2022

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Ramadhani Suleiman Ramadhani ambao ni Walimu wa Shule ya Msingi Michakaini kutoka Jimboni kwake Chakechake Kusini Pemba. Karibuni sana. Tunao pia wageni Sita wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani ambao ni wapiga kura wake kutoka Ushetu Mkoani Shinyanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tunao wageni 10 ambao ni Umoja wa Madereva Wanawake wa Serikali kutoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni. Pia yapo matangazo mengine:

Moja; ni tangazo kutoka kwa Katibu, Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo, mbunge uliyesimama ukae, tangazo la muhimu sana hili kwa ajili yenu. Mnatangaziwa na Katibu wa Bunge kwamba Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata barua kutoka Sekreteriati ya Maadili ya Uongozi wa Umma zinazohusu zoezi la kuhakiki rasilimali na madeni waende chumba Namba 20 jengo la Utawala Annex kuazia Saa Tano Asubuhi kwa ajili ya kukutana na Maafisa kutoka Sekretariati ya Maadili ya Uongozi wa Umma. Kwa hivyo, wale wote ambao wamepata barua hizo wasiache kwenda huko.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ambalo linaendana na hili. Waheshimiwa Wabunge mnaozungumza Mheshimiwa Janejelly, Mheshimiwa Florence tusikilizane kwanza, nikiwa nimesimama ninyi mnanisikiliza, kwa sababu siwezi kuwa nimesimama kama

## **7 NOVEMBA, 2022**

sina sababu. Ninapo simama maana yake nina tangazo kwa ajili yenu na ni muhimu mkasikiliza. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge. Mnatangaziwa kuwa kwa Mujibu wa Kifungu cha 9(a) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma sura ya 398, mnatakiwa kujaza Fomu za Tamko la Mali zenu, wake au waume zenu, na Watoto walio chini ya miaka 18, na kuwa mnapswa kuzingatia masharti ya Ibara ya 70(1) na (2) ya Katiba kwa kuwasilisha nakala mbili za taarifa zenu.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnaombwa kujaza fomu hizo kabla ya kumalizika kwa Mkutano wa Tisa wa Bunge ili kukidhi matakwa ya Sheria na Katiba. Aidha fomu hizo zinapatikana kwenye tovuti ya tume ya Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma au mnaweza kupata nakala mango kutoka kwenye ofisi yangu pale juu.

Waheshimiwa Wabunge, niliwaambia msikilize kwa sababu wapo Wabunge ambao hawajazi baadae wanakuja kutoa maelezo kwamba walisahau, walipitiwa na mambo kama hayo. Kwa hiyo ni muhimu sana tuzingatie ushauri wa Katibu kwamba ni bora kujaza ukiwa hapa Bungeni ukitoka hapa ukienda huko kwa wapiga kura usiwe unawaza fomu kwa sababu mwisho huwa ni Tarehe 31 mwezi Desemba lakini Wabunge wengi huwa mnajisahau, kwa hiyo mmeshauriwa kwenye Bunge hili mjaze fomu hizo mziache hapa kabla hamjasafiri.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa Ofisi ya Katibu wa Bunge inatarajia kuanza kuboresha taarifa za Waheshimiwa Wabunge

**7 NOVEMBA, 2022**

kwenye Bunge mtandao na Bunge message yaani *Bunge SMS* aidha wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamebadili namba za simu bila kuijulisha ofisi ya Katibu wa Bunge na hivyo kushindwa kupata taarifa mbalimbali za Bunge kupitia Bunge mtandao na *Bunge SMS*.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo basi wote mnaombwa kuorodhesha majina yenu matatu kwa usahihi na namba zenu za simu, namba moja tu ambayo inatumika muda wote usiandike namba mbili ama tatu, namba moja ambayo unaitumia muda wote, kwenye fomu maalum zitakazopitishwa na wahudumu ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kuboresha kazi ya utoaji wa taarifa ya Bunge. Fomu hiyo inajieleza kabisa kuna majina hapa kamili hapo, majina matatu, namba ya simu na saini ya Mbunge kwa hiyo itakapo kuwa inapita hiyo karatasi Waheshimiwa Wabunge tutoe ushirikiano.

Waheshimiwa Wabunge, hilo ndio lilikuwa tangazo la mwisho, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutofuata Maelekezo ya Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Kamati, nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwa niaba yake Mheshimiwa Mussa Sima.

**7 NOVEMBA, 2022**

**MHE. MUSSA R. SIMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti naomba kusoma taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutokufuata maelekezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe Mosi Novemba, 2022, Bunge lilijadili hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa Mbunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 54 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Hoja hiyo ilitokana na kuwepo kwa malalamiko ya Wanafunzi wenye vigezo vya kupata Mikopo ya Elimu ya Juu ambao wamekosa mikopo hiyo na kushindwa kuendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja hiyo kutolewa Waheshimiwa Wabunge kadhaa walichangia akiwemo Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda. Wakati akitoa maelezo yake Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inamkwamisha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kauli hiyo, ulielekeza kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ifike mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii siku ya Ijumaa Tarehe 04 Novemba, 2022 saa Saba kamili Mchana ili Kamati iisikilize Bodi hiyo na kujua sababu za Bodi kutokusikiliza maelekezo wanayopewa. Taarifa hii inaeleza yaliyotokana na kikao hicho.

## **7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, njia zilizotumika. Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, imeweka masharti kwa taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni kubainisha njia au mbinu zinazotumika kutekeleza majukumu yanayoripotiwa. Kwa msingi huo, naomba kubainisha njia zilizotumika na msingi wake. Njia kuu mbili zilizotumika ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, njia ya kwanza ni mahojiano. Mnamo Tarehe 04 Novemba, 2022, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Waziri pamoja na Uongozi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa nyakati tofauti. Lengo lilikuwa ni kupata maelezo ya kina kwa njia ya mahojiano. Wakati wa kusikiliza maelezo hayo, Kamati ilijikita katika kutafuta mambo yanayosababisha Bodi hiyo kutokusiliza maelekezo yaliyotolewa na Waziri. Msingi wa msukumo huo ni maelekezo maalumu kwa Kamati yaliyotolewa katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Tisa wa Bunge, Tarehe 01 Novemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya nyaraka. Njia ya pili iliyotumika kutekeleza jukumu uliloipatia Kamati hii mapitio ya nyaraka zilizohusu mawasiliano kati ya Wizara na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu pamoja na mawasilisho yaliyowekwa mbele ya Kamati. Msingi wa njia hiyo unatokana na sehemu kubwa ya utaratibu wa mawasilisho, maelekezo na miongozo katika Taasisi za Umma kutofanyika kwa njia ya maandishi.

Hivyo, mapitio ya nyaraka yaliwezesha upatikanaji wa taarifa za nyongeza pamoja na uthibitisho wa maelekezo yaliyotolewa. Miongoni mwa nyaraka zilizopitiwa ni: -

## 7 NOVEMBA, 2022

(a) Barua ya Bodi kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye Kumbukumbu Namba AC.97/193/01/9 ya Tarehe 12 Septemba, 2022 kuhusu Bodi kupendekeza maboresho ya Hadidu za Rejea (*Terms of Reference*).

(b) Barua kutoka kwa Profesa Allen Mushi, Mwenyekiti wa Kamati ambaye pia ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe yenye Kumbukumbu Namba MU/OF/HELSEB/2 ya Tarehe 26 Oktoba, 2022 iliyothibitisha utayari wa timu ya Mheshimiwa Waziri wa kuanza kazi rasmi Jumatatu, tarehe 31 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati ilikutana na kufanya mahojiano na Uongozi wa Wizara, Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Bodi ya Mikopo. Orodha ya waliohudhuria na kushiriki mahojiano ni:-

- (a) Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Mbunge, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;
- (b) Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Mbunge, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;
- (c) Ndugu Francis Michael, Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;
- (d) Profesa Hamisi Dihenga, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; na
- (e) Ndugu Abdul-Razaq Badru, Mkurugenzi Mtendaji, Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, muundo wa taarifa. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia vizuri wasilisho langu, naomba kulijulisha Bunge muundo wa taarifa hii. Kimaudhui, taarifa hii inatoa maelezo ya jumla na matokeo ya kazi iliyofanyika. Vilevile inabainisha



## 7 NOVEMBA, 2022

uchambuzi na kutoa maoni, mapendekezo na kuhitimisha kwa kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya mahojiano na mapitio ya nyaraka. Waziri aliieleza Kamati kwamba msingi wa kauli yake ulitokana na kuchelewa kuanza kazi kwa Kamati aliyoionda kwa ajili ya kuangalia mifumo ya utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu na kuonekana kwa nyaraka za siri kwenye mitandao ya kijamii. Hata hivyo, Waziri aliieleza Kamati kuwa pamoja na kwamba alitoa kauli hiyo, lakini hana tatizo na Bodi na kwamba ana mamlaka ya kuisimamia na kuelekeza Bodi hiyo na Bodi inatoa ushirikiano wa Kamati aliyoionda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Bodi ya Mikopo yaliyofafanua kwamba, wamekuwa wakitekeleza maagizo yote ya Waziri yakiwemo maelekezo ya kutoa ushirikiano kwa Kamati ya Wajumbe watatu iliyoundwa na Waziri kushughulikia changamoto ya mifumo ya utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu. Aidha, maelezo ya Bodi yalifafanua zaidi kwamba Kamati iliyoundwa na Waziri ilitambulishwa kwa Bodi mnamo Tarehe 12 Julai, 2022 pasipokuwa na barua rasmi za uteuzi pamoja na hadidu za rejea. Kwa msingi huo, Bodi haikuweza kuanza kufanya kazi na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Bodi ilifafanua kuwa mnamo Tarehe 31 Agosti, 2022 walipokea barua za uteuzi wa Wajumbe wa Kamati hiyo ambazo pia hazikuwa na hadidu za rejea. Hadidu za rejea zilitumwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo kupitia barua pepe ya Tarehe 09 Septemba, 2022 na baada ya hapo mnamo Tarehe 11 Septemba, 2022 Bodi ya Mikopo iliitisha Kikao cha Bodi ya Wakurugenzi ambacho kilipendekeza nyongeza ya hadidu za rejea na muda wa Kamati kufanya kazi kutoka

## 7 NOVEMBA, 2022

siku 14 zilizopendekezwa na Waziri mpaka angalau siku 21 au siku 30.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa matokeo. Kamati ilitathmini maelezo ya pande mbili, upande wa Waziri na maelezo na mawasilisho ya Bodi. Katika uchambuzi huo, Kamati ilitaka kujiridhisha na changamoto kubwa iliyopo kuhusu Bodi kusikiliza au kutokusikiliza maelekezo yaliyotolewa na Waziri. Kamati ilipitia tena maelezo ya Waziri aliyoyatoa Bungeni na kwenye Kamati kwa lengo la kumuelewa vizuri kuhusu kuzingatiwa au kutokuzingatiwa kwa maelekezo yake kwa Bodi. Katika maelezo aliyoyatoa Bungeni, Mheshimiwa Waziri alisema na ninanukuu: “...mimi nilichogundua, baada ya kuunda hii Tume, Kamati siyo Tume, resistance ambayo ilikuwepo ya kuzuia isifanye kazi imenishawishi kwamba huenda kuna madudu makubwa sana katika Bodi...” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, maelezo ya Waziri kwenye Kamati hayakuonesha wazi kwamba analalamika kutokusikilizwa kwa maelekezo yake, muonekano huo wa maelezo hautofautiani na nukuu ya maelezo yake Bungeni, kwenye nukuu limetumika neno *resistance* kuonesha namna Bodi ilivyopokea Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri. Neno hilo limetumika kumaanisha kwamba maelezo ya Waziri hayakutekelezwa vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati wa kikao cha Kamati Waziri alisema kuwa hana tatizo na Bodi na kwamba maelekezo yake yametokelezwa na ana mamlaka ya kuisimamia na kuelekeza Bodi. Bodi nayo kwa upande wake haikuonesha ugumu wa kusikiliza maelekezo ya Waziri, badala yake imekuwa ikifuata maelekezo yote

## 7 NOVEMBA, 2022

yanayotolewa na Waziri. Hata hivyo, katika suala la Kamati iliyoundwa na Waziri, Bodi ilitekeleza mara tu baada ya kupokea barua za uteuzi wa Wajumbe ambazo pia zingeweza kuonesha hadidu za rejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa tathmini hiyo, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba:-

(a) Kamati haijapata ushahidi wowote unaoonesha kwamba Bodi ilileta kiburi na kukwamisha utendaji wa Waziri.

(b) Baada ya hadidu za rejea kuwasilishwa Bodi ya Mikopo Kamati imeanza na kuendelea kufanya kazi, jambo lililoashiria kutekelezwa kwa maelekezo ya Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo yanadhihirisha uwepo kwa changamoto ya mawasiliano na mahusiano katika maeneo mawili ambayo ninayataja:-

(a) Ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na

(b) Baina ya Wizara na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya mawasiliano ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imedhihirika kutokana na muda uliotumika kutekeleza maelekezo ya Waziri. Waziri aliunda Kamati hiyo Tarehe 12 Julai, 2022 lakini barua za uteuzi kutoka Wizarani zilisainiwa Tarehe 31 Agosti, 2022. Imechukua takribani mwezi mmoja na nusu kwa uamuzi uliotolewa na Waziri

## 7 NOVEMBA, 2022

kutotekelezwa kwa kuandika barua. Isingekuwa tatizo la mawasiliano ndani ya Wizara, isingefikia hatua ya Waziri kuona kama kuna *resistance*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mawasiliano baina ya Wizara na Bodi, changamoto hiyo inaonekana katika hatua zilizopaswa kuchukuliwa na Bodi baada ya kupokea maelekezo ya Waziri aliyoyatoa kwa mdomo akiwa Ofisi za Bodi hiyo. Katika hali ya kawaida, haikuwa ni kosa kwa Bodi kuanzisha mawasiliano rasmi na Waziri baada ya kuona umepita muda mrefu bila kupokea barua kutoka Wizarani. Iwapo changamoto hiyo isingelikuwepo, bila shaka Bodi ingekumbushia barua na tatizo la *resistance* lisingeliripotwa.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo. Kwa ujumla suala la kukwamisha utekelezaji wa maelekezo ya Waziri halijabainika. Hata hivyo, changamoto za mawasiliano zilizobainika zinahitaji kupatiwa ufumbuzi. Umuhimu wa ufumbuzi kwa changamoto hizo unatokana na nafasi ya Bodi, nafasi ya Waziri na Watendaji wa Wizara kufanikisha azma ya kuundwa kwa Bodi. Kwa msingi huo, Kamati inapendekeza yafuatavyo:-

(a) Mawasiliano kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yaboreshwe ili maelekezo ya viongozi wa sera na wasimamizi wa utekelezaji wa maelekezo ya kisera yaratiwiwe kwa ufanisi na tija.

(b) Kamati iliyoungwa na Waziri iendelee kufanya kazi yake ambayo imeonekana kuwa na tija. Ufanisi wake unategemea ushirikiano itakaoupata kutoka Bodi na Wizara pamoja na miongozo na mawasiliano bora baina ya Bodi na Wizara kwa upande mmoja na Kamati hiyo kwa upande mwingine.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, msingi wa changamoto ambayo tumeshughulikia ni ufinyu wa bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, hivyo Kamati imesisitiza suluhu ya changamoto hii ni kuongezwa kwa bajeti ili wanafunzi wote wanaostahili kupata mikopo waweze kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa mara nyingine napenda kutoa shukurani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha taarifa hii ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Huduma ya Mendeleo ya Jamii pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Aloyce Kamamba pamoja pia na Sekretarieti nzima na viongozi wote ambao wameshiriki katika zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Nanelwa Mwihambi, *ndc*, kwa kuielekeza Kamati kutekeleza majukumu yake vyema, pamoja naye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge, Ndugu Athumani Hussein, *ndc*, na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili kwa ushirikano wanayoipa Kamati yetu wakati wote. Aidha, tunawashukuru sana Sekretarieti na Kamati kwa utendaji, wao waliwezesha kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU KUTOKUFUATA MAELEKEZO YA**

**7 NOVEMBA, 2022**

## **WAZIRI WA ELIMU SAYANASI NA TEKNOLOJIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

### **1.0 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 01 Novemba, 2022, Bunge lilijadili Hoja iliyowasilishwa na Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa (Mb) kwa mujibu wa Kanuni ya 54 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Hoja hiyo ilitokana na kuwepo kwa malalamiko ya wanafunzi wenye vigezo vya kupata mikopo ya Elimu ya Juu ambao wamekosa mikopo hiyo na kushindwa kuendelea na masomo yao.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Hoja hiyo kutolewa, Waheshimiwa Wabunge kadhaa walichangia akiwemo Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda. Wakati akitoa maelezo yake Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inamkwamisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na kauli hiyo, ulielekeza kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ifike mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii siku ya Ijumaa tarehe 04 Novemba, 2022 Saa Saba Kamili mchana ili Kamati iisikilize Bodi hiyo na kujua sababu za Bodi kutokusikiliza maelekezo wanayopewa. Taarifa hii inaeleza yaliyotokana na kikao hicho.

### **1.1 Njia zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, imeweka masharti kwa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni kubainisha njia au mbinu zilizotumika kutekeleza majukumu yanayoripotiwa. Kwa

msingi huo, naomba kubainisha njia zilizotumika na msingi wake. Njia kuu mbili zilizotumika ni kama ifuatavyo:-

### **1.1.1 Mahojiano**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 4 Novemba, 2022, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Waziri pamoja na Uongozi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa nyakati tofauti. Lengo lilikuwa ni kupata maelezo ya kina kwa njia ya mahojiano. Wakati wa kusikiliza maelezo hayo, Kamati ilijikita katika kutafuta mambo yanayosababisha Bodi hiyo kutokusiliza maelekezo yanayotolewa na Waziri. Msingi wa msukumo huo ni maelekezo maalumu kwa Kamati yaliyotolewa katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Tisa wa Bunge, Tarehe 01 Novemba, 2022.

### **1.1.2 Mapitio ya Nyaraka**

**Mheshimiwa Spika**, njia ya pili iliyotumika kutekeleza jukumu uliloipatia Kamati hii ni mapitio ya nyaraka zinazohusu mawasiliano kati ya Wizara na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu pamoja na mawasilisho yaliyowekwa mbele ya Kamati. Msingi wa njia hiyo unatokana na sehemu kubwa ya utaratibu wa mawasiliano, maelekezo na miongozo katika taasisi za umma kufanyika kwa njia ya maandishi. Hivyo, mapitio ya nyaraka yaliwezesha upatikanaji wa taarifa za nyongeza pamoja na uthibitisho wa maelezo yaliyotolewa. Miongoni mwa Nyaraka zilizopitiwa ni:

(a) Barua ya Bodi kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye Kumbukumbu Namba AC.97/193/01/9 ya tarehe 12 Septemba, 2022 kuhusu Bodi kupendekeza maboresho ya Hadidu za Rejea (*Terms of Reference*);

(b) Barua kutoka kwa Prof. Allen Mushi, Mwenyekiti wa Kamati ambaye pia ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu

## 7 NOVEMBA, 2022

cha Mzumbe, yenye Kumbukumbu Namba MU/OF/HELSEB/2 tarehe 26 Oktoba, 2022 iliyohibitisha utayari wa Timu ya Mheshimiwa Waziri wa kuanza kazi rasmi Jumatatu, tarehe 31 Oktoba, 2022;

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati ilikutana na kufanya mahojiano na Uongozi wa Wizara, Bodi ya Wakurugenzi na Menejiment ya Bodi ya Mikopo. Orodha ya waliohudhuria na kushiriki mahojiano ni:

- (a) Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda, Mb, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;
- (a) Mhe. Omari Juma Kipanga, Mb, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;
- (b) Ndg. Fransis Michael, Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;
- (c) Prof. Hamisi Dihenga, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; na
- (d) Ndg. Abdul-Razaq Badru, Mkurugenzi Mtendaji, Bodi ya Mikopo.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia vizuri wasilisho langu, naomba kulijulisha Bunge muundo wa Taarifa hii. Kimaudhui, Taarifa hii inatoa maelezo ya Jumla na matokeo ya kazi iliyofanyika. Vilevile, inabainisha uchambuzi na kutoa maoni, mapendekezo na kuhitimisha kwa kutoa hoja.



## **2.0 Matokeo ya Mahojiano na Mapitio ya Nyaraka**

**Mheshimiwa Spika**, Waziri alieleza Kamati kwamba, msingi wa kauli yake ulitokana na kuchelewa kuanza kazi kwa Kamati aliyoiunda kwa ajili ya kuangalia mifumo ya utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu na kuonekana kwa nyaraka za siri kwenye mitandao ya kijamii. Hata hivyo, Waziri alieleza Kamati kuwa pamoja na kwamba alitoa kauli hiyo lakini hana tatizo na Bodi, na kwamba ana mamlaka ya kuisimamia na kuielekeza Bodi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea maelezo ya Bodi ya Mikopo yaliyofafanua kwamba, wamekuwa wakitekeleza maagizo yote ya Waziri yakiwemo maelekezo ya kutoa ushirikiano kwa Kamati ya Wajumbe Watatu iliyoungwa na Waziri kushughulikia changamoto ya mifumo ya utoaji wa mikopo ya elimu ya juu. Aidha, maelezo ya Bodi yalifafanua zaidi kwamba, Kamati iliyoungwa na Waziri ilitambulishwa kwa Bodi mnamo tarehe 12 Julai, 2022 pasipokuwa na barua rasmi za uteuzi pamoja na hadidu za rejea. Kwa msingi huo, Bodi haikuweza kuanza kufanya kazi na Kamati hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Bodi ilifafanua kuwa, mnamo tarehe 31 Agosti, 2022 walipokea barua za uteuzi wa Wajumbe wa Kamati hiyo ambazo pia hazikuwa na hadidu za rejea. Hadidu za rejea zilitumwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo kupitia baruapepe tarehe 9 Septemba, 2022, na baada ya hapo mnamo tarehe 11 Septemba, 2022 Bodi ya Mikopo iliitisha Kikao cha Bodi ya Wakurugenzi ambacho kilipendekeza nyongeza ya hadidu za rejea na muda wa Kamati kufanya kazi kutoka siku kumi na nne zilizopendekezwa na Waziri mpaka angalau siku ishirini na moja au siku thelathini.

## **3.0 Uchambuzi wa Matokeo**

**7 NOVEMBA, 2022**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitathmini maelezo ya pande mbili: Upande wa Waziri na Maelezo na mawasilisho ya Bodi. Katika uchambuzi huo, Kamati ilitaka kujiridhisha na changamoto kubwa iliyopo kuhusu Bodi kusikiliza au kutokusikiliza maelekezo yanayotolewa na Waziri. Kamati ilipitia tena maelezo ya Waziri aliyoyatoa Bungeni na kwenye Kamati kwa lengo la kumuelewa vizuri kuhusu kuzingatiwa au kutokuzingatiwa kwa maelekezo yake kwa Bodi. Katika maelezo aliyoyatoa Bungeni, Mheshimiwa Waziri alisema: -

*“... Mimi nilichogundua, baada ya kuunda hii Tume, Kamati sio Tume, **resistance** ambayo ilikuwepo ya kuzuia isifanye kazi imenishawishi kwamba huenda kuna madudu makubwa sana katika Bodi...”*

Aidha, maelezo ya Waziri kwenye Kamati hayakuonesha wazi kwamba analalamika kutokusikilizwa kwa maelekezo yake. Muonekano huo wa maelezo hautofautiani na nukuu ya maelezo yake Bungeni. Kwenye nukuu limetumika neno “**resistance**” kuonesha namna Bodi ilivyopokea Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri. Neno hilo limetumika kumaanisha utekelekezaji wa maelekezo kwa kujivuta.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa kikao cha Kamati Waziri alisema kuwa hana tatizo na Bodi na kwamba ana mamlaka ya kuisimamia na kuielekeza. Bodi nayo kwa upande wake haikuonesha wazi ugumu wa kusikiliza maelekezo ya Waziri, badala yake imekuwa ikifuata maelekezo yote yanayotolewa na Waziri. Hata hivyo katika suala la Kamati iliyoundwa na Waziri, Bodi ilisita kutokana na kuchelewa kupokea barua za uteuzi wa

## 7 NOVEMBA, 2022

Wajumbe ambazo pia zingeweza kuonesha hadidu za rejea.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa tathmini hiyo, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba:

(a) Kamati haijapata ushahidi wowote unaoonesha kwamba Bodi ilileta kiburi na kukwamisha utendaji wa Waziri; na

(b) Baada ya hadidu za rejea kuwasilishwa Bodi ya Mikopo Kamati imeanza na kuendelea kufanya kazi, jambo linaloashiria kutekelezwa kwa maelekezo ya Waziri.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo hayo yanadhihirisha kuwepo kwa changamoto ya mawasiliano na mahusiano katika maeneo mawili ambayo ni:

(a) Ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na

(b) Baina ya Wizara na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu nchini;

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto ya Mawasiliano ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imedhihirika kutokana na muda uliotumika kutekeleza maelekezo ya Waziri. Waziri aliunda Kamati hiyo tarehe 12 Julai, 2022 lakini barua za uteuzi kutoka Wizarani zilisainiwa tarehe 31 Agosti, 2022. Imechukua takriban mwezi mmoja na nusu kwa uamuzi uliotolewa na Waziri kutekelezwa kwa kuandika Barua. Isingelikuwa tatizo la mawasiliano ndani ya Wizara, isingelifikia hatua ya Waziri kuona kama kuna “resistance”.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa mawasiliano baina ya Wizara na Bodi, changamoto hiyo inaonekana katika hatua zilizopaswa kuchukuliwa na Bodi baada ya kupokea maelekezo ya Waziri aliyoyatoa kwa mdomo akiwa ofisi za Bodi hiyo. Katika hali ya kawaida haikuwa ni kosa kwa Bodi kuanzisha mawasiliano rasmi na Wizara baada ya kuona umepita muda mrefu bila kupokea barua kutoka Wizarani. Iwapo changamoto hiyo isingelikuwepo, bila shaka Bodi ingekumbushia barua na tatizo la “resistance” lisingeliripotwa.

#### **4.0 Maoni na Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla suala la kukwamisha utekelezaji wa maelekezo ya Waziri halijabainika. Hata hivyo, changamoto za mawasiliano zilizobainika zinahitaji kupatiwa ufumbuzi. Umuhimu wa ufumbuzi kwa changamoto hizo unatokana na nafasi ya Bodi, nafasi ya Waziri na Watendaji wa Wizara kufanikisha azma ya kuundwa kwa Bodi. Kwa msingi huo Kamati inapendekeza kama ifuatavyo: -

(a) Mawasiliano ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yaboreshwe ili maelekezo ya viongozi wa sera na wasimamizi wa utekelezaji wa maelekezo ya kiseru yaratiwiwe kwa ufanisi na tija;

(b) Kamati iliyoundwa na Waziri iendeele kufanya kazi yake ambayo imeonekana kuwa na tija. Ufanisi wake utategemea ushirikiano itakaoupata kutoka Bodi na Wizara pamoja na miongozo na mawasiliano bora baina ya Bodi na Wizara kwa upande mmoja na Kamati hiyo kwa upande mwingine; na

(c) Msingi wa malalamiko ya wanafunzi wa vyuo vikuu yaliyosababisha hoja iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa

Eng. Ezra Chiwelesa (Mb) ni kupungua kwa bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza. Kamati inasisitiza Serikali itekeleze maagizo ya Bunge ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaostahili mikopo wanapata mikopo hiyo.

## **5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha taarifa hii ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na Mheshimiwa Mhe. Aloyce John Kamamba (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Wajumbe hawa ni wamechapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika vikao. Nawapongeza sana na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Aloyce John Kambamba, Mb, - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Eng. Samweli Hhayuma Xaday, Mb- Mjumbe
5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele - Mjumbe
7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
8. MheKassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Latifa Khamis Juwakali, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Bernadeta K. Mushashu, Mb -Mjumbe
14. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb, - Mjumbe

## 7 NOVEMBA, 2022

15. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb - Mjumbe
17. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb- Mjumbe
18. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb- Mjumbe
19. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb- Mjumbe
25. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Prof. Kitila A. Mkumbo, Mb - Mjumbe
27. Mhe. Anastazia J. Wambura, Mb - Mjumbe
28. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb- Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Nanelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja naye namshukuru Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati yetu wakati wote. Aidha, tunawashukuru sana Sekretarieti ya Kamati kwa utendaji wao uliowezesha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**

6 Novemba, 2022

**7 NOVEMBA, 2022**

*(Hoja iliitolewa lamuliwe)*

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huwa mnajivuta sana kusimama, siku hoja itaondolewa hapa mezani.

Hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Sima kwa wasilisho hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kama Kanuni zetu zinavyotutaka, yapo majina hapa mbele ya Wabunge watakaochangia halafu mtoa hoja atahitimisha hoja yake na kisha mtahojiwa.

Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kama Mjumbe wa Kamati niweze kuchangia.

Kwanza naunga mkono taarifa hiyo, na nataka kuchangia ile sehemu ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, msingi wa changamoto ambayo tumeijadili hapa leo na siku iliyopita; moja, ni ukweli kwamba Waheshimiwa Wabunge pengine kuna haja ya kubadilisha tafsiri ya suala la anayestahili na asiyestahili. Hili ni tatizo ambalo limeendelea kujitokeza; na tulipoongea na bodi walikuwa wazi sana, kwamba kwa

## 7 NOVEMBA, 2022

kweli wanafunzi wengi wanaoomba mikopo ya elimu ya juu wanastahili kupata mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ambayo ipo ni ukweli kwamba bajeti inakuwa haitoshi, ni kama sisi Waheshimiwa Wabunge tunapokwenda kugombea huko, wote wanaogombea wanastahili lakini sasa inabidi warudi watatu. Kwa hiyo, ni lazima utaratibu upatikane wapatikane watatu na hatimaye mmoja, lakini haimaanishi kwamba wale ambao hawakuteuliwa hawastahili.

Kwa hiyo, hata kwenye suala la mikopo tuliona kwa upana wake. Nitawapeni kidogo tathmini, Bodi ya Mikopo inapitia hatua tatu muhimu kabla haijatoa orodha. Kwanza inapokea majina ya watu waliomba, pili wanahakiki. Wakishahakiki wanachukua wale ambao wamepata udahili katika vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mwaka 2021/2022 waliyoomba mikopo walikuwa 88,688, Bodi ikafanya uhakiki, waliokuwa na sifa zile ambazo bodi inazo wakawa 81,654. Hii ina maanisha kwamba kwa vigezo vya Bodi hawa wote walistahili kupata mikopo. Hata hivyo baadaye waliokuwa wamekidhi vigezo vya udahili katika vyuo vikuu na taasisi ya elimu za juu, kwa sababu unaweza ukawa na kigezo cha kukopa kumbe kule katika taasisi ya chuo kikuu haujapata sifa za udahili. Kwa hiyo, waliokidhi wakawa 74,312. Kati ya hawa Bodi iliwapa mikopo wanafunzi 70,603.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utaona kwamba waliokosa hapa ni chini ya wanafunzi 3,000. Mwaka huu hali ikoje; mwaka wa fedha 2022/2023. Waliyoomba wanafunzi 97,760 baada ya uhakiki wa Bodi, waliostahili,



## 7 NOVEMBA, 2022

wenye sifa za Bodi ni wanafunzi 85,876. Baada ya Bodi kufanya uhakiki kwa mujibu wa udahili, wanaostahili mwaka huu ni 80,502; lakini sasa mwaka huu bajeti wanayo kwa wanafunzi wa *first year*, kwa sababu tukumbuke Waheshimiwa Wabunge bajeti ambayo tulipitisha hapa ni bajeti ya shilingi bilioni 570 kama mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu mwaka jana waliongezeka sana, ina maana wanafunzi wanaoendelea, wale waliokuwa wanaendelea haiwezekani ukawatoa lazima uwapate. Kwa hiyo, kwa sababu bajeti ni ile ile, katika wanafunzi 80,502 wanaostahili kupata mikopo mwaka huu, kwa mujibu wa bajeti sio kwa mujibu wa sifa, ni 42,000. Sijui kama mnanipata hapo? Wanafunzi 80,000 wanaostahili au wenye sifa za kupata mikopo na ambao wamefanyiwa uhakiki, lakini bajeti ambayo tunayo ni ya wanafunzi 42,000 ndio ambayo tunayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, takriba wanafunzi 40,000 hawatapata mikopo, kwa hiyo ndiyo maana *messages* zimekuwa nyingi kwetu kuliko mwaka jana. Sasa, huu ndiyo msingi wa changamoto ambayo tunashughulika nayo, na ni muhimu kutibu tatizo badala ya kutibu dalili za tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri kwa taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri alitupa; nadhani baadaye Serikali itapata nafasi ya kueleza kwamba wamewasiliana vizuri na Wizara ya Fedha na kuna maendeleo mazuri naamini kwa maelekezo yako Serikali itatoa maendeleo hapa. *(Makofi)*

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, hiyo ndiyo changamoto, lakini habari njema ni kwamba...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kitila Mkumbo, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

### **T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nilitaka kuongeza mnofu kidogo kwa Mheshimiwa Kitila kwamba lipo tatizo lingine ambalo linafanana na hilo. Kwamba mwanafunzi wa maskini ambaye hana uwezo wa kupeleka karo, amepewa sifa za kupewa mkopo na Bodi ya Mikopo lakini kigezo lazima afanye *registration*, ajisajili kwanza kwenye shule aliyopata ndipo wampe mkopo. Sasa kama hana hela ya kwenda kujisajili, maana yake chuo hakimtambui kama ana pesa za mkopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kigezo nacho kitambulike kwamba kama kuna mwanafunzi maskini ana sifa za kupata mkopo na hana uwezo wa kujisajili, chuo kitambue kwamba mkopo wake wa asilimia mia kama amepewa, basi chuo kikubali apokee hiyo hela. Hela zikija ili aweze kujisajili, lakini wanamzuia, hawawezi kumpa mpaka ajisajili na hela hana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijazungumza na Mheshimiwa Kitila Mkumbo, turejee kwenye hii taarifa ya Kamati. Kwanza nilitoa maelekezo mahususi ni jambo gani ambalo Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii inaenda kulitazama. Haya mengine nilikuwa

## 7 NOVEMBA, 2022

nimemwacha Profesa Mkumbo nilikuwa nasikiliza anaelekea wapi na amesema hoja ya msingi ni wanafunzi kukosa mkopo. Hoja hiyo ni ya msingi, lakini ni kwa ajili ya Bunge linalokuja si Bunge hili na si kwa ajili ya Kamati hii ambayo niliunda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mchanganyiko umekuja kwenye jambo la tatu, Mwenyekiti wa Kamati, nadhani msoma taarifa kwa niaba, hili jambo mliloleta kama (c), hili ndiyo mmelichomeka hapa, linalopelekea Wabunge kuchangia kwa namna ambayo inataka kuzungumza yaani kwa msingi wa kwamba wanafunzi wamekosa mkopo. Kwa hivyo ndiyo hoja iliopo mbele yetu.

Lile azimio lilishapita na mimi nilisema siku ile, hoja za msingi za wanafunzi kukosa ama kupata mkopo zitajadiliwa wakati Kamati hii itakapoleta taarifa yake ya mwaka hapa Bungeni. Kwa sasa hivi hoja iliyokuwa imepelekwa kwenye Kamati ni kuangalia, je, ile Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri haiheshimiwi na Bodi ya Mikopo? Kwa sababu ndiyo hoja iliyokuwa imeletwa hapa na Mheshimiwa Waziri na ninyi mmesoma kwamba maelezo yaliyowapeleka huko kwenye Kamati ni yapi; ni yale ambayo yanayoonesha kwamba Waziri na Bodi ya Mikopo kuna changamoto. Bodi ya Mikopo haisikilizi ama ina ugumu fulani, ndiyo hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Hii hoja ya kupata mikopo ama kutokupatikana, nani anapata nani hapati, vigezo vipi tutumie, tuboreshe wapi, hii ni hoja itakayokuja ama huu ni mjadala utakaokuja kwenye Bunge linalofuata.

Kwa hiyo, tuelewane vizuri na Mheshimiwa Profesa Kitila nadhani utakuwa umenielewa. Wewe ni mjumbe

**7 NOVEMBA, 2022**

wa hii Kamati, hili pendekezo (c) mlilolileta hapa ndilo linaloleta changamoto. Yalipaswa yaje mambo mawili, mliyoyaandika hapa juu, kwamba ni mawasiliano kati ya chombo hiki na chombo hiki na mnapendekezo fulani; lakini tukianza kujadili kwa msingi hakuna hoja iliyoletwa mbele yetu ya kuhusu wanafunzi kupata au kutokupata; vigezo vya kupata au kutokupata na mambo kama hayo. Tutatakuwa hatulielekezi Bunge kwenda kwenye kufanya maamuzi kwenye hoja ile ambayo mimi niliagiza ije kwenye Kamati.

Kwa hiyo wachangiaji wengine pia naamini mtakuwa mmelewa mchango wenu utakuwa kwenye hoja gani. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa muongozo huo mzuri na nitazingatia katika mchango wangu kwa dakika ambazo zimebaki. Tuliona sisi kama Kamati tukitoka hapa bila kugusia msingi wa tatizo, tutakuwa hatujatenda haki, lakini nashukuru kwa maelekezo yako.

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie hilo la kwanza la mawasiliano. Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake na maelezo ya Bodi, alienda kwenye Bodi tarehe 12 Julai akatoa maelekezo na akaitambulisha Kamati ile ambayo ilikuwa ifanye kazi na Bodi wakaipokea.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida, katika utendaji wa Kiserikali, Waziri alishamaliza kazi yake. Ina maanisha kwamba baada ya hapo vyombo vingine vilivyofuata vilitakiwa vifuatilie. Kwa mfano, Waheshimiwa Mawaziri wanafahamu kwamba Katibu wake wa Mheshimiwa Waziri angemwandikia Katibu Mkuu, kwamba alipokuwa kwenye ziara tarehe hii na

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo, moja, mbili, tatu, naomba kuwasilisha kwa utekelezaji, hilo halikufanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Bodi wamekuja kupokea maelekezo rasmi ya Wizara tarehe 31 Agosti. Na kwa kweli kwa ushahidi ya maelezo ya Bodi na nyaraka ambazo waliwasilisha, mara walipopokea maelekezo ya tarehe 31 Agosti walitekeleza lile agizo kwa kasi ambayo hata sisi Wajumbe ilitushangaza. Hata hiyo kazi haijaanza, basi Mwenyekiti wa Kamati ameandika barua Wizarani akieleza kwamba, sasa nimepokea na tupo tayari kuanza kazi tarehe 31 Oktoba, ambayo ni juzi. Bodi baada ya kupata kibali cha Wizara, mara moja walishalipa na hela ya *advance* ya Kamati kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika mazingira hayo, utakuta kwamba Kamati ilipata ugumu *from documentary evidence* kwamba ni lini uweze kuihukumu Bodi kwamba imekwamisha maelekezo ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, kuna changamoto hiyo ya mawasiliano ambayo tumeieleza na tumetoa mapendekezo ambayo tumeyatoa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia mjadala huu

## 7 NOVEMBA, 2022

muhimu sana kwa mstakabali wa Wizara ya Elimu na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, na mimi nataka nielekee moja kwa moja kwenye hadidu ya rejea iliyotokana na maelekezo yako ndani ya Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba maelekezo yaliyokuja kwenye Kamati yalikuwa ni kuona na kusikiliza Wizara pamoja Bodi ya Mikopo kama kuna pingamizi, kuna *resistance* au kuna kupingwa kwa maelekezo ya Wizara. Hata hivyo, kabla sijaendelea nataka kulithibitishia Bunge lako, mimi ni msema kweli na nitasema kweli daima, hakuna chembe chembe za kuzuia au kutokutekelezwa kwa maelekezo ya Wizara kwenye Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri alipofika mbele ya Kamati alieleza kwa uwazi kwamba yeye hana shida na Bodi ya Mikopo. Na maelezo yake alithibitisha kwa kuonesha kwamba yeye ndiyo mwenye mamlaka ya kuiwajibisha Bodi, na kwamba kama kungekuwa na namna yoyote ya kupingwa na Bodi angechukua hatua kwa sababu ipo kwenye mamlaka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini alikwenda mbali zaidi, akasema maelekezo aliyoyatoa yote yalitekelezwa na Bodi, kwa hiyo hakuna suala la *resistance*. Hii inakinzana na maelezo ambayo yalitolewa mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo walithibitisha kwamba siku ambayo Wizara iliitembelea Bodi, ilikuwa ni mwaliko wa Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kwenda kuzindua utaratibu mpya wa utolewaji wa mikopo kwa mwaka 2022/2023. Wakati Wizara imefika kwenye Bodi, ilienda pamoja na Wajumbe wa Kamati ambao Mheshimiwa Waziri aliwateua na Waziri alitoa maelekezo. Kwamba analeta Kamati husika ambayo alitambulisha katika mkutano huo kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa mambo kadhaa, lakini hapakuwa na maandishi.

Mheshimiwa Spika, *government works on paper*, hapakuwa na maelekezo ya kimaandishi kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara kwenda kwenye Bodi kuelekeza namna gani timu hiyo itakwenda kufanya kazi na hadidu za rejea ni zipi. Jambo hilo lilisababisha kuchelewa kutekelezwa kwa maelekezo hayo. Mpaka ilipoandikwa barua, Bodi haikuleta *resistance*, ilitekeleza. Kwa kuthibitisha hayo Bodi iliongeza hadidu za rejea katika hadidu za rejea mbili zilizopelekwa kwenye Bodi na Katibu Mkuu wa Wizara. Hii inatuonesha kwamba Bodi ilikuwa tayari kufanya kazi na Kamati iliyoundwa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini mbali zaidi, Bodi imegharimia gharama za Wajumbe wa Timu ya Uchunguzi kwenye Bodi ya Mikopo, Bodi ndiyo imegharamia. Hii inathibitisha pia kwamba hapakuwa na shida yoyote ya utekelezaji wa maelekezo ya Waziri kwenye Bodi.

Mheshimiwa Spika, shida ambayo tumeiona kubwa ni mawasiliano na mahusiano. Mbele ya Kamati tumethibitishiwa hilo, lakini namna ambavyo taarifa zimekuja pia imeonekana kuna namna fulani ama kuna hofu ndani ya Wizara au kuna hofu inatengenezwa

## 7 NOVEMBA, 2022

kwenye Bodi, jambo ambalo linakwamisha utekelezaji wa majukumu katika maeneo hayo mawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ushauri Wangu; Mheshimiwa Kitila Mkumbo ameeleza vizuri, kwamba kama Waziri angetoa tamko hata kwenye vyombo vya habari, ingekuwa ni ngumu kutekelezwa na Bodi kama hapakwenda maandishi mahsusi kwa ajili ya tamko la Waziri. Na kwa kuwa *machinery* ya Waziri ipo; kuna Katibu Mkuu, kuna Katibu wa Waziri wao wangeweza kushusha yale maelekezo kwa maandishi kwa Bodi ingerahisha utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri na hizi *resistance* ambazo zinazungumziwa leo zisingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kikubwa ambacho naishauri Serikali ni kuimarisha mifumo ya mawasiliano. Kiongozi anapotoa maelekezo kwenye taasisi, wanaohusika kushusha hayo maelekezo kwa maandishi wafanye jambo hilo kwa wakati ili kuondoa hii mikanganyiko ambayo inaweza kutokea na kupoteza muda kama inavyotokea sasa.

Mheshimiwa Spika, utulivu ulio sasa kwenye Bodi ya Mikopo, mtakumbuka takribani miaka sita sasa inatengenezwa na namna ambavyo *machinery* ya Bodi inafanya kazi yake vizuri. Twende mbali zaidi, tusije tukahukumu mtu badala ya mfumo. Mfumo uliopo, Bodi ya Mikopo inatekeleza, inatoa mikopo kwa idadi ya wanafunzi kulingana na kiasi cha bajeti iliyopelekwa. Hapa tunaweza kuizungumzia Bodi kama wameshindwa kuwalipa hao watoto kwa wakati, lakini kama watoto wamelipwa kwa wakati hata kama wangelipwa watoto watatu kulingana na bajeti iliyopelekwa, hilo sio jambo la bodi ni jambo la Serikali kukaa chini, kuangalia namna nzuri ya kuongeza wanufaika wa Bodi kwa maana ya



**7 NOVEMBA, 2022**

kupanua bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuleta tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana naunga mkono hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mheshimiwa Elibariki Kingu ajiandae.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa fursa hii nami nichangie hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza vizuri sana msomaji wa taarifa mbele yetu. Katika taarifa hiyo imeonekana wazi kabisa kwamba Waziri mwenyewe kwa kauli yake kama alivyonukuliwa na muwasilishaji akisema kwamba anajukumu la kuisimamia bodi lakini pili bodi haijakaidi maelekezo yake. Pia *on Hansard* Waziri huyo huyo hapa mbele ya Bunge lako Tukufu, jambo lililopelekea mpaka ukatoa maelekezo aende kwenye Kamati akahojiwe.

Mheshimiwa Spika, pia *on Hansard*, Waziri huyo huyo hapa mbele ya Bunge lako tukufu, jambo lililopelekea mpaka ukatoa maelekezo aende kwenye Kamati akahojiwe na Kamati iwasikilize watu wote, iweze kutuletea taarifa ambayo leo tunaijadili hapa; ulimsikia na tulimsikia sote hapa ndani *on Hansard* akisema kwamba Bodi imeweka *resistance* kubwa, imekataa maelekezo yake na pengine kuna kitu kilichofichika. *(Makofi)*

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, hizi ni kauli tata za Waziri huyu huyu mmoja; moja, ndani ya Bunge, ndani ya Kumbukumbu Rasmi za Bunge; pia kauli nyingine kwenye Kamati na kauli zake zinapingana hata saa 72 hazijapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, ni dhahiri kwamba Waziri amelidanganya Bunge lako Tukufu kwa kusema uongo ndani ya Bunge. Pia uongo aliosema Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni, umeleta taharuki ndani ya Bunge, ndani ya Umma wa Watanzania na zaidi kwa watoto ambao wanasikiliza Bunge kwa matumaini makubwa juu ya hoja yao ya msingi kwamba ni namna gani Serikali yao itawapatia mikopo waendeleo na masomo yao ya elimu ya juu. Kwa hiyo, Waziri hakuwa makini na taarifa ambayo alikuwa anaipeleka kwenye jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utangulizi huo, naomba Waziri aliombe radhi Bunge lako Tukufu; pili, awaombe radhi wananchi kwa kusababisha taharuki kubwa iliyojitokeza; tatu, nilikuwa naomba Waziri mwenyewe ajitathmini kama anatosha kuwa mwakilishi wa Rais kwenye usimamizi wa sekta hii. Kama hii ndiyo taswira anayoipeleka mbele ya Bunge Tukufu na kwa Umma, ajitathmini kama bado ana hadhi na uhalali wa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kwenye nafasi hiyo. Kama akiona hawezi, ampe fursa Mheshimiwa Rais aweke mtu mwingine anayeweza kumsaidia vizuri kwa sababu yeye ni dhahiri ameshindwa kusimamia sekta yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kuaibisha Serikali kuona kwamba Mheshimiwa Waziri anatamka mbele ya Bunge; kwenye Kumbukumbu Rasmi, ndani ya vyombo

**7 NOVEMBA, 2022**

vya habari vyote na Umma wote ukimsikiliza kwamba taasisi anayoisimamia imekaidi maelekezo yake. Hata kama ingekuwa imekaidi, nisingetarajia Waziri wa Serikali kuja kulalamika ndani ya Bunge. Kuna *machinery* za kiutendaji na kiutawala ndani ya Serikali yenyewe za namna ya kuchukua hatua dhidi ya watu wanaokaidi viongozi wao wa juu, watu wanaokaidi maelekezo yanayotolewa na Serikali, kuna namna za kiutawala za kushughulika na mambo hayo na siyo kuja kulalamika Bungeni.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangalla, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

### **T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri samahani. Nilitaka Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla *a-declare interest* kwamba alipokuwa Waziri wa Maliasili na Utalii alikuwa na mgogoro na Katibu Mkuu wake ambaye kwa sasa ni Waziri wa Elimu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, kabla sijakuuliza kuhusu taarifa hiyo ambayo umepewa hapo, ukiacha hayo, nimeletewa taarifa hapa mbele kwamba mambo haya ulishayazungumza mahali, kwa maana ya kwamba umeshaandika kwenye mitandao. Nimeletewa hapa kwamba umeshaandika kwenye mitandao, kwa hiyo, ulishatoa hukumu kabla.

Waheshimiwa Wabunge, sasa changamoto tunayoipata ambayo labda niseme ni kosa letu wote

## 7 NOVEMBA, 2022

kama Bunge. Kanuni zetu za Kudumu za Bunge zinazungumzia maslahi ya kifedha. Maslahi mengine hazizungumzi. Kwa hiyo, hiyo ni changamoto ya kikanuni.

Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri kwamba kwa mahusiano ambayo yapo kwenye jamii, kila mtu anafahamu wala haihitaji kusoma mahali, mahusiano binafsi ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia yanaleta mushkeli kwenye mchango wa Mheshimiwa Mbunge kwamba anasimama sehemu ambayo pengine Wabunge wengine watasimama. Yeye anaweza kuwa alishachukua upande kabla, kwa nini? Kwa ajili ya mahusiano ambayo nchi nzima inajua, wala haina haja ya mtu kusema. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, kabla hajasimama Mheshimiwa Getere utaona nilikuwa nimewasha hapa kisemeo, nilitaka nikueleze haya ili unapochangia, nawe kama kiongozi uwe umejiweka sehemu ambayo unao uwezo wa kusimama katikati kuliko kusimama upande fulani hivi ambao tayari ulishaamuliwa na yale mambo yanayojulikana yaliyo kati yako wewe na Mheshimiwa Prof. Mkenda. Sasa na wewe ukielekea huko, basi yale unayochangia kuhusu Mheshimiwa Prof. Mkenda itakuwa sasa na wewe umechukua upande, naye anao wa kwake.

Kwa hiyo, nadhani tujikite kwenye taarifa ya Kamati, kwa sababu pia Waheshimiwa Wabunge wamenyamaza tu hapa, lakini na unayemzungumzia pengine yeye ni ngumu kusimama kuanza kujisemea, lakini uhalisia ni kwamba taarifa ya Kamati haijasema mahali kwamba Mheshimiwa Waziri alisema uongo. Hakuna mahali, mimi sijapona. Kwa hiyo, wewe umesema amesema uongo,

## 7 NOVEMBA, 2022

lakini Waheshimiwa Wabunge mmenyamaza na kanuni mnazifahamu. Sasa sijui mnataka Spika ndio awe anafanya hilo zoezi!

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla malizia mchango wako kwa kuzingatia misingi hii ambayo imeelezwa hapa. Pia taarifa ya Mheshimiwa Getere, nimefafanua hapa kwamba kanuni zetu zina changamoto hiyo, hazielezi maslahi mengine, zinazungumzia maslahi ya kifedha. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa mwongozo huo. Kiukweli namshukuru pia Mheshimiwa Getere kwa kulileta hili. Sina maslahi yoyote kwenye jambo hili, lakini kiuhalisia ni kwamba tumefika hapo tulipofika kwa sababu Mheshimiwa Waziri ametumia, yaani kufanya *personal attack* dhidi ya Bodi ya Mikopo kuja kulidanganya Bunge, kwamba Bodi imemgomea na vitu kama hivyo, badala ya kutafuta suluhu ya tatizo la msingi ambalo ni bajeti ndogo kwenye mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu huo ambao ulipelekea kwenye hilo ambalo umekuwa ukilisema kwamba yeye anapenda migogoro, ugomvi na ku-*attack* watu binafsi badala ya kufanya kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla tafadhali! Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, tafadhali! Tafadhali! (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nimeshamaliza huko.

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Tuelewane vizuri Waheshimiwa. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, wakati akitoa mchango wake Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo nimeeleza wazi hapa kwamba jambo la msingi kwenye hoja hii ni lipi? Kwa sababu ukisema tu ni kuongeza bajeti; ndiyo maana nimesema mjadala huu bora uelekee Kamati itakapoleta taarifa yake rasmi Bungeni. Kwa nini?

Ukisema hiyo ndiyo sababu pekee ambayo imeundwa hii Kamati, utakuwa unakosea kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wenyewe humu ndani huwa kuna malalamiko kwamba kuna watu wasiostahili huwa wanapewa mkopo na kwamba kuna watu ambao wanapewa mikopo kwa kiasi kikubwa kuliko wanachohitaji. Sasa hayo yote yatatazamwa na nani kama siyo jicho tofauti ndiyo likayatazame hayo?

Kwa hiyo, hoja siyo kutosheleza tu kwa kiasi cha fedha. Fedha zingeweza kutosha, yaani kwa maana ya uhitaji wa wale wanafunzi, lakini bado wakapewa wale ambao tunaona kwamba hawa kwa kweli hawakupaswa kupewa. Kwa hiyo, tatizo bado litakuwepo. Kwa hiyo, nasi tusilipeleke kwa namna hiyo.

Sasa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla naona mchango wako unakoendelea unaanza sasa na kufanya jambo ambalo wewe unajaribu kulikataa. Maana unaposema amefanya *personal attack*, kwa nani? Kwa sababu kile ni chombo na ni taasisi; leo aliyepo yupo, kesho hatakuwepo. Kwa hiyo, hiyo hoja yako kidogo inanipelekea kufanya maamuzi ambayo nisingependa kuyafanya katika mazingira haya.

**7 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla nadhani umechangia, yamekutosha hayo. Atafuatia Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, na Mheshimiwa Elibariki Kingu, ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia ajenda ambayo Kamati imeleta. Kimsingi nami naiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, kuna haja sasa baada ya haya kutokea, kuona umuhimu wa Mawaziri na Makatibu Wakuu kufanya wajibu wao kitaasisi. Nafikiri Mheshimiwa Waziri alipokwenda kuitambulisha ile timu aliyoichagua kwa bodi, kimsingi tu Katibu ilikuwa achukue jukumu la kuendelea kufanya shughuli za kiofisi na kuandika barua, ndivyo ninavyoona mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninalo swali dogo tu kwamba, kwa nini hii bodi iliamua kuilipa fedha Kamati hiyo? Kwa sababu kama timu imechaguliwa kuja kukuchunguza, halafu unaenda kuilipa fedha, hakuna kitu ambacho kama unashawishi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najaribu tu kujuliza kwa sauti labda kama sijaiielewa Kamati. Kwa sababu wewe unaenda kuchunguzwa, halafu wewe bodi unatoa fedha kwenye hiyo timu; huoni kama kuna tatizo hapo? Kwa hiyo, hilo tu peke yake nilikuwa nalifikiria...*(Makofi)*

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**7 NOVEMBA, 2022**

**T A A R I F A**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilitaka nimpe taarifa dada yangu Mheshimiwa Sophia kwamba, nia ya Waziri ilikuwa ni kuboresha mfumo wa utoaji mikopo na siyo kufanya uchunguzi kwa bodi na ndiyo maana unakuta hata hadidu za rejea hizo mbili walizokuwa wamezitanguliza, wakajadiliana, na bodi ikashauri kwamba ziongezwe hadidu za rejea nyingine. Ingekuwa ni uchunguzi, nadhani bodi isingepata nafasi ya kuongeza hadidu za rejea kwa ajili ya hiyo kazi ya maboresho ya mfumo wa utoaji mikopo. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa hapo naona tunaanza kuchanganya mambo. Hebu turejee maelezo ya Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni alisema nini na hiyo bodi inaenda kufanya nini?

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, malizia mchango wako.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kimsingi najua Waziri amefanya kazi yake kama Waziri, na hapo mwanzo nimesema Makatibu na Wasaidizi wa Mawaziri kazi yao kubwa ni kuwasaidia Mawaziri kutimiza makusudi na kazi zao wanazozifanya. Nimesema bodi yenyewe ambayo inafanya kazi na Waziri, hatujasema imegombana na Waziri, lakini kama umepewa jukumu la kufanya kazi hiyo ya kuisaidia bodi kwa Watanzania na hasa wanafunzi wetu, kwa nini utoe fedha? Basi kama ni hivyo, basi kanuni zibadilishwe kama inawezekana. Mimi nafikiri hivyo, *unless* kama sijaiielewa Kamati.



## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, naomba, kukosea kupo, lakini hata kama wanasema amelidanganya Bunge, mimi sijaona kama amelidanganya Bunge, vinginevyo wewe usingetoa nafasi ya kufanya. Aliomba msaada wa kusaidiwa kuweza kuhakikisha Taifa letu linafanya kazi vizuri. Mimi sijaona kama ameshitaki, alifanya wajibu wake kama Waziri. Sijaona kama ni kitu kibaya, wala tusikichukulie hivyo, ndiyo maana wewe ukaona usimame kama mhimili kuhakikisha kazi hii inatendeka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tupo hapa kwa ajili ya kujenga, kutengeneza na ndiyo maana sisi hapa tunaitwa Wapinzani, tunaotoa mawazo mbadala pale ambapo Serikali imekosea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaamini Mheshimiwa Waziri alikuwa sahihi, bodi iko sahihi na kuanzia sasa bodi itakuwa very sensitive, kwa sababu tayari imeshaona kumbe ukikosea kidogo unaweza ukaitwa, unaweza ukaenda kufanywa kitu fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Kamati, naipongeza na maoni yao yazingatiwe, na Wabunge wenzangu tuyawekee mfumo mzuri na tuyakubali maoni yao. Ninampongeza Waziri na ninaipogeza bodi vile vile maana tunataka kusonga mbele, hatutaki kurudi nyuma. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, mbele yetu hapa hatuna hadidu za rejea ambazo zinaihusu hii Kamati ambayo Mheshimiwa Waziri ameiunda. Kwa hiyo, kwa maana ya kule inaenda kufanya uchunguzi, kuboresha mfumo au itatoa jambo gani, lazima tuwe na zile hadidu za rejea. Pengine

**7 NOVEMBA, 2022**

Wajumbe wa Kamati ndiyo wanaweza kuwa wameziona, lakini hapa hazijaletwa kwa sababu haikuwa sehemu ya hoja.

Sasa hilo nalo linatupelekea kidogo kutokuwa na uhakika sana kama tunataka kusema fedha zingetoka upande gani, kwa sababu hatujaziona zile hadidu za rejea.

Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kuchangia na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati atapata nafasi ya kuhitimisha hoja. Kwa hiyo, baadhi ya mambo pengine atayatolea ufafanuzi kwa sababu hata mimi sina hizo hadidu za rejea hapa kuweza kupendekeza fedha itoke wapi? Kwa sababu inategemea wanaenda kufanya nini kwenye hiyo bodi?

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Elibariki Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, halafu Mwenyekiti wa Kamati ajiandae kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa mtazamo wangu tunapokutana na changamoto, kwanza nianze na kukushukuru. Kuna kauli umeitoa hapo kabla, binafsi nimeona ni kauli ya kiuongozi. Jambo hili tusipolisema hapa ndani ya Bunge tunaweza tukajenga taswira kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita imeingia madarakani, kuna matatizo makubwa, wanafunzi hawapati mikopo, Serikali haitoi fedha, ndiyo *notion* ambayo imejengeka huko nje. Sasa nataka tuweke mambo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Samia toka ameingia madarakani, ameongeza fedha za mikopo ya

## 7 NOVEMBA, 2022

Elimu ya Juu kutoka Shilingi bilioni 464 mpaka Shilingi bilioni 570, ambalo ni ongezeko la Shilingi bilioni 100 na kitu kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Hilo nataka tuliweke sawasawa. Kwa sababu ilivyozungumzwa itaonekana kwamba, sasa yaani bodi pamekuwa panayumba, kuna myumbo. Namna hii tukifanya tutakuwa hatumtendei haki Mheshimiwa Rais aliyeko madarakani, tutakuwa hatutendei haki Serikali kwa juhudi wanazozifanya kuhakikisha watoto wetu wanapewa mikopo. Hilo lazima tuliweke vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kiti chako kimetoa maelekezo kwamba tunavyozungumza *it is like* kwamba hakuna kitu kinafanyika kwenye bodi, jambo ambalo nimeshukuru sana umetoa hayo maelekezo na huo ndiyo msimamo wangu. Kwa sababu takwimu zinaonesha, Mama Samia toka ameingia madarakani, Rais wetu amefanya *deliberate decision* ya kuongeza fedha kuwasaidia watoto wa Kitanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama kuna changamoto zimejitokeza za kiutendaji, hatuwezi kufumbiana macho hapa. Mimi sifungwi mdomo na mtu, kama kuna changamoto naiona *for the interest* ya nchi nitasimama hapa kusema ukweli bila kufungwa mdomo na mtu; na ndiyo kazi ya Mbunge na ndiyo jukumu la Kibunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumesikia ripoti hapa, naomba niseme kwa unyenyekevu mkubwa sana. Hii ripoti iliyosomwa hapa na Mwenyekiti wa Kamati, siyo ripoti ya Kamati, hii ni ripoti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu Kamati imepewa majukumu kama wanafanya kwa niaba ya Bunge.

**7 NOVEMBA, 2022**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare.

### **T A A R I F A**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mdogo wangu Mheshimiwa Elibariki Kingu. Tunachokizungumza hapa ni kwa maslahi mapana ya wananchi wetu, na mjadala huu unalenga amri yako ambayo uliitoa kwa Serikali. Uliiambia Serikali kuwa watoto wote waende vyuoni wakati tunaandaa taratibu namna gani watapatiwa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tujadili namna ya kuwasaidia watoto wa masikini, wa wakulima na wafanyakazi wa nchi hii. Mheshimiwa Rais alishatoa fedha. Sasa kama changamoto ni utekelezaji, ndiyo tulizungumze hilo. Nani kakosea; nani kafanya nini; lakini dhamira yetu ituweke wapi? Tuna nia ya kuwasaidia, Mheshimiwa Rais upande wake kashamaliza, sisi kama Bunge tulishatoa na wewe kama Mkuu wa Mhimili huu ulishatoa maelekezo kwamba wanafunzi hawa waende vyuoni.

Mheshimiwa Spika, ili kumaliza changamoto hii, watoto walioko vyuoni hawajalipwa *tuition fees*, zinatoka wapi? Matarajio yao ni hii Bodi ya Mikopo na Wizara ya Elimu. Ndiyo tujadili hao watu ili namna gani waende kama timu moja. Watoke huku na kule; nani ni nani; na nani ni nani; na afanye nini; kwa kipindi hiki? Tuisaidie nchi hii, tuisaidie watu wetu na tuisaidie watoto wa wananchi masikini ambao wazazi wao nao wenyewe walipiga kura kwa ajili yetu na tumo ndani ya nyumba hii.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mdogo wangu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, malizia mchango wako.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, wewe ni kiongozi mstahimilivu na mvumilivu sana. Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nakisema, taarifa hii iliyoletwa katika Bunge lako ni Taarifa ya Bunge kwa sababu Kamati imekasimiwa madaraka na Bunge lako. Hoja yangu ya msingi, hivi kweli Bunge hili lije kuanza kufanya kazi ya kumfundisha Waziri namna ya kufanya *communication* na watu wake wa Wizarani? *it is impossible*. Unajua tusichukulie mambo haya kimzaha mzaha, *at the end of day* tunaharibu hali ya hewa ya siasa nje, tunaona kwamba ni mambo ya kawaida. Bunge hili lianze kumfundisha Waziri namna ya kuwasiliana na watu wa Bodi ya Mikopo? Bunge lianze kumfundisha Waziri umeipa kazi Tume uliyoiunda wewe...

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, *terms of reference* zinatengezwa na mtu mwingine, aliyempa kazi bodi nani ametengeneza *terms of reference*? Tunaambiwa hapa kwenye ripoti, kama tumeamua kufunika kombe mwanaharamu apite tulifunike, lakini ukweli utabaki Waziri na timu yake wapange mawasiliano vizuri na Wizara, hatutaki kuharibiwa hali ya hewa ya siasa nje. Ahsante. *(Makofi)*

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, naona umesimama.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Elibariki Kingu kwamba jambo hili ambalo tunalijadili humu la mawasiliano yasiyofuata utaratibu au kuvunjika kwa mawasiliano katika Wizara ya Elimu ni jambo ambalo ndilo lilimfanya Mheshimiwa Spika atengeneze hii Tume, kwa kuonekana kwamba hakuna utendaji unaoendelea baina ya Wizara na Bodi. Jambo hili pia ndio tatizo la msingi linalosababisha vijana wetu kutokupata mikopo kwa wakati. Tatizo la mikopo kuwa kubwa ni kwamba Wizara ya Elimu imeshindwa kusimamia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ndio taarifa nilitaka kumpa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Mtoa Hoja ajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuchangia hoja ya Kamati yetu na naishukuru Kamati kwa kazi waliyoifanya na mambo waliyoibua.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kidogo; la kwanza, Kamati inasema kwamba nanukuu kwenye taarifa; “kwamba wakati akitoa maelekezo yake Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inamkwamisha.”

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, niliyosema hapa yapo kwenye *Hansard*, sikusema maneno hayo nadhani ni kughafirika, naomba iondolewe kwenye taarifa.

Mheshimiwa Spika, nilipokutana na Kamati tulizungumza, niliwaeleza kwamba ile Kamati ya Kupitia Mikopo ilishaanza kazi na kwa kweli ilianza kazi kabla hoja iliyotolewa hapa kuhusu mikopo ya elimu ya juu na mtoa hoja wakati ule Mheshimiwa Ezra alinukuu siku naongea na vyombo vya habari, kwamba atakayekwamisha kazi ya Kamati hii nitakula kichwa. Nilisema vile kwa sababu nilikuwa nataka nione *speed* ya kazi inaongezeka. Sasa hata ukienda kwa *whatever explanation* kuanzia tarehe 12 Julai mpaka 31 Oktoba, 2022. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati ile ilikuwa tayari kufanya kazi mwezi Septemba, *on record* na ilipeleka *proposal* na ilikuwa tayari kufanya kazi mwezi Septemba, haikuanza kufanya kazi na wale watu wameajiriwa sehemu nyingine wakawa wametawanyika. Kamati iliniuliza, wewe Bodi imekwamisha? Niliwaambia Bodi naimudu, ikinikwamisha mimi nitaishughulikia siji kushtaki Bungeni hapa na sikuishtaki Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakaniuliza ulitumia neno *resistance*, kwamba *resistance* uliyoiona inasababisha uamini kwamba huenda kuna madudu, ulikuwa unamaanisha nini na *resistance*? Kwa sababu sikusema Bodi wala sikuitaja, niliwaambia moja, sikuridhika na *speed*, nitaeleza kidogo.

Mheshimiwa Spika, pili, nilieleza na nilieleza hapa *leakages* za taarifa mitandaoni, ya barua zinazotoka kwenye Bodi na maelezo kwamba hapa Mkenda anafanya *witch-hunting* anataka kuweka Mchaga

**7 NOVEMBA, 2022**

kuongoza, aache kufuatilia huku, yeye atafute hela ziongezeke zaidi. Sasa ile hisia huwezi kujua na hata sasa hivi siwezi kujua *leakage* inatoka wapi, lakini *fact of the matter is*, mimi kazi yangu na CAG ameeleza kwamba *oversight* ya Wizara kwenye Bodi ya Mikopo si nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi yangu ya ku-*exercise oversight* sio *witch-hunting* na uzuri *clip* zipo. Mara ya mwisho nilivyokutana na Bodi tarehe 5 Septemba nadhani, niliwaeleza sina haja ya kumuumbua mtu hii ripoti ni ya Waziri na ni ya Bodi. Tunataka kuangalia wapi tunaweza tuka-*improve*. Ripoti ni ya Waziri na ni ya Bodi, tunataka kuangalia wapi tunataka...

Mheshimiwa Spika, sasa mtu anapodhani kwamba ni *witch-hunting* au nataka kumwondoa mtu siwezi kuelewa.

Mheshimiwa Spika, pili na hili siku...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ngoja nikuongoze kidogo, ukitoa maelezo yale ambayo hayako kwenye hii taarifa na michango ya Waheshimiwa Wabunge kwenye hoja hii, utataka tena tufungue, watu watataka kujibu tena hoja hizo.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Haya, basi...

**SPIKA:** Na ile Bodi haitapata tena fursa ya kuanza kujibu haya, kwa hiyo, tutakuwa tunaenda mbele, tunarudi nyuma.



**7 NOVEMBA, 2022**

Kwa hiyo, nikuombe ufafanuzi umepewa muda, hoja zile zilizotolewa na Wabunge hapa baada ya kuwa Kamati imeleta taarifa na zile za kwenye taarifa ambazo wewe unataka kuzitolea ufafanuzi ili tuwe tumejielekeza kwenye jambo lililo mbele yetu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, ahsante na nitafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza sikuja kuishtaki Bodi humu, sina haja ya kuishtaki Bodi, ninaimudu na wala sikusema kwamba Bodi inanikwamisha kama ilivyoandikwa hapa. Neno *resistance* nililieleza vizuri kwenye Kamati na nilieleza mambo ya *speed*, nilieleza mambo ya mitandao. Vilevile maelezo ambayo nilikuwa nimeyapata ambayo sikuridhika nayo na Kamati niliwaeleza vilevile kwamba waliambiwa na Kamati fulani ya Bunge kwamba Kamati yangu ivunjwe, tulipotafuta maandishi hatukuyapata.

Mheshimiwa Spika, kitu cha muhimu ni kwamba kazi imeanza tarehe 31 na lazima niseme ukweli Kamati inapata ushirikiano mkubwa sana na Bodi na nimeongea nao hata leo kwamba kazi inaendelea vizuri sana, wanaendelea. Watanzania wote wanaosikiliza wajue kwamba tutajaribu kuchambua na kuelewa kwamba tunavyogawa mikopo kama kweli tunagawa kwa haki, mahali ambapo pana upungufu tutaweza kuparekebisha.

Mheshimiwa Spika, lazima niseme vilevile kwamba suala kubwa ambalo hata CAG alizungumza na kila mtu alizungumza hapa ni suala la kugawa mikopo kwa haki. Kamati yenyewe hadidu za rejea kama ulivyouliza ya kwanza, kwa sababu ni wataalam wa mifumo na ni

**7 NOVEMBA, 2022**

wataalam wa *programming* ni kwenda kuangalia takwimu na kuzi-program, kuhakikisha kwamba kila aliyeomba mkopo, sio *some...*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Ni kila aliyeomba mkopo na vigezo alivyonavyo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kasalali Mageni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba anaposema hakuna shida kati ya Waziri na Bodi ya Mikopo na hakuna ukwamishaji wowote, nataka nimpe tu taarifa kwamba Kamati hii iliambiwa ikaketi na Mheshimiwa Spika, kwa sababu ilionekana kuwa maelekezo ya Waziri kwa Bodi ya Mikopo yalikuwa yanakumbana na upinzani, ina maana kulikuwa kuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa inapoonekana hakuna tatizo, inaonekana hakuna sababu hata ya kujadili hii ripoti ya Kamati na hakuna hata sababu ya kuwepo hii Kamati kwenda kukaa na kutumia fedha za umma. Kwa hiyo, taarifa ni kwamba tatizo lipo na kwa mujibu wa maneno yake na maelekezo ya Bunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Mkenda, taarifa hiyo.

**7 NOVEMBA, 2022**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, hii taarifa siipokei na nimeeleza kwamba *at some point* nilikuwa sijaridhika na *speed* ya utekelezaji. Ie Kamati ilikuwa tayari kufanya kazi mwezi Septemba...

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, kwa nia njema, inabidi tuisaidie hii nchi. Waziri amepewa dhamana ya kusimamia Wizara, kuna *some extent* anasema hakuwa ameridhika na utendaji wa Bodi, *why did that matter come in the Parliament?* Hilo jambo kwa nini limekuja Bungeni? Kwa nini Waziri *on its own* asichukue hatua kwa Bodi mpaka lije Bungeni?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe na utulivu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, nilikuwa sijaridhika na *speed* ya kazi, nikatoa onyo *public*, siyo humu Bungeni na kazi ikaanza na ushirikiano ni mkubwa na ndio jukumu langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilizungumza *in public* na labda ni-*quote* maneno; “kwamba atakayekwamisha Kamati hii nitakula kichwa” iko ndani ya uwezo wangu na nilizungumza hivyo...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**7 NOVEMBA, 2022**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, sasa Kamati imeanza kazi...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumpe muda achangie, labda ngoja nifafanue jambo moja ili tumpe nafasi aweze kuchangia.

Mheshimiwa Waziri jambo ambalo lilipelekea Kamati kwenda kukusikiliza wewe na Bodi ni kwamba hapa ndani tulikuwa tunajadili hoja ya dharura ambayo ilikuwa inahusu mikopo. Mheshimiwa Waziri ukapata nafasi ya kuchangia, maneno yale uliyoyasema ndio yaliyopelekea Bodi kuambiwa itokeze mbele ya Kamati na wewe uende mbele ya Kamati. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndio maana nimesema kwa yale ya ziada kwa sababu Taarifa ya Kamati hii ya utendaji kazi wake na mapendekezo yake yatakuja mwezi Januari, kwa sasa tujielekeze pale kwenye maneno ambayo yalipelekea Kamati kuambiwa ikakutane kwa sababu Taarifa Rasmi za Bunge zinayo hayo uliyosema Waziri, zinayo maagizo niliyotoa na Kamati imeleta taarifa.

Mimi naenda na wewe vizuri, kuna maneno umesema humu kwenye Kamati yaondolewe, kwa hiyo naamini Mwenyekiti atakuja atoe hapa ufafanuzi. Ukitoka tu nje ya hapo ndio hizi taarifa zinazokuja Mheshimiwa Waziri. Hizi taarifa zinazojitokeza ni kwa sababu unaenda kwenye maelezo ya ziada ambayo hatutapata muda tena wa kuanza kufuatilia uhalisia wake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri muda wako bado unalindwa, karibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, ahsante, nimekuelewa na nakushukuru kwa mwongozo wako.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo yako mambo yangu ya kazi yangu niliyasema nje ya Bunge, wakati naongea na press na yale niliyoyasema humu na yale niliyoyasema humu nilijaribu kuyafafanua kwenye Kamati kwamba yalikuwa na maana gani kama nilivyoeleza ni hayo nilikuwa najaribu kuyaeleza. Lakini bado tunarudi tena kwenye hoja ya msingi kwamba, kazi ya ile Kamati ni kujaribu kuhakikisha kwamba mikopo ya wanafunzi inagawanywa kwa haki. Nadhani hata ukiangalia kwenye ripoti ya CAG imesema wako yatima ambao wamekosa mikopo. Kwa hiyo, kazi ile na Waheshimiwa Wabunge wakati tunajadili bajeti yetu hayo mambo yalikuwepo na Wabunge wengi walipenda tuyafanyie kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, cha muhimu sasa hivi ni kwamba kazi inafanyika na ushirikiano upo na ile Kamati imetoa *communication strategy*, mtu yeyote mwenye taarifa za ziada atapeleka kwenye Kamati. Naamini kazi itakapokamilika tutakuwa na fursa nzuri sana ya kuboresha namna ya kutoa mikopo. Kwa hiyo, hilo ni kubwa na nadhani hatutakiwi kutoka kwenye reli.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, labda nieleze kidogo tu kuhusu TOR ambazo ulikuwa umesema hadidu za rejea, sijui kama ni wakati wake wa kuzieleza hapa, kwa sababu kazi kubwa ile ni *compliance*, kwamba vigezo ambavyo vimetangazwa, mwombaji anapoomba mkopo anavisoma kwenye tovuti, kwamba nikiwa na hivi naweza nikapata mkopo. Je, ukiomba na unakidhi hivyo vigezo unapata mkopo? Kama nilivyosema wakati ule hata kama vigezo hivyo bado vina mashaka, ni vizuri kwanza tuvitendee haki tufanye hivyo.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, la pili, tunahitaji na iko kwenye *CAG Report* kuangalia taarifa zipi za ziada tunaweza tukazitumia kwa ajili ya ku-*improve means testing* na hii wanaifanya. Tumefanya kazi na Bodi kama ninavyosema na wenyewe wameongeza *TOR* zao kwa sababu kuna kazi wanataka kuifanya na niliridhia na nataka kutoa tena taarifa hapa, Kamati ipo kazini, inafanya kazi vizuri, *speed* nilikuwa sijaridhika nayo, sasa hivi ninaridhika na kazi inavyokwenda na Bodi. Nisiporidhika hatua za kuchukua zipo ndani ya mikono yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana, sasa nimwite mtoa hoja...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, ahitimishe hoja yake.

**MHE. MUSSA R. SIMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kuendelea kuruhusu mjadala huu ambao una tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge sita pamoja na Mheshimiwa Waziri kwanza wamekubaliana na kazi ya Kamati, tunawashukuru sana kwa niaba ya Mwenyekiti na Wanakamati wote, kwa kukubali kazi ambayo tumeifanya. *(Makofi)*

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, umekuwa ukielekeza mara kwa mara na hoja ya msingi hapa ni kwamba Bodi inamkwamisha Waziri kufanya kazi yake na Waziri amesema na *Hansard* zipo. Sasa ame-declare ina maana hili alilolisema sasa angelisema awali usingeitisha Kamati kufanya kazi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sitaki kurejea sana ndani, kwa kuwa Waziri amesema kwamba hakusema, hakuwa anamaanisha *resistance* ya Bodi kwenye kufanya kazi yake na ameomba *Hansard*, nataka hii niachie meza yako au kiti chako kifanyie kazi hilo, lakini sisi tumetekeleza wajibu wa maelekezo uliotupatia na hayo ndio yalikuwa majibu yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo naweza kulitolea maelezo la Mheshimiwa Mwakagenda alizungumza kuhusiana na Bodi kulipa fedha. Bodi fedha zote zile ni za Wizara ya Elimu isipokuwa kulikuwa na Mradi wa *HEET*. *HEET* maana yake ni *Higher Education Economic Transformation* ambayo ina mchanganyiko wa miradi mingi ndani.

Mheshimiwa Spika, moja ya fedha iliyoko pale ni ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Sasa ile Bodi zaidi ya nadhani shilingi milioni 79 ilikuwa imetengwa kwa ajili ya kulipa hiyo Kamati ambayo Mheshimiwa Waziri aliiunda na hizo fedha hawezi kuidhinisha Mkurugenzi wa Bodi au Mwenyekiti, ni lazima uandike barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara, Katibu Mkuu ndio awape ruhusa ya kulipa hizo fedha. Kwa hiyo kwa ujumla ni fedha za Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine nikushukuru sana na nishukuru Bunge lako tukufu kwa hatua hii ambayo tumefikia. Ahsante sana. (Makofi)

**7 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hujatoka hapo mbele, tusaidie kwa sababu hujaja na ile taarifa yako, lakini katika yale maoni na mapendekezo kulikuwa na mapendekezo matatu; (a); (b) na (c). Lile la tatu linasema msingi wa malalamiko ya wanafunzi wa Vyuu Vikuu yaliyosababisha hoja ya...; mimi naona hili kwa sababu halikuwa sehemu ya ile hadidu ya rejea, sijui kama hii huwa ina umoja na wingi, lakini kwenye hadidu za rejea hili halikuwepo, kwa hivyo wakati nawahoji Wabunge ili tuwe tumeongozana vizuri, tusaidie aidha, uliondoe hili lisiwepo ili wanapohojiwa wahojiwe kwenye haya mawili ambayo Kamati mmependekeza au kuna namna yoyote ambayo ungetamani hili liwepo, lakini sasa liendane na ile hoja ambayo ililetwa mbele ya Kamati.

**MHE. MUSSA R. SIMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nikushukuru, tutaondoa neno msingi wa hoja hiyo, lakini hiyo ni miongoni mwa mambo ambayo yamepelekea mjadala uliopelekea hoja hiyo kutuagiza Kamati kuifanyia kazi. Tutaondoa hilo neno kwamba sio msingi wa hiyo hoja.

**SPIKA:** Sawa. Sasa hapa mwisho inasema; Kamati inasisitiza Serikali itekeleze maagizo ya Bunge ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaostahili mikopo wanapata mikopo yao, yaani ndio mwendelezo wa hii hadidu ya rejea na hiyo siku tulishapitisha sisi azimio, yaani Bunge lilishapitisha azimio kuhusu jambo hili.

**MHE. MUSSA R. SIMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wewe sasa



**7 NOVEMBA, 2022**

tunaweza kuondoa hicho kipengele (c) kwa sababu tulishapitisha azimio hapa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kwa hoja hii ikiwa na hayo mapendekezo mawili ambayo ili sote tuwe kwenye picha moja nitayasoma. Kamati inapendekeza kama ifuatavyo:-

Mosi; mawasiliano ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yaboreshwe ili maelekezo ya viongozi wa sera na wasimamizi wa utekelezaji wa maelekezo ya kiseru yaratiwiwe kwa ufanisi na tija.

La pili, ni Kamati iliyoungwa na Waziri iendeleo kufanya kazi yake ambayo imeonekana kuwa na tija. Ufanisi wake utategemea ushirikiano itakayopata kutoka Bodi na Wizara pamoja na miongozo na mawasiliano bora baina na Bodi na Wizara kwa upande mmoja na Kamati hiyo kwa upande mwingine. Kwa hiyo mmesikia haya ambayo Bunge linaazimia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Sima uko sehemu gani? Ilibidi utoe hoja tena, eeh kwa hiyo rudi utoe hoja, halafu tuone inaungwa mkono ama haiungwi mkono. Kama haiungwi mkono hatutalihoji Bunge, ikiungwa mkono ndio tunalihoji Bunge.

**MHE. MUSSA R. SIMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru naomba sasa kutoa hoja juu ya wasilisho la Kamati ambalo nimelisoma hivi karibuni. *(Makofi)*

**7 NOVEMBA, 2022**

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Haya Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Kaimu Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutokufuata maelekezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru kwanza Wajumbe wa Kamati hii, lakini na Wabunge wengine ambao mmeshiriki katika mjadala huu.

Jumba hili ni jumba ama ni Muhimili wa wananchi, kwa hiyo jambo lolote linalogusa mambo ya wananchi likisemwa hapa ndani linachukuliwa kwa uzito unaostahiki. Kwa hivyo, hata hili ambalo lilipelekwa kwenye Kamati ni kwamba tusingependa majibu yanayotafutwa ama suluhu zinazotafutwa kwa ajili ya kuwapa wananchi majibu ya hoja zao au ya changamoto zao ziwe zinakwama kwama pahala. Sasa nadhani ni dhahiri na wote tumepata picha.

Mheshimiwa Waziri, ameeleza sasa na alieleza kwenye Kamati akifafanua alikuwa na maana gani, alitamani jambo liende haraka, likawa haliendi haraka.

## 7 NOVEMBA, 2022

Sasa katika hali hiyo ya kutamani jambo liende haraka na haliendi haraka, ikawa ni kuweka msukumo pengine hapa na pale, lakini sasa ukishalisema katika kuweka msukumo hapa na pale ndomana amekiri kwamba hapa alishazungumza kwenye vyombo vya habari ili watu wajue kwamba Waziri anafuatilia jambo hilo na hapa Bungeni alilisema kwa muktadha huo. Sasa maneno yaliyotumika hapa Bungeni ndiyo yaliyopelekea kwamba hebu Kamati ikutane na hii Bodi tujue shida iko wapi, kwa nini haifanyi kazi kadri inavyoelekezwa (*Makofi*)

Hivyo, Bodi imepata nafasi pia ya kusikilizwa na Kamati yetu na wao wameeleza mtiririko wa mambo, kwa hivyo tumepata picha, picha gani? Kwamba Bodi ya Mikopo haina ujeuri wowote kwenye mambo ambayo inaagizwa na Serikali na wakati huo huo inao sasa utayari wa kukimbizana na kazi ya Kamati hii ambayo imeundwa na Mheshimiwa Waziri hapa, Waziri, ameonesha dhahiri kwamba Kamati ile inapewa ushirikiano na Bodi na kwa hivyo tatizo lililofikiwa kuwepo halipo tena. Kwa hivyo, hiyo ndiyo hoja ya msingi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka pamoja na haya maazimio ya leo ya Bunge. Kwa sababu haya tukishahojiana hivi ni maazimio ya Bunge, hivyo Wizara itayachukua na kuyapeleka kule yanakotakiwa. Bunge hili wakati tukijadili hoja za Kamati zetu zile tatu kwa maana ya PIC, PAC na LAAC mojawapo ya maazimio ambayo yameazimiwa hapa ni kwamba CAG akafanye ukaguzi, sikumbuki kama ni ukaguzi maalum au ukaguzi wa kiuchunguzi lakini mojawapo kati ya hayo, Bunge limeazimia kwamba CAG aende huko, kwa hivyo na yeye ataleta taarifa kwa hivyo tusiwe na wasiwasi. (*Makofi*)

**7 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Mheshimiwa Waziri, ikafanye kwa mujibu wa hadidu za rejea walizopewa pia CAG ataenda kufanya kwa niaba yetu sisi, kwa maana ya mahesabu yamekaa vipi huko kwenye Bodi yetu ya Mikopo ya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu hili la mwisho ambalo nimesema kwamba ama nimemshawishi Mwenyekiti aliondoe kwa sababu Bunge lilishaamua kuhusu jambo hilo, naamini kwamba Serikali italeti mrejesho huo kabla Bunge hili halijaondoka hapa Dodoma kuhusu Mikopo ya Watoto wetu ambao hawajapata mikopo. Kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi naamini hivyo kwa sababu za msingi kabisa, Serikali na Bunge ushirikiano ni wa karibu na mambo naamini yataenda vizuri kabla Bunge hili halijaahirishwa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH-KATIBU MEZANI:**

### **KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, nimuite naona amekaa mbali sijui kama anajua yeye ndiye anaeitwa? Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa

**7 NOVEMBA, 2022**

Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba aje awasilishe Mapendekezo ya Mpango. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili mapendekezo ya Mwongozo ya maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuendelea kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana ili kuwasilisha na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa, kwa uongozi wake mahili katika kuendelea kuwatumikia Watanzania kwa kusimamia utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya maendeleo na kuboresha huduma za jamii kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa busara hekima na weledi katika kazi zake za kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais, kuongoza Taifa letu. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa

**7 NOVEMBA, 2022**

Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake bora na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi mzuri na dhamira yake ya dhati ya kuwaletea wananchi wa Zanzibar maendeleo ya kweli. Vilevile ninampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa uongozi wake hodari ndani ya Serikali na hapa Bungeni, pamoja na kumsaidia Mheshimiwa Rais, kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mipango ya Bajeti pamoja na ahadi zilizopo katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe na Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi. Naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Muhimili mzima wa utoaji wa haki, kipekee pongezi ziende kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, vikiongozwa na *General* Jacob Mkunda Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kwa kuendelea kusimamia imara ulinzi na usalama wa nchi yetu na kuwezesha shughuli zote za maendeleo hapa nchini kufanyika kwa uhakika.

Aidha, pongezi zingine ziende kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, inayoongozwa na Mheshimiwa Sillo Daniel Barani, Mbunge wa Babati Vijijini, Makamu Mwenyekiti Mheshimwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, pamoja na Wanakamati wote kwa maoni na ushauri wao walioutoa kwa Wizara yetu. Maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa kwa kiwango kikubwa kwa ajili ya kuboresha mapendekezo pamoja na mwongozo wa mpango pamoja na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa Mwaka 2023/2024.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Hamad Hassani Chande Mbunge, na Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na timu za wataalam wote wa Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika kuandaa vitabu pamoja na mapendekezo haya ambayo ninawasilisha hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yanabainisha juhudi ambazo Serikali ya Awamu ya Sita inachukua katika kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuimarisha huduma za jamii, kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara hapa nchini na ukuaji wa sekta binafsi pamoja na fursa za ajira ili kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa, pamoja na kuimarisha sekta ya utalii na uwekezaji kwa kuendelea kutangaza vivutio vya utalii na uwekezaji kupitia *Royal Tour*, kuweka msukumo katika kuimarisha sekta za uzalishaji na zile zinatoa ajira kwa vijana wengi kama utamaduni, sanaa na michezo pamoja na sekta zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango pamoja na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2023/2024 yameandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Aidha, mapendekezo haya yamezingatia mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mwongozo na maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya

## **7 NOVEMBA, 2022**

Serikali pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2021/2022 na katika robo ya kwanza ya Mwaka 2022/2023. Mapendekezo haya yameainisha masuala mbalimbali ikiwemo mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Mpango pamoja na Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 na robo ya kwanza ya Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/2024 na maeneo ya vipaumbele kwa mpango na bajeti ya mwaka 2023/2024 pamoja na vihatarishi vya ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa mpango na bajeti na mikakati ya kukabiliana navyo. Mapendekezo yanayotakiwa katika kuzingatia na Maafisa Masuuli kwa uandaaji, utekelezaji na ufuatiliaji pamoja na tathmini ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viashiria vya uchumi katika Mwaka 2021 Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 4.9 ikilinganishwa na asilimia 4.8 kwa Mwaka 2020. Aidha, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya Mwaka 2022 Januari hadi Juni uchumi ulikuwa kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.4 katika kipindi kama hicho kwa Mwaka 2021. Kuimarika kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 pamoja na uwekezaji uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM, hususani kuwekeza katika miundombinu ya afya, elimu, nishati, maji, ujenzi wa barabara za mijini na vijijini, sanaa, michezo na utamaduni pamoja na biashara ndogondogo na shughuli za kiuchumi zinazotokana na ongezeko la mikopo katika sekta binafsi kama vile



## **7 NOVEMBA, 2022**

uchimbaji wa madini, utawala bora unaozingatia misingi ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2020/2022 kiwango cha ukuaji wa uchumi wa dunia kilitarajiwa kupungua kwa kufikia asilimia 3.2 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 6.1 wa mwaka 2021. Hali hii ilitokana na changamoto zinazokumba uchumi wa dunia ikiwemo vita inayoendelea nchini Ukraine, sambamba na mabadiliko ya tabianchi yaliyopelekea kuwepo kwa ukame na upungufu wa chakula, pamoja na mwendendo mzuri wa uchumi wa Taifa katika nusu ya kwanza hali inayoikumba uchumi wa dunia, kwa sasa itaathiri pia uchumi wa Tanzania Katika nusu ya pili. Hivyo kufuatia mwelekeo na muingiliano wa uchumi wa dunia kiwango cha jumla cha ukuaji wa uchumi wa Tanzani kinatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 4.7 kutoka asilimia halisi ya asilimia 4.9 ya Mwaka 2021. Hata hivyo matarajio haya ni zaidi ya wastani wa ukuaji wa uchumi wa nchi za Afrika zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara ambao unatarajiwa kuwa asilimia 3.8 kwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2020/2023 ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuanza kuongezeka na kufikia makadirio ya asilimia 5.3, maoteo ya ukuaji wa uchumi wa Tanzani yamezingatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suhulu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukabiliana na athari zinazotokana na vita inayoendelea Nchini Ukraine, ikiwemo uimarishaji wa sekta za uzalishaji ambapo bajeti ya kilimo, mifugo, na uvuvi zimeongezaka kwa kiasi kikubwa. Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara Mijini na Vijijini pamoja na Nishati, pamoja na Maji. Uboreshaji wa Huduma za Jamii na Utekelezaji wa

## 7 NOVEMBA, 2022

Miradi inayochachua Shughuli za uchumi na Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei uliongezeka katika nchi nyingi duniani kutokana na athari za vita za Ukraine pamoja na UVIKO Kumi na Tisa. Kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya Mwezi Julai 2022, mfumuko wa bei wa Dunia kwa Mwaka 2021 uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.7 ikilinganishwa na asilimia 3.2 kwa Mwaka 2022.

Aidha, mfumuko wa bei wa duniani kwa mwaka 2022 unatarajiwa kuendelea kuwa juu na kufikia wastani wa asilimia 8.3, kwa upande wa hapa nchini mfuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4.0 kwa mwaka unaoishia Juni 2022 ambapo upo ndani ya lengo la nchi la wastani wa asilimia Tatu hadi Tano na mfuko wa bei kwa kiasi kikubwa ulichangiwa na athari za Vita inayoendelea kule Ukraine ambayo imesababisha kuongezeka kwa bei na gharama za usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje hususani bidhaa za *petrol*, mafuta ya kula, ngano, mbolea, pia kutokana na mfumuko wa bei kumekuwepo na kupanda kwa gharama za maisha duniani kote kwa nchi zinazoendelea, zilizoendelea na nchi maskini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika kukabiliana na athari hizo, Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayowajali wananchi wake, imeendelea kuchukua hatua ili kuweza kupunguza makali hayo. Baadhi ya hatua ni kama kutoa ruzuku ya bidhaa ya mafuta ambapo takribani Shilingi Billioni 100 kila mwezi zimekuwa zikitolewa kushusha bei ya mafuta ambapo bei ya mafuta kwa Tanzania zimekuwa chini ikilinganishwa na

## **7 NOVEMBA, 2022**

nchi nyingi zinazotuzunguka. Kwa lugha nyingine Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, imekuwa ikimlipia mwananchi takribani Shilingi 500 kwenye kila lita ya mafuta yanayotumika katika shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kutoa ruzuku kwenye pembejeo za kilimo yaani mbolea pamoja na mbegu ambapo takribani Shilingi Billion 150 zimepelekwa kwenye ruzuku ya kupunguza bei ya mbolea kwa zaidi ya nusu ya bei iliyokuwemo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikilipa nusu ya bei kwa mwananchi anapotumia mbolea kwa kutoa ruzuku katika hiyo bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa bidhaa muhimu kama vile mafuta ya kula, unga wa ngano kwa kufuta kodi na tozo ambazo zilikuwa zinatozwa katika bidhaa hizo. Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, imekuwa ikimlipia kila mtumiaji wa mafuta ya kula pamoja na unga wa ngano kwa kufuta kodi zile na tozo ambazo zilikuwa zinastahili kulipwa katika bidhaa hizo. Lengo ni kushusha bei ya bidhaa hizo hali kadhalika kwa bidhaa za mbolea pamoja na bidhaa zingine zinazotumiwa majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka unaoshia Juni, 2022 mikopo chechefu imepungua kwa asilimia 7.8 ya mikopo yote ambayo ilikuwa asilimia 9.3 katika mwaka unaoishia Juni, 2021. Hadi Juni, 2022, Deni la Serikali lilikuwa Shilingi Billion 71,559.0 na hii ni kutokana na kuendelea kupokelewa kwa mikopo pamoja na riba za mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundominu ya umwagiliaji, barabara,

## 7 NOVEMBA, 2022

reli viwanja vya ndege, umeme, elimu, afya pamoja na miradi mingine ya maendeleo. Tahimini ta uhimilivu wa Deni la Taifa lililofanyika Novemba, 2021 inaonesha kuwa Deni la Serikali limeendelea kuwa himilivu katika muda mfupi, wakati pamoja na muda mrefu.

Aidha, Tarehe 07 Oktoba, 2022 Kampuni ya Moody's *Investors Service* ambao ni wabobezi katika masuala ya Kupima uvumilivu wa deni duniani walitoa taarifa inayoonesha kuwa mwelekeo wa hali ya uvumilivu wa Deni la Taifa la Tanzania umeimarika (*positive outlook*) kampuni hiyo inafanya uchambuzi wa athari na uwezo wa nchi katika kukopa na kulipa madeni yake katika nchi mbalimbali duniani. Matokeo haya yanatokana na kuwepo kwa viashiria imara vya uchumu na kuwepo kwa utulivu wa kisiasa hapa nchini hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu Sita katika kufungua uchumi na kuvutia mitaji, mtazamo huo unaenda sambamba na kauli ya Benki ya Dunia kama ilivyotolewa na Makamu wa Rais, wa Benki ya Dunia Madam Victoria Kwakwa, aliyetoa sifa kubwa kwa Tanzania kwa kusimamia vyema masuala ya uchumi licha ya changamoto za kiuchumi zinazoikabili Dunia (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni zimekuwa ni Dola za Kimarekani Billion 5.11 hadi Juni, 2022 kiasi ambacho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma za nje kwa kipindi cha zaidi ya miezi 4.6, kiwango hiki ni zaidi ya kiwango cha Kimataifa cha kupima uwezo wa fedha za kigeni ambacho kinakidhi miezi 4.0 ya uagizaji wa bidhaa za nje, kiwango hicho ni zaidi ya lengo la asilimia 4.5 ya kiasi cha kupima uwezo huo kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiba ya fedha ya kigeni katika Mataifa mengi zimeathiriwa na vita vinavyoendelea Ukraine vilivyosababisha kuongezeka kwa gharama ya uagizaji wa bidhaa na huduma mbalimbali kutoka nje ya nchi. Sehemu kubwa ya bidhaa hizo zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ni bidhaa zinazohusisha kukuza mitaji na malighafi za viwandani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia fedha za kigeni katika mataifa mengi zimeathiriwa na vita vinavyoendelea Ukraine iliyosababisha kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma mbalimbali kutoka nje ya nchi. Sehemu kubwa ya bidhaa hizo zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ni bidhaa ambazo zinahusisha kukuza mitaji na mlighafi za viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Kwanza ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024. Sura ya Kwanza ya Kitabu Cha Mapendekezo ya Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa bajeti ya 2021/2022. Katika mwaka 2022 Serikali ilikusanya jumla ya Shilingi bilioni 36,924.8 kutoka vyanzo vyote, sawa na asilimia 97 ya bajeti iliyoidhinishwa ya shilingi bilioni 37,992.5. Ufanisi wa mapato kwa asilimia 97 ulitokana na jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kufuatilia kwa karibu vyanzo vyote vya mapato vya kugharamia bajeti ya Serikali. Kiasi cha mapato yaliyokusanywa kinajumuisha Shilingi bilioni 24,395.6 mapato ya ndani na

## **7 NOVEMBA, 2022**

Shilingi bilioni 4,825.3 ya misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo na shilingi bilioni 7,703.9 za mikopo ya kibiashara ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali ilitumia Shilingi bilioni 37,215.8 kugharamia utekelezaji wa bajeti. Kati ya kiasi hicho Shilingi bilioni 22,561.5 ni matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 14,654.3 ni matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi bilioni elfu, hizo ni trilioni kwa lugha nyingine ndizo tunazoziwekea takwimu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023 mapato ya jumla ya Shilingi bilioni 9,100.1 yalikusanywa kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje. Kati ya mapato hayo mapato ya ndani yalikuwa Shilingi bilioni 6,211.3 sawa na asilimia 95.0 ya lengo la Shilingi bilioni 6,537.1. Mapato ya ndani yalichangia asilimia 68 ya mapato yote yaliyopatikana katika kipindi cha rejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 9,153.9 ilitolewa, sawa na asilimia 90.6 ya lengo la shilingi bilioni 10,107.6. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 5,848.7 ni ridhaa ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3,305.1 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 36.1 ya matumizi yote ya kawaida katika robo hiyo ya mwaka. Maelezo ya Kina Kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2021 na Robo ya Kwanza ya mwaka 2022/23 yanapatikana katika Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Pili na Sura ya Tatu mtawalia ya Kitabu cha Mwongozo na Sura ya Pili ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2023/2024.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2021 na robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023 Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya kielelezo ya shughuli nyingine katika maendeleo ya kipaumbele yaliyobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 hadi 2025/2026). Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa reli. Ujenzi wa Reli ya Kati kipande cha Dar-es-Salaam – Morogoro kilometa 300 umefikia asilimia 97.41, kipande cha Morogoro – Makutupora asilimia 89.7, kipande cha Mwanza – Isaka asilimia 12.53. Aidha, kipande cha Makutupora – Tabora kilometa 371 na kipande cha Tabora – Isaka tayari vimepata mkandarasi na upatikanaji wa fedha tayari umeshafanyika. Kipande cha Tabora – Kigoma na Uvinza – Malagarasi kinachoelekea Burundi kwenda Kitega na Kindu, DRC viko katika hatua ya kupata mkandarasi. Jumla ya Shilingi trilioni 1.38 zimetumika katika mwaka wa fedha 2021 na Shilingi bilioni 255.42 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania hatua zilizofikiwa ni kukamilika kwa malipo ya awali ya ndege tano ambapo ndege nne ni za abiria na ndege moja ni kwa ajili ya mizigo. Jumla ya Shilingi bilioni 732.56 zimetumika katika mwaka 2021/22 na Shilingi bilioni 494.61 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023. Aidha, mradi mkubwa wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato unaojumuisha ujenzi wa njia za kurukia ndege na majengo ya abiria unaoendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya AFDB kwa gharama ya Shilingi bilioni 360 na uwekaji wa jiwe la msingi umefanywa mwezi Novemba, 2022. Ukamilishaji wa taratibu za fedha kwa

## 7 NOVEMBA, 2022

ajili ya viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora, Shinyanga na Rukwa zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mradi wa mradi wa kufua umeme, Bwawa la Julius Nyerere, kwa ujumla hadi kufikia Oktoba, 2022 utekelezaji wa mradi umefikia zaidi ya asilimia 75. Jumla ya Shilingi trilioni 1.273 zimetumika katika mwaka 2021/2022 na Shilingi bilioni 394.02 ni katika robo ya kwanza ya mwaka 2022 na kazi inaendelea na kila mwezi zaidi ya bilioni 130 zinatumika kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mradi wa umeme vijijini kunaendelea na usambazaji wa umeme vijijini ambapo vijiji 9,163 kati ya vijiji 12,345 vya Tanzania Bara vimeunganishwa na umeme. Jumla ya Shilingi bilioni 313.4 zimetumika katika mwaka 2021/2022 na Shilingi bilioni 84.90 katika robo ya kwanza yam waka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuchakata gesi asilia kule Lindi kunaendelea na majadiliano ya mkataba kati ya nchi hodhi kati ya Serikali na wawekezaji kwa kushirikiana na mshauri mwelekezi wa masuala ya sheria, fedha na biashara, uchumi pamoja na masoko. Jumla ya Shilingi bilioni 3.69 zimetumika katika mwaka 2021/2022 na Shilingi milioni 963.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wa barabara na madaraja ambayo yanasimamiwa chini ya *TANROADS*, kazi ambazo zimeendelea ni pamoja na kuendelea kubpresha mtandao wa barabara hapa nchini na kujenga barabara za mikoa na barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani na barabara za mijini na vijijini. Kazi ambazo zimeshafanyika na kukamilika



## 7 NOVEMBA, 2022

kwa ujenzi wa Madaraja ya *Tanzanite*, Kiyegeya, Ruhuhu na kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigongo–Busisi kule Mwanza pamoja na barabara zinazounganisha zenye urefu wa kilometa 1.66 ambapo ujenzi umefikia zaidi asilimia 47.32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Wami na barabara unganishi kilometa 3.8 lieshafikia asilimia 83 na kuanza kutumika katika kipindi cha uangalizi. Daraja la Kitengule kule Kagera barabara unganishi yenye kilometa 18 asilimia 95.15 na Daraja la Sibiti kule Singida asilimia 95.15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla miradi 14 yenye urefu wa kilometa 883 imekamilika katika Aprili, 2021 hadi sasa. Yaani ndani ya kipindi cha Awamu ya Sita Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetumia jumla ya Shilingi trilioni 1.37. Pamoja na hayo, kuna jumla ya miradi mingine 44 ya barabara zenye urefu wa kilometa 1,523 yenye gharama ya Shilingi trilioni 3.8 ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi nchi nzima. Vilevile miradi 62 ya barabara iko katika hatua mbalimbali za manunuzi kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami. Utekelezaji wa miradi kwa kutumia utaratibu wa *EPC + F* mchakato umekwishanza kwa miradi 8 yenye urefu wa kilometa 2,533 na hatua za kimanunuzi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishazitaja barabara hizo kwenye orodha na zinapatikana, moja ikiwa ina chanja kutokea Ifakara kwenda mpaka Lumecha. Nyingine ikiwa inatoka karatuna inaenda Sibiti kwenda mpaka Maswa na nyingine ya Handeni, Kibereshi kwenda mpaka Singida pamoja na zile nyingine za Mtwango kule Mafinga na zile nyingine za kutoka Arusha kuja mpaka hapa Kongwa.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara ambazo ziko chini ya usimamizi wa *TARURA*. Kwa upande wa barabara za vijijini na mijini zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Vijijini, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 275.85, changarawe kilometa 11,120.89. Madaraja 596, makaravati na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 67.44 na kufanyika kwa matengenezo ya kwaida ya barabara zenye jumla ya kilometa 25,078.73. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Shilingi trilioni 2.36 zimetumika katika ujenzi wa barabara na madaraja kwa mwaka 2021/2022 na Shilingi bilioni 670.46 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023 katika barabara za vijijini na mijini zinazosimamiwa na *TARURA* katika kiwango ambacho ni kikubwa zaidi kwa *TARURA* kupata fedha hizo. Kwa kupitia bajeti ya mwaka 2022/2023 jumla ya zabuni 1,706 zenye thamani ya shilingi bilioni 621.66 zimetangazwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini ambapo kati ya hizo wakala imekwishaingia jumla ya mikataba 1,246 na wakandarasi wakaazi mbalimbali kwa nchi nzima yenye thamani ya Shilingi bilioni 406.21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za mikataba hiyo zimeshaanza na zinaendelea na zinahusisha ukarabati, ujenzi na matengenezo ya barabara na madaraja ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madaraja makubwa matatu ya Brega kule Kilosa lenye mita 140, Masabya kule Pimbwe, Katavi, lenye urefu wa mita 60 na Mkomazi kule Korogwe lenye urefu wa mita 40. Madaraja haya yanaunganisha maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo. Zabuni 460 zilizobaki ziko katika hatua za mwisho za kuweza kuwapata wakandarasi na kufikia mwishoni mwa

## 7 NOVEMBA, 2022

mwezi Novemba kwenda Disemba, mikataba itakuwa imesainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezea pia uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam pamoja na Mtwara na Tanga, ambapo zaidi ya bilioni 19.5 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo. Moja ya kazi kubwa ambayo imeshafanyika ni ruzuku ya mbolea katika upande wa korosho pamoja na pamba. Kwa kutumia mfumo wa wataalam wa utambuzi unaotumia QR Code, Serikali imeratibu uuzaji wa mbolea ambapo kufikia tarehe 5 Novemba, 2022 tani elfu 67,296 za mbolea zenye thamani ya ruzuku ya Shilingi bilioni 74.47 zimenunuliwa kwa wakulima kwa kutumia mfumo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na zoezi la usajili wa wakulima kwa kutumia alama za vidole ambapo hadi kufikia tarehe 5 Novemba, 2022 wakulima milioni 2.11 wamesajiliwa kwenye mfumo huu. Kutolewa kwa Shilingi bilioni 29 kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo ya korosho na kutolewa kwa ruzuku ya mbegu, viuatilifu vya pamba vyenye thamani ya Shilingi bilioni 75 na uzalishaji wa mbegu chini ya ASA kuwezesha upatikanaji wa mbegu za alizeti tani 2,500 ikiwa ni sehemu ya mafanikio; pamoja na kuwa na tani 1,700 za mbegu za ngano, tani 400 za mbegu za soya na kuzalishwa kwa miche milioni 7.9 ya mazao mbalimbali. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya uzalishaji wa

mbegu hekta 800 ambapo wakandarasi wanaendelea na kazi, pia jumla ya hekta 1,300 za mashamba mapya ya kuzalisha mbegu yanaendelea.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TARI*, kukamilika kwa tathmini ya zabuni ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba, ya uzalishaji mbegu yenye ukubwa wa hekta 854 ni moja ya mafanikio, yakiwa sambamba na kuanza kwa ujenzi wa maghala matano, ukarabati wa maghala matano ya kuhifadhi mbegu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 300 kila moja, kupata mzabuni wa ununuzi wa vifaa vya dawa za maabara ya Mikocheni, ununuzi wa vifaa vya dawa kwa maabara ya udongo ya *TARI*, Mlingano, ili kuweza kudhibiti ithibati ya kimataifa. Ujenzi wa maabara ya Kituo cha *TARI*, Mlingano na ukarabati wa *bio technology*, Mikocheni, ujenzi wa uzio pamoja na mashamba ya *TARI* ya kule uyole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, hadi kufikia mwisho wa robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023 jumla ya mikataba 21 ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye skimu za kijamii zenye thamani ya Shilingi bilioni 182 imesainiwa na wakandarasi wako uwandani (*site*) wanaendelea na kazi. Aidha, miradi 15 yenye thamani ya Shilingi bilioni 199.7 ipo katika hatua mbalimbali za kimanunuzi na inategemewa kusainiwa mwezi Disemba, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo cha mashamba makubwa ya pamoja (*block farming*) Wizara husika ya Kilimo imeratibu upatikanaji wa jumla ya ekari 183,000 za mashamba makubwa ya pamoja (*block farms*). Lengo ni kutatua changamoto ya upatikanaji wa ardhi, mitaji, teknolojia za kisasa na masoko kwa vijana na akina mama. Kazi ya kupima ardhi na afya ya udongo imekamilika. Kazi ya kusafisha shamba lenye ukubwa wa ekari 11,000 katika Kijiji cha Dogowe, Halmashauri ya

## 7 NOVEMBA, 2022

Chamwino ya Dodoma inaendelea. Ujenzi wa bwawa lenye uzio wa lita za ukubwa milioni 12 litakalotumika kumwagilia shamba hilo lenye ekari 8,000 katika Kijiji cha Membe, Chamwino, na mkandarasi yuko *site* kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mifugo, kukamilika kwa ujenzi wa majosho 192 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 85 ni moja ya mafanikio yakiwa sambamba na kuzalishwa kwa jumla ya dozi 50,261 ya mbegu za mifugo. Kukamilika kwa ujenzi wa minada nane na ukarabati wa minada tisa ni moja ya mafanikio. Mafanikio mengine ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Mabwawa ya Chamakweza yaliyoko Pwani, Kimambi kule Lindi, Manga kule Singida na kuanzishwa kwa program ya vituo vya utamizi pamoja na *SAUTI Program* ya Samia Ufugaji kwa Tija *Program* katika vituo nane na kila kituo kuwa na vijana 30. Jumla ya vijana 240 wameripotwa kupata nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezea kwa kirefu upande wa madini. Kwa upande wa afya ni kukamilika kwa ukarabati wa hospitali za rufaa za mikoa 19, ujenzi wa hospitali 135 za Halmashauri na hospitali 70 zimeanza kutoa huduma. Vituo vya afya 335, zahanati 668 na kununuliwa na kusambazwa kwa chanjo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yangu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maji utekelezaji umeshafanyika ikiwa ni zaidi ya asilimia 74.5 kwa upande wa vijijini na asilimia 72.3 kwa upande wa mijini. Pia, tayari utekelezaji wa miradi 394 ambapo wananchi wapatao milioni 1.3 waishio vijijini wameanza kunufaika na miradi 145 imetangazwa ili kuweza kupata

## 7 NOVEMBA, 2022

wakandarasi. Tayari seti za mitambo kwa ajili ya kuchimbia visima pamoja na seti za kitambo za kuchimbia mabwawa utaratibu wake umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu. Tunaendelea na *program* ya elimu bila malipo, bila ada ambapo zaidi ya bilioni 296 tayari zimeshatumika katika robo ya kwanza ya mwaka. Kwa upande wa mikopo ya elimu ya juu tayari fedha hizo zimeshatolewa ambazo ni bilioni 569 kwa wanafunzi wapatao 177,000 walioko elimu ya juu ikiwa ni ongezeko la zaidi ya bilioni 128 ukilinganisha na bajeti zilizopita. Serikali pia inatekeleza utaratibu wa elimu bila malipo kwa kidato cha tano na sita. Tayari fedha zimeshatolewa zaidi ya bilioni 160 kwa upande wa ujenzi wa madarasa zaidi ya 8,000 na fedha nyingine kwa ajili ya madarasa mengine takribani 8,000 tunaendelea na utaratibu wa upatikanaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utawala bora, usimamizi wa fedha za umma. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imeanza kuchukua hatua za kimakusidi ikiwemo kupitia upya muundo wa Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu, kuimarisha uhuru wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani na Taasisi za Umma, kuipatia fungu linalojitegemea, mafunzo ya ukaguzi wa mifumo na kuzifanya kamati za ukaguzi kuwa na wajumbe watatu wanaotola nje. Kadhalika Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM imeiongezea bajeti Ofisi ya CAG na kujengea uwezo wakaguzi na kuajiri wakaguzi wapya, ili kuongeza uwazi katika matumizi ya Serikali. Pia kuwezesha ofisi hizi kufanya kwa wakati na kukagua thamani ya fedha katika miradi

## 7 NOVEMBA, 2022

inayoendelea (*Real Time Audit*) pamoja na *value for money*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa ya CAG, kati ya kipindi cha 2019 hadi 2022 TAKUKURU ilifungua majalada 897. Kati ya hayo majalada 594 yalitokana na Taarifa ya CAG. Na katika mwaka huo majalada 303 yalifunguliwa kutokana na taarifa ya CAG iliyokuwa imekabidhiwa kwa Mheshimiwa Rais. Kati ya majalada hayo 353 uchunguzi wake ulikuwa umekamilika na watuhumiwa wake kufikishwa Mahakamani. Majalada 96 kesi zake zinaendelea na ziko hatua nzuri na kati ya kesi hizo 11 ambazo uamuzi ulishafanyika, Serikali ilishinda kesi 10 na kesi moja Serikali haikushinda. Majalada 32 watuhumiwa wake wamechukuliwa hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie. Kati ya majalada 353 ambayo yalitokana na taarifa ya CAG majalada 96 yalishafikishwa Mahakamani na kesi zake ziko katika hatua nzuri; 11 uamuzi ulishafanyika na Serikali ilishinda na majalada 32 watuhumiwa wake wamechukuliwa hatua za kinidhamu. Kwa hiyo, niwatake Watanzania waone kwamba Serikali inachukua hatua na haina mchezo katika kusimamia mali za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliokuwa vijijini mtakumbuka kuna wakati tulikuwa na vingedere vilivyokuwa vinasogeasogelea mazao yetu. Hatukuacha kulima bali tuliwadhibiti tu wale ngedere. Na kuna wakati tulikuwa tunalala kwenye vitanda ambavyo vilikuwa na kunguni, hatukuchoma nyumba nzima ili kuuwa wale kunguni, tuliwamwagia maji ya moto tu. Na kuna wakati chawa walitukuta vichwani, hatukukata kichwa kwa sababu, chawa wameingia kwenye kichwa, tuliondoa nywele tu, tulinyolewa upara. (*Makofi*)

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongeza uwazi katika matumizi na tumeziongezea nguvu ofisi hizi za ukaguzi ili ziweze kuzuia matumizi mabaya ya mali za Umma. Kwa hiyo, hakuna atakayefuja fedha za Umma, fedha za walipa kodi wa Tanzania na akabaki salama. Fedha za walipa kodi ziko salama, na yule atakayefuja atakutana na mkono wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ukikutana na mtu kwa maneno machache akakuuliza kuhusu Tanzania, mwambie nchi inasonga mbele kwa uongozi sahihi, uelekeo sahihi na mwendokasi sahihi chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Mwambie ukiwa unajiamini, awaeleze na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezea pia masuala ya Ripoti ya Sensa, kwa sababu taarifa ilishazinduliwa, naomba iingie kwenye kumbukumbu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta binafsi, ushiriki wa sekta binafsi umeendelea kuongezeka ambapo jumla ya miradi 329; 127 ikiwa ya wageni na 111 ikiwa ya Watanzania ilisajiliwa, 91 ikiwa ya ubia ya wageni na Watanzania ilisajiliwa yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 4,517.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakuongeza dakika tatu, malizia; kengele ya pili ilishagonga.



**7 NOVEMBA, 2022**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo yanaonekana katika sura ya pili ya mapendekezo ya mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uandaaji wa bajeti, tumeeleza kwa kina mwongozo katika ukurasa wa 23 wa taarifa yangu. Kuhusu ufuatiliaji na tathmini tumeeleza kwa kina ukurasa wa 22. Maelezo ya kina kuhusu maelekezo mahususi ya Mwongozo yako katika sura ya kwanza, sura ya pili ya kitabu cha Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa tumeeleza kwa kina katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango sura ya tatu. Pia katika kuhitimisha Mapendekezo ya Mwongozo wa Mpango yatawezesha kukamilika kwa maandalizi ya bajeti ya mafungu kwa wakati, kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma, kuimarika kwa utawala bora unaozingatia misingi ya sheria, kuongezeka kwa uwajibikaji na ushiriki wa wadau mbalimbali, utekelezaji na ufuatiliaji wa tathmini ya mpango wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Maafisa Masuuli wa Wizara na idara zinazojitegemea, Mawakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi na mashirika ya Umma, wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyomo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024. Aidha, wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu Sheria ya Bajeti, Sura Na. 439 na kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili

**7 NOVEMBA, 2022**

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Kabla hujatoa hoja Mheshimiwa Waziri, hebu twende sehemu ya miradi ya maji, namba XV ya Kirumi.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, niko hapo.

**SPIKA:** Umefika hapo?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**SPIKA:** Sasa hiyo sehemu ya kwanza, hebu tusomee upya hizi takwimu kwa sababu nadhani wakati unazungumza hapa kwenye vijiji ni kwamba umefikia wastani wa asilimia 74.5 vijijini kutoka asilimia 72.3, yaani hiyo Juni, 2021. Sasa hapa badala ya kusema hii ni ya vijijini ilitoka hapo ukasema vijijini asilimia 74.5 halafu mijini 72.3. Kwa hiyo, watu wasije wakarudisha nyuma hizo. Tusomee vizuri hiyo sehemu ili takwimu zetu ziwe zimekaa vizuri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilivyosikia kengele nikaingiwa kile kiwewe Simba huwa inakipata ikiiona Yanga. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maji, naomba kurudia. Kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji ambapo hadi Juni, 2022 umefikia wastani wa asilimia 74.5 vijijini kutoka asilimia 72.3, yaani

**7 NOVEMBA, 2022**

Juni 2021, na mijini asilimia 86.5 kutoka asilimia 86 ya mwaka 2021. Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi...

**SPIKA:** Hapo tu mwanzoni. Huku kwingine ulienda sawa. Ahsante sana. Sasa unaweza kutoa hoja yako.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(Makofi)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Kwa hiyo, tunaendelea. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ili aje awasilishe mawazo ya Kamati kuhusu hoja hii. Mheshimiwa Daniel Sillo Baran.

**MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura ya 439 Kifungu cha 9 kifungu kidogo cha (1) kipengele (a) pamoja na Kanuni ya 113 fasili ya (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024

## **7 NOVEMBA, 2022**

pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024 ni mpango wa tatu katika mfululizo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026) uliobeba dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Hivyo, Mapendekezo ya Mpango huu yanalenga kuweka mazingira mahsusi ya kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024 yaliyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya taarifa hii yalifanyika kwa kurejea Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025, utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa wa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Dunia ya mwezi Februari, 2022 inayotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu saba ambazo ni Mapitio ya Hali ya Uchumi, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2021/2022, Utekelezaji wa Bajeti

## **7 NOVEMBA, 2022**

ya Mwaka 2021/2022, Utekelezaji wa Bajeti kwa Robo ya Kwanza ya Mwaka 2022/2023, Mwongozo wa Uandaaji wa Bajeti wa Mwaka 2023/24, Maoni ya Ujumla ya Kamati na sehemu ya mwisho ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi jumla, ambavyo ni msingi mzuri wa kupima ukuaji wa uchumi. Viashiria vilivyofanyiwa mapitio ni ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, deni la Serikali, mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi, pamoja na urari wa biashara na malipo ya nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022, yaani Januari hadi Machi, Uchumi wa Taifa ulikua kwa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba sekta zote zilizokua kwa kiasi kikubwa zimetokana na Serikali kuwekeza zaidi katika sekta hizo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi katika sekta za uzalishaji zenye manufaa makubwa kiuchumi kama vile sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, utalii na uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei wa Taifa ulifikia wastani wa asilimia 4.0 mwezi Agosti, 2022 sawa na kipindi kama hicho mwaka 2021, hivyo kuendelea kuwa ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kikanda wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Uchumi ya Kusini mwa Afrika, yaani EAC na SADC. Vilevile, katika kipindi cha

## 7 NOVEMBA, 2022

mwaka unaoisha mwezi Agosti, 2022, wastani wa mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi umeongezeka hadi asilimia 7.8 kutoka asilimia 3.6 kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwezi Agosti, 2021. Sambamba na hilo, mfumuko wa bei usiojumisha vyakula na nishati umepungua na kufikia wastani wa asilimia 3.2 katika mwaka unaoishia mwezi Agosti, 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwezi Agosti, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba sababu za mfumuko wa bei ni pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa yaani mafuta ya kula, mbolea, na petroli; kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika Soko la Dunia uliotokana na athari za UVIKO - 19 na vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine; na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula kwa nchi jirani uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi hususan katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuona namna ya kubadili changamoto hizi na kuwa fursa kwa Tanzania ambayo haijaanza kutumia ipasavyo rasilimali zake. Mfano vyanzo vya maji ambavyo vinaweza kutumika kwenye kilimo cha umwagiliaji katika uzalishaji wa chakula na matumizi ya nishati ya LNG. Hivyo ni wazi, lazima mpango wa mwaka unaofuata ujielekeze kwenye kutumia changamoto hizi kama fursa. Aidha, Serikali ihakikishe inaanza kutumia nishati ya gesi asilia inayozalishwa ndani ili kupunguza madhara ya kupanda kwa bei ya nishati ya mafuta inayosababishwa na vita ya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba katika akaunti zote tatu za Urari wa

## 7 NOVEMBA, 2022

Biashara na Malipo ya Nje (*Balance of Payment*), akaunti ya Urari wa Huduma na Uhamisho wa mali ndiyo pekee yenye ziada ukilinganisha na akaunti nyingine. Ziada iliyopatikana katika akaunti ya Urari wa Huduma na Uhamisho wa Mali ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta ya utalii. Hatua hii ni ya kupongeza hasa kwa uthubutu wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuitangaza Tanzania kupitia Filamu ya *Royal Tour*. Pamoja na manufaa ya sekta hii, Kamati imebaini kwamba Mpango wa mwaka 2023/2024 haujaipa kipaumbele sekta ya hii ya kilimo. Jedwali Na. 01 linaonesha urari wa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kwamba sekta ya utalii inakuwa mojawapo ya sekta zinazopewa kipaumbele katika kupewa fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024;

(ii) Kuiongezea fedha sekta ya utalii katika mgao unaofuata wa mkopo wa *ECF* katika mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Kuanzisha mkakati maalum wa kuvutia wawekezaji katika ujenzi wa hoteli za hadhi mbalimbali pamoja na kutoa vivutio mbalimbali ili kuvutia wawekezaji katika sekta ya utalii katika fukwe zetu;

(iv) Kufungua kanda nyingine za utalii hasa ukanda wa nyanda za juu kusini (*southern circuit*);

## 7 NOVEMBA, 2022

(v) Kuangalia upya uamuzi wa Serikali wa kuanza kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye Ndege za Kukodi (*Chartered Aircraft*) ili kuchochea utalii;

(vi) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kutangaza utalii kama ilivyofanyika kwa *Royal Tour*; na

(vii) Kuondoa migogoro kati ya wananchi na hifadhi, mapori tengefu, mbuga za wanyama na ushoroba ili tutunze maliasili zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Mwezi Oktoba 2022, Deni la Serikali lilifika Shilingi trilioni 71.56 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 64.50 katika kipindi kama hicho mwaka 2021, sawa na ongezeko la Shilingi trilioni 7.062 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 10.95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za ongezeko hilo ni kutokana na kupokelewa mikopo mipya kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kutolewa kwa hatifungani maalumu ya Shilingi trilioni 2.18 kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma linalohusu michango ya watumishi waliokuwa kwenye utumishi kabla ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba deni la Serikali ni himilivu kwa viwango vyote vya Kimataifa, Kamati inaishauri Serikali kwamba mikopo ielekezwe kwenye miradi ya maendeleo itakayochochea uzalishaji na mauzo nje ya nchi ili kuongeza mapato ya kigeni yatakayosaidia kulipa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, miradi yote inayochukua muda mrefu kukamilika na ina faida, itumie mikopo ya masharti nafuu na siyo yenye masharti ya



## 7 NOVEMBA, 2022

kibiashara ambayo kipindi cha kutoanza kulipa mtaji (*grace period*) ni kifupi na riba ni kubwa. Aidha, imekuwa ni rai ya Kamati ya muda mrefu kuweka na kutumia kiashiria cha ukomo wa ulipaji wa deni la Serikali kwa mapato ya ndani (*Debt Service to Domestic Revenue Ratio*) ili kuhakikisha kwamba mapato ya ndani yana uwezo wa kugharamia shughuli zote za Serikali pamoja na deni la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kwamba kiashiria hiki kinatambulika Kimataifa isipokuwa hakijawekewa ukomo katika muundo unaotumika kupima na kutathmini uhimilivu wa deni kutokana na utofauti wa sifa za masoko ya fedha ya ndani kwa nchi zinazotumia muundo huo hususan nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imetambua umuhimu wa kiashiria hicho na imeanza kuchukua hatua za awali za kufanyia utafiti na kisha uchambuzi na tathmini ikishirikiana na Taasisi za Kimataifa za Benki ya Dunia na *Macroeconomic and Financial Management Insitute of Eastern and Southern Africa* ili kuhakikisha kwamba matokeo ya kiashiria cha ukomo huo yanakubalika Kimataifa. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii muhimu na ni matumaini yake kuwa itaweza kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kutoka Shilingi trilioni 20.6 mwishoni mwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia Shilingi trilioni 24.59 mwezi Juni 2022, ikiwa ni ukuaji wa wastani wa asilimia 19.4, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.6 mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati imechambua na kubaini kwamba mikopo iliyoelekezwa

## 7 NOVEMBA, 2022

kwenye shughuli binafsi ni asilimia 38.3, mikopo iliyoелеkezwa kwenye shughuli za kibiashara ni asilimia 16.0, na mikopo iliyoелеkezwa kwenye shughuli za viwanda ni asilimia 10.7. Aidha, viwango vya riba vinavyotozwa kwenye mikopo vimepungua kutoka asilimia 16.6 hadi asilimia 16.41, sawa na kupungua kwa asilimia 0.19 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango hivi vya riba haviwezi kuchochea ukopaji kwa ajili ya uwekezaji wenye tija, badala yake mikopo mingi itaelekezwa kwenye shughuli binafsi. Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

(i) Benki Kuu ya Tanzania ibadili mkopo wa Shilingi trilioni moja kuwa dirisha maalumu ili kutoa mikopo kwa mabanki kwa sharti la kuwakopesha wakulima kwa riba ya 3% hadi 10%. Hadi tarehe 30 Oktoba, 2022 zilikuwa zimetumika Shilingi bilioni 95 tu; na

(ii) Serikali iendelee kuziongezea mtaji Benki za TADB na TIB ili ziweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2022/23. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali ilipanga kutumia Shilingi trilioni 15.26 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Serikali ilitumia jumla ya Shilingi trilioni 14.65 sawa na asilimia 96.0. Utekelezaji huu unaonesha wazi nia na dhamira ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwakwamua Watanzania kutoka katika wimbi la umasikini.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilipanga kutumia jumla ya Shilingi trilioni 15.01, na hadi kufikia Robo ya Kwanza ya Mwaka 2022/2023 Serikali imetumia jumla ya Shilingi trilioni 3.2, sawa na asilimia 21.32. Hivyo ni wazi kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Serikali inaweza kuwa imetoa fedha za maendeleo kati ya asilimia 85 hadi 90 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa miradi ya maendeleo ya kimkakati na iliyopewa kipaumbele na ina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya usafiri na usafirishaji; Reli ya Kisasa ya SGR na Reli ya TAZARA; Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wake, hivyo kufanikisha kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa kipande cha Tabora – Isaka (kilometa 165) ambapo maandalizi ya ujenzi yanaendelea; kuendelea na ununuzi wa mkandarasi kwa vipande vya Tabora – Kigoma (kilometa 411) na Kaliua – Mpanda – Karema (kilometa 321). Pamoja na mafanikio hayo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Taasisi za Serikali kuharakisha kuhamisha miundombinu yao ili kupisha ujenzi wa reli ya Kisasa (SGR);

(ii) Kulipa hati za madai ya mkandarasi kwa wakati ili kuepusha ongezeko la gharama za mradi kutokana na riba;

(iii) Serikali kuhakikisha kwamba Mkandarasi Mkuu wa Reli ya Kisasa analipa madeni yote ya *subcontractors* ambayo yanakadiriwa kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 12;

## 7 NOVEMBA, 2022

(iv) Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya *DRC Congo* iangalie uwezekano wa kufikisha Reli ya Kisasa (*SGR*) katika Bandari ya Kasanga iliyopo Wilaya ya Kalambo Mkoa wa Rukwa ili iunganishwe na Ferry kubwa kati ya Bandari ya Kasanga na Bandari ya Mulilo iliyoko upande wa *DRC Congo*. Hatua hii itaiwezesha reli yetu kuhudumia soko la nchi hiyo;

(v) Kuharakisha mapitio ya Sheria ya *TAZARA* ili kutoa fursa kwa Tanzania kuwekeza kwenye reli hiyo kwa upande wa Tanzania ili iwe na manufaa kwa upande wa Tanzania. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuingia ubia na makampuni makubwa ya uendeshaji wa njia za reli ili kupata vichwa na mabehewa kwa ajili ya reli ya *TAZARA*; na

(vi) Serikali kupitia Wakala wa Barabara Vijijini (*TARURA*) itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara zinazounganisha vituo vya *SGR* na makazi ya watu, mfano Stesheni ya Kongowe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*); Kamati inatambua umuhimu na mchango wa Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) kwa lengo la kuchochea uchumi katika sekta mbalimbali kama vile utalii, usafiri na usafirishaji wa mizigo. Hata hivyo, shirika hilo bado linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwepo wa madeni ya muda mrefu na yasiyolipika. Kutokana na changamoto hizo Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iendeele kutoa kipaumbele katika safari za ndege za kibiashara kwa ndege za *ATCL*. Sambamba na hilo, Serikali kupitia Kampuni ya Ndege ijijenge na kuwa na mifumo imara ya biashara ili iweze kujiunga na mifumo ya Kimataifa ya biashara ya ndege kama vile

## 7 NOVEMBA, 2022

*Airline Global Alliance*. Vilevile, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha safari katika nchi zenye makampuni/mashirika ya ndege yanayofanya safari nchini;

(ii) Serikali irekebishe mikataba ya ukodishaji ndege baina ya Kampuni ya Ndege (*ATCL*) na Wakala wa Ndege (*TGFA*). Kwa mfano, mikataba ya ukodishaji ndege haikuwa na kipengele cha msamaha wa matukio ya majanga, hivyo, *TGFA* iliendelea kuitoza fedha za ukodishaji ndege za *ATCL* hata wakati wa janga la UVIKO-19 ambapo ndege zilikuwa hazifanyi kazi. Kamati inaamini kwamba kurekebisha mikataba hii kutaboresha utendaji kazi wa *ATCL*;

(iii) Kuboresha viwanja vya ndege kwa kuviwekea taa ili kuongeza safari za ndege za *ATCL* kuliko hivi sasa ambavyo ndege zinaruka muda wa mchana tu na kutoruka wakati wa usiku;

(iv) Kuongeza safari za ndege kwenye maeneo/mataifa ambayo Tanzania inapokea watalii wengi;

(v) Serikali kuboresha jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ambalo kwa muda mrefu limekuwa katika hatua za usanifu. Kiwanja hiki kina fursa ya kuwa *transit route* ya ndege za Rwanda, Burundi na *DRC Congo*; na

(vi) Serikali ifanye marekebisho ya deni la *ATCL* ili liwe sehemu ya mtaji. Hii itatoa nafasi kwa *ATCL* kuaminika na taasisi nyingine kibiashara. (*Makofi*)

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kufua umeme wa maji wa Mwalimu Julius Nyerere (MW 2,115); Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba taarifa ya mpango iliyowasilishwa na Serikali haijaonesha ni lini mradi huu unatarajiwa kukamilika. Japokuwa taarifa ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) inaonesha kwamba Mkandarasi wa mradi huu ameongezewa muda wa miezi 12 kukamilisha mradi huu toka tarehe 14 Juni, 2022 iliyopangwa katika mkataba hadi tarehe 15 Juni, 2023. Sambamba na hilo, Kamati ilibaini masuala ya msingi yafuatayo:-

(i) Sababu za mkandarasi kuomba kuongezewa hazikuwa za msingi na bado Serikali imekubali kumwongezea muda wa utekelezaji;

(ii) Mpango kazi uliowasilishwa na Mkandarasi Serikalini unaonesha kwamba mradi huu utakamilika Julai, 2024, kinyume na muda wa miezi 12 kukamilisha mradi huu, yaani hadi 15 Juni, 2023 ambao Serikali imemwongezea mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na masuala yaliyobainika katika Mradi huu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Kamati inashauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa, moja ya changamoto iliyosababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi huu kwa wakati ni Mkandarasi kukiuka baadhi ya masharti ya mkataba ikiwemo mkandarasi kuchelewa kuleta wataalamu wanaohitajika kimkataba, mkandarasi kujenga chini ya kiwango kwa baadhi ya maeneo ya bwawa, kwa mfano, handaki la kuchepusha maji (*diversion channel*) la Mto Rufiji lilijengwa kwa *methodology* hafifu na hivyo kusababisha maji kuingia katika handaki kabla ya ujenzi

## 7 NOVEMBA, 2022

wake kukamilika. Hivyo basi ni vyema Serikali ikatanzua changamoto hii bila kuleta hasara kwa nchi;

(ii) Serikali iweke mikakati ya kulinda vyanzo vya maji vinavyozunguka mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ili kuwezesha uwepo wa maji ya kutosha pindi mradi utakapokamilika hasa ukizingatia mabadiliko ya tabia nchi;

(iii) Serikali ifanye ukaguzi wa kina (*special audit*) kwenye mradi huu ili kuhakikisha fedha zilizotumika zinaendana na matakwa ya mradi na endapo mkandarasi atakiuka masharti ya mkataba hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi yake; na

(iv) Serikali ihakikishe fedha za michango ya hisani za jamii (CSR) kiasi cha shilingi bilioni 262 zitumike kwenye miradi iliyopangwa sambamba na miradi mingine katika maeneo ambayo mradi unatekelezwa katika Mkoa wa Pwani na Morogoro na si vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uunganishwaji wa umeme vijijini; Kamati imebaini kwamba vijiji 8,804 kati ya vijiji 12,345 vimeunganishwa na umeme Tanzania Bara, sawa na asilimia 71.32. Jumla ya shilingi bilioni 313.40 zimetumika katika mwaka 2021/2022 na shilingi bilioni 84.90 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa iliyotolewa na Serikali ni taarifa ya kijumla (*cumulative*) na hivyo ni vigumu kupima ufanisi wa kasi ya uunganishaji wa umeme vijijini. Mfano, miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kwa mwaka huu imekumbwa na changamoto mbalimbali kama vile kusitishwa kwa mikataba na upandaji wa bei za vifaa vya umeme, hivyo ni vigumu kujua ni kiasi gani imetekelezwa kwa kulinganisha na lengo. Kamati inashauri Taarifa ya Miradi hii iwe inawasilishwa kwa kulinganisha lengo la mwaka husika na

## 7 NOVEMBA, 2022

vijiji vilivyounganishwa na umeme na sio kutoa taarifa ya vijiji vyote vilivyounganishwa tangu mradi ulipoanza. Hatua hii italetwa uwazi na uwajibikaji. Aidha, ni vyema Serikali ikafanya tathmini ya vijiji na vitongoji halisi vilivyofikiwa na umeme wa REA hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Miundombinu; Miradi ya Bandari, Kamati imepitia tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga na ina maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Tanga; Kamati imebaini Bandari ya Tanga haihudumii meli na shehena ya kutosha kutokana na umbali wa kilomita 1.7 toka gatini hadi meli zinapotia nanga na hivyo kuwa na kasi ndogo ya kupakia na kushusha shehena ya mizigo ya meli ambazo zilipaswa kuhudumiwa nangani. Kamati inaishauri Serikali kufanya maboresho ya Bandari kwenye miundombinu, mitambo na vifaa ili kuvutia meli na shehena nyingi. Aidha, Serikali iweke mkakati wa kimasoko mahsusi kwa ajili ya Bandari ya Tanga ambao lengo lake ni kuteka soko la Kaskazini mwa Tanzania na nchi jirani za Rwanda, Burundi na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Mtwara; Kamati imebaini kwamba kuna uhaba wa makasha katika Bandari ya Mtwara hivyo meli nyingi zinaepuka gharama za kwenda Bandari ya Mtwara bila kuwa na shehena inayoenda kushushwa katika bandari hiyo ili ziweze kubeba zao la korosho. Hii ndiyo sababu ya msingi ambayo inasababisha bandari hiyo isitumike kwa ajili ya kusafirisha zao la korosho. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari kuhakikisha kwamba inatatua changamoto ya upatikanaji wa makasha ili kuifanya Bandari ya Mtwara kutumika ipasavyo.



## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwamba, Serikali itafute ufumbuzi wa changamoto ya mlundikano na msongamano wa malori katika eneo la Malawi cargo na mlundikano wa magari katika gati la magari (RO-RO). Vilevile, Kamati inaishauri Serikali isimamie kanuni za EWURA zinazoelekeza kwamba mafuta yachukuliwe katika bandari iliyopo katika Kanda ili kuchochea matumizi ya bandari za kanda husika. Kamati inashauri Mikoa ya Kaskazini itumie Bandari ya Tanga na Mikoa ya Kusini itumie Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Bagamoyo; Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika Bandari ya Dar es salaam ili ijiendeshe kwa ufanisi. Hata hivyo, bandari hiyo haina eneo la kuendelea na upanuzi kulingana na eneo ilipo. Aidha, Mradi wa SGR unaoendelea ni lazima kuwe na bandari kubwa ya kisasa ambayo italetta mizigo ya kutosha ili reli hiyo iwe na manufaa. Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia nzuri ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Bagamaoyo ambayo itazingatia manufaa mapana ya Taifa kwa vizazi vya sasa na vijavyo ili kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo ya TEHAMA; Mifumo ya Kutunza kumbukumbu za Watumishi; Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyoanza kuchukua kwenye kuhuisha na kuunganisha mifumo mbalimbali ya TEHAMA, ukiwemo Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Watumishi na Malipo ya Mishahara (HCMIS). Kamati imebaini kwamba bado kuna changamoto katika utunzaji wa nyaraka za watumishi wa umma kidijitali. Mfano, mtumishi anaajiriwa na Serikali, mafao yake yanakatwa na Serikali kwa niaba yake, lakini anapofika

## 7 NOVEMBA, 2022

umri wa kustaafu anatakiwa kuwasilisha nyaraka hizo kwa Serikali iliyomwajiri. Kamati inashauri kwamba katika mwaka ujao wa fedha, Serikali ianzishe na kuendeleza utunzaji wa kumbukumbu za watumishi kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifumo ya ukusanyaji wa mapato; Mifumo ya Mamlaka ya Mapato na Mamlaka ya Bandari; uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mapato ya Serikali yamekuwa yakipotea kutokana na kukosa ufanisi kwenye ukusanyaji, uwepo wa mifumo dhaifu pamoja na kutosomana kwa mifumo hiyo. Hivyo, Kamati inaendelea kusesitiza kwamba, mifumo ya ukusanyaji ya mapato ya Mamlaka ya Mapato TRA ambayo ni (IDRAS, TANCIS) iboreshwe na kuunganishwa ili iweze kukusanya mapato kwa ufanisi na Serikali kupata mapato stahiki. Aidha, Serikali iendeleo kuunganisha mfumo wa GePG katika taasisi zote za umma ili utumike kikamilifu katika kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifumo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa; uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba mapato mengi ya halmashauri hasa yale yanayokusanywa nje ya mfumo hupotea bila kuingizwa kwenye akaunti za Serikali. Aidha, Kamati imebaini kwamba kutokusomana kwa mifumo ya mapato ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kunaongeza tatizo la kupotea kwa mapato ya Serikali. Hivyo, Kamati inashauri kuweka katazo la kutokusanya fedha yoyote ya umma bila kutumia mfumo na kuhakikisha mashine zote za kukusanyia mapato ya Serikali za Mitaa (POS) zinatumiwa kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Barabara na Madaraja makubwa; Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi

## 7 NOVEMBA, 2022

mbalimbali ya barabara na madaraja nchini na ina ushauri ufuatao:-

(i) Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukarabati barabara zote zinazounganisha mikoa ambazo hazijafanyiwa matengenezo muda mrefu. Aidha, Serikali kuendelea kutoa fedha kwa wakati ili barabara zetu ziweze kukamilika kama ilivyopangwa;

(ii) Ni vyema Serikali ikachagua barabara chache kwa kila mwaka wa fedha ili zitekelezwe kwa Bajeti iliyopangwa katika mwaka husika, kuliko kuwa na miradi mingi ya barabara ambayo inazalisha madai kutokana na kuchelewa kulipwa (*arrears*). Kwa msingi huo Kamati inashauri kwamba barabara zitakazotekelezwa ziwe ni zile ambazo ni za Kimkakati.

(iii) Serikali kuangalia uwezekano wa kuwa na mikataba ya ujenzi wa barabara ambayo haitoi fursa ya kulipa riba kubwa pindi malipo yanapochelewa; na

(iv) Kupunguza kiasi kikubwa cha matumizi ya fedha kwenye ubunifu (*design*) na ubunifu wa kina (*detailed design*) kwa miradi ambayo haitekelezwi hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya Taifa; Kuanzia mwaka 2012 hadi mwezi Septemba, 2022, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilikuwa imesajili na kutoa namba kwa watu 19,509,202, kati ya hao waliokuwa wamepewa vitambulisho katika kipindi chote hicho cha miaka 10 ni Watu 11,117,264 sawa na asilimia 56 ya lengo. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba zoezi la uandikishaji na utoaji wa vitambulisho vya Taifa limekuwa likitekelezwa kwa kasi ndogo kutokana na changamoto zifuatazo:-

## 7 NOVEMBA, 2022

(i) Uwepo wa deni la Mkarandarasi lenye thamani ya Dola za Marekani milioni 7.58 sawa na shilingi bilioni 17 ambalo limelipwa na Serikali mwezi Oktoba, 2022;

(ii) Kuchelewa kwa upatikanaji wa Kadighafi za Vitambulisho vya Taifa milioni 13 kutokana na uhaba wa fedha na *smartcard chips* katika soko la dunia;

(iii) Kuchelewa kupatikana kwa fedha kiasi cha shilingi bilioni 42.5 kwa ajili ya ununuzi wa kadighafi 11,775,728; na

(iv) Upungufu wa Vitendea kazi pamoja na Rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaushauri ufuatao kwa Serikali: -

(i) kuhakikisha kwamba kiasi cha Shilingi bilioni 42.5 zinapatikana kwa mkupuo mmoja au miwili ili utengenezaji na ugawaji wa vitambulisho ufanyike kwa kasi;

(ii) Kufungamanisha Taarifa baina ya Taasisi za Serikali mfano endapo mwananchi ataenda kuchukua Hati ya Kusafiria Taarifa zake za awali zichukuliwe *NIDA* na sio mwananchi huyo kuwasilisha taarifa zile zile alizoziwasilisha *NIDA*;

(iii) Kuangalia uwezekano wa kuanza kuchukua Taarifa hata kwa watoto wa chini ya miaka 18 ili jinsi anavyokua ziwe zinahuishwa kuliko kusubiria hadi afike miaka 18; na

## **7 NOVEMBA, 2022**

(iv) Kutumia Ofisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa kugawa Vitambulisho ambavyo bado havijachukuliwa na wananchi ambavyo viko Takribani 785,222.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo ni mhimili wa maendeleo ya uchumi ilichangia asilimia 26.1 mwaka 2021 kwenye Pato la Taifa na kutoa fursa za ajira zaidi ya asilimia 65 na hivyo kuifanya ndio sekta pekee inayotegemewa na wananchi wa kipato cha chini. Vilevile, kilimo kina uhusiano na sekta nyingine katika kutoa malighafi kwa viwanda na soko kwa bidhaa zilizotengenezwa. Kilimo kinachukua sehemu muhimu katika kukua kwa uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na manufaa mapana ya sekta hii bado hakijaweza kukua kwa kile kiwango kinachostahili ambapo sekta hii imekua kwa asilimia 3.9 mwaka 2021. Hii imetokana na sababu mbalimbali zikiwemo pembejeo zisizotosheleza kama vile mbegu bora, mbolea na dawa za kilimo, mfumo wa kizamani wa uoteshaji mazao na ucheleweshaji wa maendeleo ya miundombinu kama vile, skimu za umwagiliaji, miundombinu ya masoko, barabara za mashambani na usindikaji wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya sekta hii imepanda takribani mara tatu na kufikia shilingi bilioni 954 mwaka 2022/2023 kutoka shilingi bilioni 294 mwaka 2021/2022. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua hii katika kuiinua sekta hii muhimu ya kilimo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza matumizi ya teknolojia bora katika uzalishaji wa mazao ili kuongeza mapato ya kigeni pamoja na upatikanaji wa malighafi za uzalishaji viwandani. Aidha, Serikali kupitia mifumo yake iendelee kutekeleza yafuatayo:-

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Vituo vya Utafiti wa Mbegu Bora; Kamati imebaini kwamba katika kipindi cha miaka kumi Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (*TARI*) imegundua aina 146 za mbegu bora za mazao mbalimbali kupitia vituo vyake vya utafiti. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023, sekta ya utafiti wa mbegu imetengewa jumla ya shilingi bilioni 40.73. Vilevile, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa miradi ya uzalishaji wa mbegu chini ya mkopo wa *ECF* umekuwa wa kusuasua. Hivyo, Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

(i) Ili mbegu zilizogunduliwa na *TARI* zipatikane kwa wingi na ziwafikie wakulima ni lazima kuwe na ushirikiano kati ya *TARI* na Wakala wa Taifa wa Mbegu; na

(ii) Serikali iendeele kuwekeza zaidi kwenye Kituo cha *TARI* ili kiwe na uwezo wa kufanya utafiti na kuzalisha mbegu bora zinazoweza kuhimili mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Huduma za Ugani; Kamati imebaini kwamba kati ya Maafisa Ugani 20,538 wanaohitajika waliopo ni 6,704, sawa na asilimia 30 ya mahitaji. Vilevile, Kamati imetaarifiwa kwamba kuna mfumo uitwao M-Kilimo unaotumika kuwafikia wakulima kutoa huduma za ugani ili kuziba pengo la mahitaji ya Maafisa Ugani wanaohitajika. Aidha, Kamati imebaini kwamba pikipiki 7,000 zilizogawiwa na Serikali hazitumiki kama ilivyokusudiwa kutokana na kukosekana kwa mafuta ya kuendeshea pikipiki hizo. Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

## 7 NOVEMBA, 2022

- (i) Kuhakikisha kwamba halmashauri zote nchini zitenge fedha kutoka kwenye mapato ya ndani (*own source*) kwa ajili ya Maafisa Ugani;
- (ii) Pamoja na Serikali kununua vifaa vya kupimia afya ya udongo, bado huduma hiyo haijaanza kutolewa kutokana na kukosekana kwa vifaa vingine vinavyoweza kupima afya ya udongo; na
- (iii) Kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima namna ya kutumia mfumo wa M-Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Mbolea; Kamati inatambua jitihada za Serikali za kuhakikisha upatikanaji wa mbolea kwa ruzuku ambapo hadi hivi sasa zimetolewa tani 46,000 za mbolea za aina mbalimbali kupitia makampuni na mawakala walioajiriwa. Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:

(i) Kuhakikisha kwamba makosa yaliyotendeka katika mfumo wa vocha za pembejeo hayajirudii kwenye ruzuku ya mbolea inayotolewa;

(ii) Serikali kuwawezesha wawekezaji wa ndani kimtaji ili waweze kutumia malighafi zinazopatikana nchini kuzalisha mbolea ya kutosha; na

(iii) Kuendelea kuwekeza kwenye Kiwanda cha Viuadudu Kibaha ili kiweze kuzalisha mbolea pamoja na viuatilifu. Hadi hivi sasa Serikali imewekeza kiasi cha shilingi bilioni 83 na bado hiajaweza kupata manufaa yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mitaji kwa ajili ya uendelezaji sekta ya Kilimo; Kamati inaipongeza Serikali

**7 NOVEMBA, 2022**

kwa kuwekeza katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kwa kuweka mtaji wa kianzio kiasi cha shilingi bilioni 60 na hivi sasa imeshawekeza jumla ya shilingi bilioni 268. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza mtaji katika benki hii ili kuchochea uwekezaji na maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Ni vigumu kutegemea benki za biashara kukopesha sekta ya kilimo kwa sababu sekta hiyo ina vihatarishi vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia tangazo la Gavana wa Benki Kuu la tarehe 27 Julai, 2021 lililokuwa na kichwa cha habari *Policy Measures to Promote Credit to Private Sector and Lower Interest Rates*. Tangazo hilo lilikuwa na lengo la kutumia nyenzo mbalimbali za Benki Kuu katika kusimamia sera ya fedha ili kuongeza ukwasi katika mabenki na mikopo kwa sekta binafsi katika kipindi cha janga la UVIKO -19. Aidha, Serikali ilianzisha mkopo maalum kwa mabenki wenye thamani ya shilingi trilioni moja ili sekta ya kilimo ikopeshwe kwa asilimia kati ya tatu hadi 10 "*Introduction of a special Loan amounting to TZS 1.0 Trillion to Bank and other financial institution for on lending private sector*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masoko ya Mazao ya Biashara; Kamati inaishauri Serikali kuwezesha upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali ihakikishe miundombinu ya maghala yanayomilikiwa na Serikali katika Mataifa ya DRC Congo na Sudani Kusini iunganishwe na wafanyabiashara wa ndani ili itumike kikamilifu sio kwa Taasisi za Serikali za (NFRA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bei ya Korosho katika Soko la Dunia imeshuka; hii ni kutokana na ukweli kwamba



## 7 NOVEMBA, 2022

mazao ya kilimo ambayo hayajaongezwa thamani yana asili ya kuathiriwa na mabadiliko ya bei. Endapo kuna mabadiliko madogo kwenye bei athari yake katika mahitaji ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba Makubwa (*Block Farming*); Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuanzisha mashamba makubwa ya umwagiliaji *block farming* katika maeneo mbalimbali kama vile Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino (ekari 11,453), Halmashauri ya Wilaya ya Bahi (ekari 3,560) na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya (ekari 65,000). Kamati imebaini kwamba asilimia kubwa ya mashamba haya yapo katika maeneo ambayo hayana vyanzo vya uhakika vya maji kama vile mito au maziwa, hivyo ni vyema Serikali ikaweka mkakati wa kuweka mashamba ya namna hii katika maeneo ambayo yana vyanzo vya uhakika vya maji ili kufanya kilimo cha umwagiliaji kiwe chenye tija kuliko kutegemea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo cha Umwagiliaji na Ujenzi wa Mabwawa; Tanzania ina jumla ya hekta 29,000,000 za kilimo ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Aidha, hadi kufikia mwaka 2021/2022, kiwango cha Ardhi ambayo iko chini ya umwagiliaji ni hekta 800,000 sawa na asilimia 2.75, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kujenga miundombinu ya umwagiliaji pamoja na mabwawa kama vile Bwawa la Kidunda na Farkwa ili kuwa na kilimo cha uhakika na chenye tija kuliko kutegemea mvua pekee. Hatua hii itasaidia kuwa na kilimo cha uhakika hasa kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi ambayo Taifa inakumbana nayo.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato katika Halmashauri; Kamati inatambua juhudi za Serikali za kuwajengea uwezo watumishi kwenye halmashauri mbalimbali nchini jinsi ya kuandaa maandiko ya miradi inayokidhi vigezo. Aidha, Kamati inatambua kwamba Serikali imeandaa mkakati wa ugharamiaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri kupitia vyanzo mbadala. Hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali bado hazibadilishi sera ya mradi huu kupelekwa kwenye halmashauri zenye uwezo wa kifedha na si zile zenye hali mbaya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuna haja ya Serikali kuangalia sera ya miradi hii ambayo inaelekeza fedha hizi kwenye Halmashauri za Miji na Majiji na hivyo halmashauri ambazo zina hali mbaya na zinahitaji usaidizi wa fedha ili kuongeza mapato hazipati fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kufanya mgawanyo wa fedha za uwekezaji kati ya zile zenye hali mbaya na majiji na miji ili kuzisaidia zote ziweze kuongeza mapato na kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utoaji wa Mikopo ya Serikali kwa Wajasiliamali; kuna changamoto kubwa ya usimamizi na uratibu wa mikopo inayotolewa na Wizara, Idara, Wakala na Taasisi za Serikali. Mfano, Mamlaka ya Serikali za Mitaa inatoa mikopo ya asilimia 10, mikopo kwa wachimbaji wadogo wa madini inatolewa na Wizara ya Nishati na kuna mikopo inatolewa na *SELF*, *TADB*, *NEEC*, hizi ni baadhi ya Taasisi za Serikali zinazotoa mikopo.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kufanya kwanza tathmini ya ufanisi wa mikopo hiyo na kufanya uratibu na usimamizi wa pamoja wa namna ya utoaji wa mikopo Serikalini. Aidha, uangaliwe uwezekano wa kuunganisha mikopo hii ili kuwepo na taasisi moja ya Serikali itakayokuwa na jukumu la kutoa mikopo kwa sekta mbalimbali kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushiriki wa Sekta Binafsi; katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/2026 Serikali ilibainisha kwamba Sekta Binafsi katika mwaka 2023/2024 inatakiwa kuchangia jumla ya Shilingi trilioni 9.08, kati ya Fedha hizo Sekta Binafsi ya ndani ilitarajiwa kuchangia Shilingi trilioni 5.17 na ya nje Shilingi trilioni 3.91. Pamoja na kwamba Serikali imebainisha kuwa Sekta Binafsi imeshirikishwa katika mchakato wa maandalizi ya mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Mwaka 2023/2024, bado mchango wake hauonekani katika utekelezaji wa Mpango. Kamati inashauri Serikali ni vyema Mpango wa mwaka 2023/2024 ukaainisha maeneo hayo ya ushirikishwaji wa Sekta Binafsi na inatarajiwa kuchangia kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP); ni namna pekee ya kupunguza mzigo kwa Serikali kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo yenye sura ya kibiashara. Matumizi ya njia hii yanatoa unafuu kwenye mapato ya Serikali ili Serikali ijielekeze kwenye maeneo ambayo hayana mvuto wa kibiashara. Pamoja na uwepo wa Sheria ya Ubia, Sura ya 103 na kufanya mabadiliko makubwa mwaka 2018, bado chanzo hiki cha kugharamia miradi ya maendeleo hakijaleta

## 7 NOVEMBA, 2022

manufaa yaliyokusudiwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo:-

(i) Mwamko mdogo wa Sekta ya Umma kutekeleza miradi kwa njia ya ubia;

(ii) Maandalizi duni au kutokufanya maandalizi kabisa kwa miradi ambayo inaweza kutekelezwa kwa njia ya ubia (*PPP*);

(iii) Uwezo mdogo wa Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi za Serikali kuandaa maandiko ya miradi inayotekelezwa kwa njia ya ubia;

(iv) Kiwango kikubwa cha Mtaji wa chini (*minimum capital*) cha dola za Marekani milioni 20 ambayo ni sawa na Shilingi bilioni takribani 46.3 ili mradi utekelezwe kwa njia ya Ubia; na

(v) Masharti magumu ya kutekeleza miradi inayobuniwa na Sekta Binafsi ili itekelezwe kwa njia ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kwamba, katika mwaka ujao wa fedha kufanyia kazi changamoto zilizoinishwa hapo juu ili miradi ya ubia ianze kutekelezwa. Aidha, Kamati imebaini kwamba miradi iliyotajwa katika mpango kutekelezwa kwa njia ya ubia ni ile ile na imekuwa haitekelezwi. Vilevile, Kamati inaitaka Serikali katika mwaka ujao wa fedha kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli kubuni, kuandaa na kutekeleza miradi kwa mfumo wa *PPP* hasa yenye sura ya kibiashara.

## 7 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi katika kipindi cha Mwaka 2021/2022; Kamati imebaini kwamba miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini kwa mwaka 2021/2022 ilikuwa ni 253 tu ukilinganisha na jumla ya miradi 2,034 iliyoko katika kitabu cha Miradi ya Maendeleo cha Bajeti ya mwaka 2021/2022, hii ni sawa na asilimia 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika mbili malizia, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ambavyo imeoneshwa kwenye taarifa yetu kubwa. Kwa hiyo naomba Waheshimiwa Wajumbe waipitie, lakini utekelezaji wa Bajeti Mwaka 2021/2022 ni kama ambavyo iko kwenye taarifa kubwa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niweze kuhitimisha. Kama nilivyosema taarifa hii imesheheni mambo mazuri kabisa kwa hiyo naomba Waheshimiwa Wabunge muipitie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naomba kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mbunge

## 7 NOVEMBA, 2022

na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa miongozo yako iliyoiwzesha Kamati yetu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Naibu Spika, kwa ushirikiano wake kwa Kamati. Vilevile ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwingulu Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wake kwa Kamati. Aidha Kamati inamshukuru pia Ndugu Jenifa C. Omolo Naibu Katibu Mkuu, Utawala na Huduma za Mfuko Mkuu kwa ushirikiano wake wakati wa majadiliano ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti ya 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omari Kigua Mbunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa umakini na weledi wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu taarifa hili. Naomba majina yao yote yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelewa Mwihambi (*ndc*), kwa kuiwzesha Kamati kutekeleza majukumu yake kama ipasavyo pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Emmanuel Rhobi na Makatibu wa Kamati Ndugu Liliani Masabala, Ndugu Wilfred Akassi, Ndugu Maombi Kakozi na Ndugu Triphina Tanzania kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalam hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**7 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI  
KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA  
TAIFA UNAOKUSUDIWA KUTEKELEZWA NA SERIKALI KWA  
MWAKA 2023/2024 PAMOJA NA MWONGOZO WA  
KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA  
WA FEDHA 2023/2024 - KAMA YALIVYOWASILISHWA  
MEZANI**

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura ya 439 Kifungu cha 9(1) kipengele (a) pamoja na kanuni ya 113 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24.

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 ni Mpango wa tatu katika mfululizo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) uliobeba Dhima ya “Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”. Hivyo, Mapendekezo ya Mpango huu yanalenga kuweka mazingira mahsusi ya kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 pamoja na Mapendekezo ya

## 7 NOVEMBA, 2022

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24 yaliyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake. Maandalizi ya Taarifa hii yalifanyika kwa kurejea Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021/22-2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025, utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa wa mwaka wa fedha 2021/22, Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23 na Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Dunia ya mwezi Februari, 2022 inayotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu saba ambazo ni Mapitio ya Hali ya Uchumi, Utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2021/22, Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22, Utekelezaji wa Bajeti kwa robo ya kwanza ya mwaka 2022/23, Mwongozo wa Uandaaji wa Bajeti ya mwaka 2023/24, Maoni ya Ujumla ya Kamati na sehemu ya mwisho ni Hitimisho.

### 2.0. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi ujumla ambavyo ni msingi mzuri wa kupima ukuaji wa uchumi. Viashiria vilivyofanyiwa mapitio ni Ukuaji wa Uchumi, Mfumuko wa Bei, Deni la Serikali, Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi, pamoja na Urari wa Biashara na Malipo ya nje ya nchi.



## 2.1. Uchumi wa Dunia

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Julai, 2022 katika mwaka 2021 uchumi wa Dunia ulikua hadi kufikia **asilimia 6.1** kutoka ukuaji hasi wa **asilimia 3.1** mwaka 2020. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua hadi **asilimia 3.2** mwaka 2022 na **asilimia 2.9** mwaka 2023. Kwa kuwa uchumi wa Dunia umekua kutoka hasi hadi chanya, inamaanisha kwamba kutakuwa na ongezeko la mahitaji ya mitaji katika soko la Dunia. Ukuaji huu unaonyesha kwamba kwa kiasi kikubwa kutakuwa na ongezeko la riba na ugumu wa upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwenye soko la fedha la Kimataifa. Hivyo inaweza kuathiri upatikanaji wa mikopo hiyo nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuanza kutumia vyanzo bunifu na mbadala vya mapato vilivyobainishwa kwenye mpango ambavyo havijatumika kama vile hati fungani za Halmashauri (Municipal bonds), hati fungani za bluu (Blue bonds), hati fungani za makampuni (Corporate bonds), micro-saving bonds, lease financing, Bima na ugharamiaji hatarishi (risk financing), hati fungani za miundombinu (Infrastructure bonds), hati fungani za kiislam (SUKUK), hati fungani za mazingira (Green bonds) na Dhamana za muda wa kati. Hali hii italiwezesha Taifa kuepukana na mikopo yenye masharti magumu ambayo itaongeza deni la Serikali kwa kiasi kikubwa.

## 2.2. Ukuaji wa Uchumi wa Taifa

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022 (Januari hadi Machi), Uchumi wa Taifa ulikua kwa **asilimia 5.4** ikilinganishwa na **asilimia 5.0** katika

## 7 NOVEMBA, 2022

kipindi kama hicho mwaka 2021. Sekta zilizokua kwa kasi kubwa ya ukuaji ni pamoja na: Maji safi na maji taka (**asilimia 11.9**); fedha na bima (**asilimia 10.0**); uchimbaji madini na mawe (**asilimia 8.5**); huduma nyingine za kijamii (**asilimia 8.5**); na umeme (**asilimia 8.3**).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba sekta zote zilizokua kwa kiasi kikubwa zimetokana na Serikali kuwekeza zaidi katika sekta hizo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi katika sekta za uzalishaji zenye manufaa makubwa kiuchumi kama vile sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Viwanda, Utalii na Uvuvi wa bahari kuu.

### 2.3. Mfumuko wa Bei

**Mheshimiwa Spika**, Mfumuko wa bei wa Taifa ulifikia wastani wa **asilimia 4.0** mwezi Agosti, 2022 sawa na kipindi kama hicho mwaka 2021, hivyo kuendelea kuwa ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kikanda wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Uchumi ya Kusini mwa Afrika (EAC na SADC). Vilevile, Katika kipindi cha mwaka unaoishia mwezi Agosti 2022, Wastani wa Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi umeongezeka hadi **asilimia 7.8** kutoka **asilimia 3.6** kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho cha mwezi Agosti 2021. Sambamba na hilo, Mfumuko wa Bei usiojumuishia vyakula na nishati (*Core Inflation*) umepungua na kufikia wastani wa **asilimia 3.2** katika mwaka unaoishia mwezi Agosti, 2022 ikilinganishwa na **asilimia 4.5** mwezi Agosti, 2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba sababu za mfumuko wa bei ni pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa (mafuta ya kula, mbolea, na petroli), kuvurugika

kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia uliotokana na athari za UVIKO - 19 na vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula kwa nchi jirani uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi hususan katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuona namna ya kubadili changamoto hizi na kuwa fursa kwa Tanzania ambayo haijaanza kutumia ipasavyo rasilimali zake mfano vyanzo vya maji ambavyo vinaweza kutumika kwenye kilimo cha umwagiliaji katika uzalishaji wa chakula na matumizi ya Nishati ya LNG, hivyo ni wazi lazima mpango wa mwaka unaofuata ujielekeze kwenye kutumia changamoto hizi kama fursa. Aidha, Serikali ihakikishe inaanza kutumia nishati ya gesi asilia inayozalishwa ndani ili kupunguza madhara ya kupanda kwa bei ya nishati ya mafuta inayosababishwa na vita ya Urusi na Ukraine.

#### **2.4. Urari wa Biashara na Malipo**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba katika akaunti zote tatu za Urari wa biashara na malipo ya nje (Balance Of Payment), akaunti ya Urari wa Huduma na Uhamisho wa mali ndio pekee yenye ziada (positive balance), ukilinganisha na akaunti nyingine. Ziada iliyopatikana katika akaunti ya Urari wa Huduma na Uhamisho wa mali ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta ya Utalii. Hatua hii ni ya kupongeza hasa kwa uthubutu wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuitangaza Tanzania kupitia Filamu ya Royal Tour. Pamoja na manufaa ya sekta hii Kamati imebaini kwamba mpango wa mwaka 2023/24 haujaipa kipaumbele sekta ya hii.

**7 NOVEMBA, 2022**

<b>Na</b>	<b>Mwaka</b>	<b>2020/21</b>	<b>2021/22</b>	<b>Badiliko(%)</b>
-----------	--------------	----------------	----------------	--------------------

**Jedwali. Na. 1 Urari wa Malipo**

## 7 NOVEMBA, 2022

<b>Na</b>	<b>Mwaka</b>	<b>2020/21</b>	<b>2021/22</b>	<b>Badiliko(%)</b>
1.	<b>Urari wa Bidhaa</b>	- 2,100.10	- 4,616.40	<b>119.8</b>
	Mauzo nje	6,446.40	7,079.00	10.1
	Uagizaji nje	8,546.60	1,713.40	37.1
	<b>Urari wa Huduma</b>	<b>1,069.70</b>	<b>1,917.40</b>	<b>79.2</b>
	Mapato	2,364.50	3,919.70	65.8
	Malipo	1,294.90	2,002.40	54.6
	<b>Urari wa Bidhaa na huduma</b>	- 1,030.50	- 2,699.00	<b>161.9</b>
	Mauzo ya bidhaa na huduma	8,811.00	11,016.70	25
	Uagizaji bidhaa na huduma	9,841.40	13,715.70	39.4
	<b>Urari wa Mapato ya vitega uchumi</b>	- 1,247.30	<b>1,277.00</b>	<b>2.4</b>
	Mapato	67.40	153.50	127.7
	Malipo	1,314.70	1,430.50	8.8
	<b>Uhamisho wa mali</b>	<b>452.10</b>	<b>589.70</b>	<b>30.4</b>
	Zilizoingia	513.50	700.20	36.4
	Kwa serikali kuu	76.70	122.40	59.7
	Zilizotoka	61.40	110.50	80.2
	<b>Urari wa malipo ya kawaida</b>	- 1,825.60	<b>3,386.30</b>	<b>85.5</b>

**Chanzo:** Wizara wa Fedha na Mipango  
**Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hiyo Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

## 7 NOVEMBA, 2022

- i. Kuhakikisha kwamba sekta ya utalii inakuwa mojawapo ya sekta zinazopewa kipaumbele katika kupewa fedha za maendeleo katika bajeti ya mwaka 2023/24;
- ii. Kuiongezea fedha sekta ya utalii katika mgao unaofuata wa mkopo wa ECF katika mwaka wa fedha 2023/24;
- iii. Kuanzisha mkakati maalum wa kuvutia wawekezaji katika ujenzi wa hoteli za hadhi mbalimbali pamoja na kutoa vivutio mbalimbali ili kuvutia wawekezaji katika sekta ya utalii katika fukwe zetu;
- iv. Kufungua kanda nyingine za utalii hasa ukanda wa nyanda za juu kusini (*Southern circuit*);
- v. Kuangalia upya uamuzi wa Serikali wa kuanza kutoza kodi ya ongezeko la Thamani (VAT) kwenye Ndege za Kukodi (*Charter air craft*) ili kuchochea utalii;
- vi. Kuendelea kutenga Bajeti kwa ajili ya kutangaza utalii kama ilivyofanyika kwa *Royal Tour*; na
- vii. Kuondoa migogoro kati ya wananchi na hifadhi, Mpori Tengefu, Mbuga za Wanyama, na Ushoroba ili tutunze maliasili zetu.

### 2.5. Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Juni 2022, Deni la Serikali lilifika **Shilingi trilioni 71.56** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 64.50** katika kipindi kama hicho mwaka 2021 sawa na ongezeko la **Shilingi trilioni 7.06** ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 10.95**. Sababu za ongezeko hilo ni kutokana na kupokelewa mikopo mipya kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kutolewa kwa hatifungani maalumu ya **Shilingi trilioni 2.18** kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma

(PSSSF) linalohusu michango ya watumishi waliokuwa kwenye utumishi kabla ya mwaka 1999.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Deni la Serikali ni himilivu kwa viwango vyote vya kimataifa, Kamati inaishauri Serikali kwamba mikopo ielekezwe kwenye miradi ya maendeleo itakayochochea uzalishaji na mauzo nje ya nchi ili kuongeza mapato ya kigeni yatakayosaidia kulipa mikopo hiyo. Aidha, miradi yote inayochukua muda mrefu kukamilika na ina faida itumie mikopo ya masharti nafuu na sio yenye masharti ya kibiashara ambayo kipindi cha kutoanza kulipa mtaji (Grace Period) ni kifupi na riba ni kubwa. Aidha, imekuwa ni rai ya Kamati ya muda mrefu kuweka na kutumia kiashiria cha ukomo wa ulipaji wa deni la Serikali kwa mapato ya ndani yaani *Debt Service to Domestic revenue ratio* ili kuhakikisha kwamba mapato ya ndani yanauwezo wa kugharamia shughuli zote za Serikali pamoja na Deni la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba kiashiria hiki kinatambulika kimataifa isipokuwa hakijawekewa ukomo katika muundo unaotumika kupima na kutathmini uhimilivu wa deni kutokana na utofauti wa sifa za masoko ya fedha ya ndani kwa nchi zinazotumia muundo huo hususan nchi zinazoendelea (Low Income Countries). Aidha, Serikali imetambua umuhimu wa kiashiria hicho na imeanza kuchukua hatua za awali za kufanyia utafiti na kisha uchambuzi na tathmini ikishirikiana na taasisi za kimataifa za Benki ya Dunia na Macroeconomic and Financial Management Institute of Eastern and Southern Africa - MEFMI ili kuhakikisha kwamba, matokeo ya kiashiria cha ukomo huo yanakubalika kimataifa. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii muhimu na nimatumaini yake kuwa itaweza kukamilika kwa wakati.

## 2.6. Mwenendo wa Mikopo ya Sekta Binafsi

**Mheshimiwa Spika**, Mikopo kwa Sekta Binafsi ilikua kutoka **Shilingi trilioni 20.6** mwishoni mwa mwaka 2020/21 hadi kufikia **Shilingi trilioni 24.59** mwezi Juni 2022, ikiwa ni ukuaji wa wastani wa **asilimia 19.4**, ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 3.6** mwaka 2021. Hata hivyo, Kamati imechambua na kubaini kwamba mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli binafsi ni **asilimia 38.3**, mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli za kibiashara ni **asilimia 16.0**, na mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli za viwanda ni **asilimia 10.7**. Aidha, viwango vya riba vinavyotozwa kwenye mikopo vimepungua kutoka **asilimia 16.6** hadi **asilimia 16.41** sawa na kupungua kwa **asilimia 0.19** tu. Viwango hivi vya riba haviwezi kuchochea ukopaji kwa ajili ya uwekezaji wenye tija badala yake mikopo mingi itaelekezwa kwenye shughuli binafsi. Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

- i. Benki kuu ya Tanzania ibadili mkopo wa **Shilingi trilioni 1** kuwa dirisha maalumu (special credit window) ili kutoa mikopo kwa mabanki kwa sharti la kuwakopesha wakulima kwa riba ya **asilimia 3 mpaka 10**. Hadi tarehe 30 Oktoba, 2022 zilikuwa zimetumika **Shilingi bilioni 95** tu; na
- ii. Serikali iendeele kuziongezea mtaji benki za TADB na TIB ili ziweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyo kusudiwa.



### 3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 NA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2022/23

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2022/23. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali ilipanga kutumia **Shilingi trilioni 15.26** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Serikali ilitumia jumla ya **Shilingi trilioni 14.65** sawa na **asilimia 96.0**. Utekelezaji huu unaonyesha wazi nia na dhamira ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuwakwamua watanzania kutoka katika wimbi la umasikini. Aidha, Katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 15.01**, hadi kufikia robo ya kwanza ya mwaka 2022/23 Serikali imetumia jumla ya **Shilingi trilioni 3.2** sawa na **asilimia 21.32** hivyo ni wazi kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Serikali inaweza kuwa imetoa fedha za maendeleo kati ya **asilimia 85 hadi 90** tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa miradi ya maendeleo ya kimkakati na iliyopewa kipaumbele na inaushauri ufuatao;-

#### 3.1. Sekta ya Usafiri na Usafirishaji

##### 3.1.1. Reli ya Kisasa ya SGR na Reli ya TAZARA

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wake, hivyo kufanikisha kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa kipande cha Tabora - Isaka (km 165) ambapo maandalizi ya ujenzi yanaendelea; kuendelea na ununuzi wa mkandarasi kwa vipande vya

## 7 NOVEMBA, 2022

Tabora – Kigoma (km 411) na Kaliua – Mpanda – Karema (km 321). Pamoja na mafanikio hayo Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuharakisha utafutaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Kaliua – Mpanda – Karema (km 321), Uvinza – Musongati – Gitega (km 282), Keza – Ruvubu (km 36) na Isaka – Rusumo (km 371)

ii. Taasisi za Serikali kuharakisha kuhamisha miundombinu yao ili kupisha ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR;

iii. Kulipa hati za madai ya mkandarasi kwa wakati ili kuepusha ongezeko la gharama za mradi kutokana na riba;

iv. Serikali kuhakikisha kwamba Mkandarasi Mkuu wa reli ya kisasa (Yapi Merkezi) analipa madeni yote ya sub-contractors ambayo yanakadiriwa kufikia kiasi cha **Shilingi bilioni 12;**

v. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya DRC Congo iangalie uwezekano wa kufikisha reli ya kisasa SGR katika bandari ya Kasanga iliyoko wilaya ya Kalambo Mkoa wa Rukwa ili iunganishwe na Ferry kubwa kati ya Bandari ya Kasanga na Bandari ya Mulilo iliyoko upande wa DRC Congo, hatua hii itaiwezesha reli yetu kuhudumia soko la nchi hiyo;

vi. Kuharakisha mapitio ya Sheria ya TAZARA ili kutoa fursa kwa Tanzania kuwekeza kwenye Reli hiyo kwa upande wa Tanzania ili iwe na manufaa kwa upande wa Tanzania. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuingia ubia na makampuni makubwa ya uendeshaji wa njia za reli ili kupata vichwa na mabehewa kwa ajili ya reli ya TAZARA; na

vii. Serikali kupitia Wakala wa barabara vijijini (TARURA) itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara zinazounganisha vituo vya SGR na makazi ya watu, mfano (Stesheni ya Kongowe);

### 3.1.2. Uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua umuhimu na mchango wa shirika la ndege la Tanzania (ATCL) kwa lengo la kuchochea uchumi katika Sekta mbalimbali kama vile utalii, usafiri na usafirishaji wa mizigo. Hata hivyo, shirika hilo bado linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwepo wa Madeni ya muda mrefu na yasiyolipika. Kutokana na changamoto hizo Kamati inaushauri ufuatao:-

- i. Serikali iendelee kutoa kipaumbele katika safari za ndege za kibiashara kwa ndege za ATCL. Sambamba na hilo, Serikali kupitia Kampuni ya Ndege (ATCL) ijijenge na kuwa na mifumo imara ya biashara ili iweze kujiunga na mifumo ya kimataifa ya biashara ya ndege kama vile “*airline global alliance*”. Vilevile, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha safari katika nchi zenye makampuni/mashirika ya ndege yanayofanya safari nchini;
- ii. Serikali irekebishe mikataba ya ukodishaji ndege baina ya Kampuni ya Ndege (ATCL) na Wakala wa Ndege (TGFA). Kwa mfano, mikataba ya ukodishaji ndege haikuwa na kipengele cha msamaha wa matukio ya majanga (Force Majeure) hivyo, TGFA iliendelea kuitoza fedha za ukodishaji ndege za ATCL hata wakati wa janga la UVIKO-19 ambapo ndege zilikuwa hazifanyi kazi. Kamati inaamini kwamba kurekebisha mikataba hii kutaboresha utendaji kazi wa ATCL;
- iii. Kuboresha viwanja vya ndege kwa kuviwekea taa ili kuongeza safari za ndege za ATCL kuliko hivi sasa ambavyo ndege zinaruka muda wa mchana tu na kutoruka wakati wa usiku;

- iv. Kuongeza safari za ndege kwenye maeneo/mataifa ambayo Tanzania inapokea watalii wengi;
- v. Serikali kuboresha Jengo la Abiria katika kiwanja cha ndege cha Mwanza ambalo kwa muda mrefu limekuwa katika hatua za usanifu. Kiwanja hiki kina fursa ya kuwa transit route ya ndege za Rwanda, Burundi na DRC Congo; na
- vi. Serikali ifanye marekebisho (restructuring) ya deni la ATCL ili liwe sehemu ya mtaji, hii itatoa nafasi kwa ATCL kuaminika na Taasisi nyingine kibiashara.

### **3.1.3. Sekta ya Nishati**

#### **3.1.3.1.Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115)**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba taarifa ya mpango iliyowasilishwa na Serikali, haijaonyesha ni lini mradi huu unatarajiwa kukamilika, japokuwa taarifa ya shirika la umeme Tanzania (TANESCO) inaonyesha kwamba mkandarasi wa mradi huu ameongezewa muda wa miezi 12 kukamilisha mradi huu toka tarehe 14 Juni, 2022 iliyopangwa katika mkataba hadi tarehe 15 Juni 2023. Sambamba na hilo, Kamati ilibaini masuala ya msingi yafuatayo:-

- i. Sababu za Mkandarasi kuomba kuongezewa hazikuwa za msingi na bado Serikali imekubali kumuongezea muda wa utekelezaji;
- ii. Mpango kazi (Work Plan) uliowasilishwa na mkandarasi Serikalini unaonyesha kwamba mradi huu utakamilika Julai, 2024; kinyume na muda wa miezi 12 kukamilisha mradi huu (hadi 15 Juni, 2023) ambao Serikali imemuongezea mkandarasi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na masuala yaliyobainika katika Mradi huu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Kamati inashauri Serikali masuala yafuatayo;-

- i. Kwa kuwa, Mkandarasi aliomba kuwepo na bodi ya maamuzi ya Rufani (Disputes Adjustment Board-DAB) ili kutoa uamuzi wa rufaa za Mkandarasi ni vyema gharama za bodi hiyo zikatolewa na Mkandarasi badala ya Serikali kwa sababu suala la DAB halikuwa sehemu ya mkataba na kwa kuwa changamoto zilizojitokeza zimesababishwa na Mkandarasi na si Serikali;
- ii. Kwa kuwa, moja ya changamoto iliyosababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi huu kwa wakati ni Mkandarasi kukiuka baadhi ya masharti ya mkataba ikiwemo mkandarasi kuchelewa kuleta wataalamu wanaohitajika kimkataba, mkandarasi kujenga chini ya kiwango kwa baadhi ya maeneo ya bwawa, kwa mfano, handaki la kuchepusha maji (*Diversion chanel*) la mto Rufiji lilijengwa kwa methodolojia hafifu na hivyo kusababisha maji kuingia katika handaki kabla ya ujenzi wake kukamilika. Hivyo basi ni vyema Serikali ikatanzua changamoto hii bila kuleta hasara kwa nchi;
- iii. Serikali iweke mikakati ya kulinda vyanzo vya maji vinavyozunguka mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ili kuwezesha uwepo wa maji ya kutosha pindi mradi utakapokamilika hasa ukizingatia mabadiliko ya tabianchi;
- iv. Serikali ifanye ukaguzi wa kina (special audit) kwenye mradi huu ili kuhakikisha fedha zilizotumika zinaendana na matakwa ya mradi;
- v. Endapo mkandarasi atakiuka masharti ya mkataba hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi yake; na
- vi. Serikali ihakikishe fedha za michango ya hisani za jamii (CSR) kiasi cha **Shilingi bilioni 262** zitumike kwenye miradi iliyopangwa sambamba na miradi mingine katika

maeneo ambayo mradi unatekelezwa Mkoa wa Pwani na Morogoro na si vinginevyo.

### **3.1.3.2.Mradi wa Usambazaji na matumizi ya Gesi Asilia**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa mipango yake ya kuanza kujenga vituo vya *Compressed Natural Gas* vitavyochochea usambazaji na matumizi ya gesi asilia. Pamoja na hatua iliyofikiwa ya kusambaza gesi majumbani ni muhimu magari yote ya umma ambayo yapo katika jiji la Dar es salaam na mikoa ya jirani kama Pwani, Lindi, Tanga na Mtwara yakaanza kutumia gesi asilia iliyogandamizwa CNG badala ya mafuta. Aidha, Serikali iendelee kuhamasisha makampuni ya usafirishaji yaliyopo nchini yaanze kutumia nishati hiyo. Hatua hii inaweza kupunguza matumizi ya mafuta nchini ambayo kwa makadirio tunatumia lita 6,120,785 za dizeli kwa siku. Vilevile, hatua hii italinda akiba yetu ya fedha za kigeni zinazotumika katika kuagiza mafuta kwenye soko la dunia. Faida nyingine zinazoweza kupatikana ni pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji viwandani na kujilinda na athari za kupanda kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia.

### **3.1.3.3.Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kutekeleza mradi huu kwanza kwa kutoa kiasi cha Dola za Marekani **milioni 111.27** kama sehemu ya awali ya hisa za Serikali kwenye kampuni inayotekeleza mradi huu. Pili kwa kutatua changamoto ya pingamizi la utekelezaji wa Mradi kutoka kwa Wanaharakati wa Mazingira na Haki za Binadamu ambapo mpaka sasa Maamuzi ya Mwisho ya Uwekezaji

(*Final Investment Decision-FID*) yamekwisha fanyika. Hata hivyo, Kamati inatoa ushauri ufuatao kwa Serikali;-

- i. Kwa kuwa, mradi huu unapita katika mikoa 8, wilaya 24 na kata 134, ni vyema mchango wa hisani kwa jamii (Corporate Social Responsibility-CSR) kwa mradi huu utumike katika maeneo ambayo yanapitiwa na mradi ili kuleta manufaa katika maeneo husika na kuimarisha ulinzi; na
- ii. Serikali iharakishe kuwalipa fidia wananchi 6,131 ifikapo mwezi Desemba 2022 kama ilivyopangwa ili mradi uanze kutekelezwa kwa wakati.

#### **3.1.3.4. Uunganishwaji wa umeme vijijini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba vijiji 8,804 kati ya vijiji 12,345 vimeunganishwa na umeme Tanzania Bara sawa na **asilimia 71.32**. Jumla ya **Shilingi bilioni 313.40** zimetumika katika mwaka 2021/22 na **Shilingi bilioni 84.90** katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa iliyotolewa na Serikali ni taarifa ya kijumla (Cummulative) na hivyo ni vigumu kupima ufanisi wa kasi ya uunganishaji wa umeme vijijini. Mfano, miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kwa mwaka huu imekumbwa na changamoto mbalimbali kama vile, kusitishwa kwa mikataba na upandaji wa bei za vifaa vya umeme hivyo ni vigumu kujua ni kiasi gani imetekelezwa kwa kulinganisha na lengo. Kamati inashauri Taarifa ya Miradi hii iwe inawasilishwa kwa kulinganisha lengo la mwaka husika na vijiji vilivyounganishwa na sio kutoa taarifa ya vijiji vyote vilivyounganishwa tangu mradi ulipoanza hatua hii italetu uwazi na uwajibikaji. Aidha, ni vyema Serikali ikafanya

tathmini ya vijiji na vitongoji halisi vilivyofikiwa na umeme wa REA hadi sasa.

### **3.1.4. Sekta ya Miundombinu**

#### **3.1.4.1. Miradi ya Bandari**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia tathmini ya utekelezaji wa miradi ya bandari ya Dar es Salaam, Mtwara na Tanga na ina maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

##### **a) Bandari ya Tanga**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini Bandari ya Tanga haihudumii meli na shehena ya kutosha kutokana na umbali wa Km 1.7 toka gatini hadi meli zinapotia nanga na hivyo kuwa na kasi ndogo ya kupakia na kushusha shehena ya mizigo ya meli ambazo zilipaswa kuhudumiwa nangani . Kamati inaishauri Serikali kufanya maboresho ya Bandari kwenye miundombinu, mitambo na vifaa ili kuvutia meli na shehena nyingi. Aidha, Serikali iweke mkakati wa kimasoko mahsusi kwa ajili ya Bandari ya Tanga ambao lengo lake ni kuteka soko la Kaskazini mwa Tanzania na nchi jirani za Rwanda, Burundi na Uganda.

##### **b) Bandari ya Mtwara**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba kuna uhaba wa makasha katika Bandari ya Mtwara hivyo meli nyingi zinaepuka gharama za kwenda Bandari ya Mtwara bila kuwa na shehena inayoenda kushushwa katika bandari hiyo ili zibebe zao la korosho. Hii ndiyo sababu ya msingi ambayo inasababisha bandari hiyo isitumike kwa



ajili ya kusafirisha zao la korosho. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari (TPA) kuhakikisha kwamba inatatua changamoto ya upatikanaji wa makasha ili kuifanya bandari ya Mtwara kutumika ipasavyo. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuweka miundombinu ya kujazia mafuta melini (bankery facility) katika bandari ya Mtwara ili bandari hiyo itumike kujaza mafuta hasa kuelekea ujenzi wa mradi wa LNG ambapo huduma hiyo itahitajika. Ikizingatiwa ni bandari pekee katika ukanda huo inayoweza kutoa huduma hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba, Serikali itafute ufumbuzi wa changamoto ya mlundikano na msongamano wa malori katika eneo la Malawi cargo na mlundikano wa magari katika gati la magari (RoRo). Vilevile, Kamati inaishauri Serikali isimamie kanuni za EWURA zinazoelekeza kwamba mafuta yachukuliwe katika bandari iliyopo katika kanda ili kuchochea matumizi ya Bandari za kanda husika. Kamati inashauri Mikoa ya kaskazini itumie bandari ya Tanga na Mikoa ya kusini itumie bandari ya Mtwara.

### **c) Bandari ya Bagamaoyo**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika bandari ya Dar es salaam ili ijiendeshe kwa ufanisi. Hata hivyo, bandari hiyo haina eneo la kuendelea na upanuzi kutokana na mahitaji kulingana na eneo ilipo. Aidha, mradi wa SGR unaeendelea ni lazima kuwe na Bandari kubwa ya kisasa ambayo italeti mzigo wa kutosha ili reli hiyo iwe na manufaa. Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia nzuri ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Bagamaoyo ambayo itazingatia manufaa mapana ya taifa kwa vizazi vya sasa na vijavyo ili kutekeleza mradi huo.

### 3.1.5. Mifumo ya TEHAMA

#### 3.1.5.1.Mifumo ya Kutunza kumbukumbu za Watumishi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyoanza kuchukua kwenye kuhuisha na kuunganisha mifumo mbalimbali ya TEHAMA, ukiwemo, mfumo wa kielektroniki wa Taarifa za watumishi na malipo ya mishahara (HCMIS). Kamati imebaini kwamba bado kuna changamoto katika utunzaji wa nyaraka za watumishi wa umma kidijitali. Mfano, mtumishi anaajiriwa na Serikali mafao yake yanakatwa na Serikali kwa niaba yake lakini anapofika umri wa kustaafu anatakiwa kuwasilisha nyaraka hizo kwa Serikali iliyomuajiri. Kamati inashauri kwamba katika mwaka ujao wa fedha Serikali ianzishe na kuendeleza utunzaji wa kumbukumbu za watumishi kidijitali.

#### 3.1.5.2.Mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

##### a) Mifumo ya Mamlaka ya Mapato na Mamlaka ya Bandari

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mapato ya Serikali yamekuwa yakipotea kutokana na kukosa ufanisi kwenye ukusanyaji, uwepo wa mifumo dhaifu pamoja na kutosomana kwa mifumo hiyo. Hivyo, Kamati inaendelea kuisitiza kwamba, mifumo ya ukusanyaji ya mapato ya Mamlaka ya Mapato TRA ambayo ni (IDRAS, TANCIS) na TPA iboreshwe na kuunganishwa ili iweze kukusanya mapato kwa ufanisi na Serikali kupata mapato stahiki. Aidha, Serikali iendeleo kuunganisha mfumo wa GePG katika taasisi zote za Umma ili utumike kikamilifu katika kukusanya mapato.

**b) Mifumo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

**Mheshmiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba mapato mengi ya Halmashauri hasa yale yanayokusanywa nje ya mfumo hupotea bila kuingizwa kwenye akaunti za Serikali. Aidha, kamati imebaini kwamba kutokusomana kwa mifumo ya mapato ya Serikali za Mitaa na Serikali kunaongeza tatizo la kupotea kwa mapato ya Serikali. Hivyo Kamati inashauri kuweka katazo la kutokusanya fedha yoyote ya umma bila kutumia mfumo na kuhakikisha mashine zote za kukusanyia mapato ya Serikali za Mitaa (POS-Point of Sales) zinatumika kama ilivyokusudiwa.

**3.1.6. Tanzania ya Kidijitali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa jitihada zake za kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na baadhi ya maeneo ya mjini yasiyo na mvuto kibiashara, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF). Licha ya jitihada hizo Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya maeneo itakuwa ngumu kufikiwa na mtandao wa mawasiliano kupitia mfuko wa UCSAF kutokana na kutokuwa na mvuto wa kibiashara (*economically feasible*). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka vivutio maalum vya kikodi kwa ujenzi wa minara na uendeshaji kwa maeneo hayo ili minara iweze kujengwa. Tofauti na ilivyo hivi sasa zabuni zilizotangazwa kupeleka huduma katika maeneo hayo hazipati makampuni yanayovutiwa kujenga minara katika maeneo hayo.

### 3.1.7. Ujenzi wa Barabara na Madaraja makubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa taarifa ya Serikali **kuhusu** utekelezaji wa miradi mbalimbali ya barabara na madaraja nchini na ina ushauri ufuatao:

(v) Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukarabati barabara zote zinazounganisha Mikoa ambazo hazijafanyiwa matengenezo muda mrefu. Aidha, Serikali kuendelea kutoa fedha kwa wakati ili barabara zetu ziweze kukamilika kama ilivyopangwa;

(vi) Ni vyema Serikali ikachagua barabara chache kwa kila mwaka wa fedha ili zitekelezwe kwa Bajeti iliyopangwa katika mwaka husika, kuliko kuwa na miradi mingi ya barabara ambayo inazalisha madai kutokana na kuchelewa kulipwa (*arrears*). Kwa msingi huo Kamati inashauri kwamba barabara zitakazo tekelezwa ziwe ni zile ambazo ni za Kimkakati;

(vii) Serikali kuangalia uwezekano wa kuwa na mikataba ya ujenzi wa barabara ambayo haitoi fursa ya kulipa riba kubwa pindi malipo yanapochelewa; na

(viii) Kupunguza kiasi kikubwa cha matumizi ya fedha kwenye ubunifu (*design*) na ubunifu wa kina (*detailed design*) kwa miradi ambayo haitekelezwi hivi karibuni.

### 3.1.8. Miradi ya Muda mrefu ya Ujenzi wa Nyumba za Viongozi pamoja na Hospital

**Mheshimiwa Spika**, Moja ya changamoto iliyopo nchini ni uwepo wa miradi ya ujenzi wa Nyumba za Wakuu wa Mikoa, Wilaya pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa. Miradi hii imekuwa haikamiliki kwa takribani miaka 5 hadi 6. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha kwanza miradi inayoendelea kabla ya kuanzisha miradi mipya ya

ujenzi wa nyumba za viongozi na kukarabati zilizopo ili ziendelee kutumika kuliko kuanzisha ujenzi mpya. Aidha, kwa upande wa miradi ya Hospitali ni vyema kukamilisha zilizopo kwanza pamoja na kuweka vifaa tiba vyote muhimu ili zianze kutoa huduma kikamilifu.

### **3.1.9. Vitambulisho vya Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kuanzia mwaka 2012 hadi mwezi Septemba, 2022 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilikuwa imesajili na kutoa Namba kwa Watu 19,509, 202, kati ya hao waliokuwa wamepewa vitambulisho katika kipindi chote hicho cha Miaka 10 ni Watu 11,117,264 sawa na **asilimia 56** ya lengo. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba zoezi la uandikishaji na utoaji wa vitambulisho vya Taifa limekuwa likitekelezwa kwa kasi ndogo kutokana na changamoto zifuatazo:-

- (i) Uwepo wa deni la Mkarandarasi lenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 7.58** sawa na **Shilingi bilioni 17** ambalo limelipwa na Serikali mwezi Oktoba 2022;
- (ii) Kuchelewa kwa upatikanaji wa Kadighafi za Vitambulisho vya Taifa milioni 13 kutokana na uhaba wa fedha na smartcard chips katika soko la dunia;
- (iii) Kuchelewa kupatikana kwa fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 42.5** kwa ajili ya ununuzi wa kadighafi 11,775,728; na
- (iv) Upungufu wa Vitendea kazi pamoja na Rasilimali watu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaushauri ufuatao kwa Serikali:-

- (i) kuhakikisha kwamba kiasi cha **Shilingi bilioni 42.5** zinapatikana kwa mkupuo mmoja au miwili ili

utengenezaji na ugawaji wa vitambulisho ufanyike kwa kasi;

- (ii) Kufungamanisha Taarifa baina ya Taasisi za Serikali mfano endapo mwananchi ataenda kuchukua Hati ya Kusafiria Taarifa zake za awali zichukuliwe NIDA na sio mwananchi huyo kuwasilisha Taarifa zile zile alizoziwasilisha NIDA;
- (iii) Kuangalia uwezekano wa kuanza kuchukua Taarifa hata kwa watoto chini ya Miaka 18 ili jinsi anavyokua ziwe zinahuishwa kuliko kusubiria hadi afike miaka 18; na
- (iv) Kutumia Ofisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa kugawa Vitambulisho ambavyo bado havijachukuliwa na Wananchi ambavyo viko Takribani 785,222.

### **3.1.10. Kupitia upya na kuangalia muundo wa Majukumu ya Taasisi za TEMDO, TIRDO na CARMATEC**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Taasisi hizi ziko chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na zinafanya majukumu yanayoshabihiana, licha ya kuanzishwa kwa sheria tofauti. Kamati inashauri Serikali kufanya tathmini ya kina kwa Taasisi hizi ili kubaini kama bado kuna umuhimu wa kuendelea na Muundo uliopo hivi sasa au kuziunganisha ili ziwe na tija. Aidha, Serikali iendelee kutenga bajeti ya kutosha kwa taasisi hizi ili ziendelee kutekeleza shughuli zote zilizokusudiwa.

### **3.1.11. Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Kilimo ni muhimili wa maendeleo ya uchumi ikichangia **asilimia 26.1** mwaka 2021 kwenye Pato la Taifa na kutoa fursa za ajira zaidi ya **asilimia 65** na hivyo kuifanya ndio sekta pekee

inayotegemewa na wanachi wa kipato cha chini. Vilevile, kilimo kina uhusiano na sekta nyingine katika kutoa malighafi kwa viwanda na soko kwa bidhaa zilizotengenezwa. Kilimo kinachukua sehemu muhimu katika kukua kwa uchumi na kupunguza umaskini. Hata hivyo, pamoja na manufaa mapana ya sekta hii bado haijaweza kukua kwa kile kiwango kinachostahili ambapo sekta hii imekua kwa **asilimia 3.9** mwaka 2021. Hii imetokana na sababau mbalimbali zikiwemo pembejeo zisizotosheleza kama vile mbegu bora, mbolea na dawa za kilimo, mfumo wa kizamani wa uoteshaji mazao na ucheleweshaji wa maendeleo ya miundombinu kama vile, skimu za umwagiliaji, miundombinu ya masoko, barabara za mashambani na usindikaji wa mazao.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya sekta hii imepanda takribani mara tatu na kufikia **Shilingi bilioni 954** mwaka 2022/23 kutoka **Shilingi bilioni 294** mwaka 2021/22. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua hii katika kuiinua sekta hii muhimu ya kilimo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza Matumizi ya Teknolojia bora katika uzalishaji wa mazao ili kuongeza mapato ya kigeni pamoja na upatikanaji wa malighafi za uzalishaji viwandani. Aidha, Serikali kupitia mifumo yake iendelee kutekeleza yafuatayo:-

### **3.1.11.1. Kuimarisha vituo vya utafiti wa mbegu bora:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba katika kipindi cha miaka kumi Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imegundua aina 146 za mbegu bora za mazao mbalimbali kupitia vituo vyake vya utafiti. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/23 sekta ya utafiti wa mbegu imetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 40.73**. Vilevile, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa miradi ya

uzalishaji wa mbegu chini ya mkopo wa ECF imekuwa ya kusuasua. Hivyo, Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

- (iii) Ili mbegu zilizogunduliwa na TARI zipatikane kwa wingi na ziwafikie wakulima ni lazima kuwe na ushirikiano kati ya TARI na Wakala wa Taifa wa Mbegu (ASA);na
- (iv) Serikali iendeele kuwekeza zaidi kwenye kituo cha TARI ili kiwe na uwezo wa kufanya utafiti na kuzalisha mbegu bora zinazoweza kuhimili mabadiliko ya tabia nchi.

### **3.1.11.2. Kuimarisha Huduma za Ugani:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba kati ya maafisa ugani 20,538 wanaohitajika waliopo ni 6704 sawa na **asilimia 30** ya mahitaji. Vilevile, Kamati imetaarifiwa kwamba kuna mfumo uitwao M-Kilimo unaotumika kuwafikia wakulima kutoa huduma za ugani ili kuziba pengo la mahitaji ya maafisa ugani wanaohitajika. Aidha, Kamati imebaini kwamba pikipiki 7,000 zilizogawiwa na Serikali hazitumiki kama ilivyokusudiwa kutokana na kukosekana kwa mafuta ya kuendesha pikipiki hizo. Kamati inashauri masuala yafuatayo:-

- (i) Kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zitenge fedha kutoka kwenye mapato ya ndani (own source) kwa ajili ya maafisa ugani;
- (ii) Pamoja na Serikali kununua vifaa vya kupimia afya ya udongo, bado huduma hiyo haijaanza kutolewa kutokana na kukosekana kwa vifaa vingine vinavyoweza kupima afya ya udongo; na
- (iii) Kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima namna ya kutumia mfumo wa M-Kilimo.



### **3.1.11.3. Upatikanaji wa Mbolea:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jitihada za Serikali za kuhakikisha upatikanaji wa mbolea kwa ruzuku ambapo hadi hivi sasa zimetolewa tani 46,000 za mbolea aina mbalimbali kupitia makampuni na mawakala walioajiriwa. Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kwamba makosa yaliyotendeka katika mfumo wa vocha za pembejeo hayajirudii kwenye ruzuku ya mbolea inayotolewa;

(ii) Serikali kuwawezesha wawekezaji wa ndani kimtaji ili waweze kutumia malighafi zinazopatikana nchini kuzalisha mbolea ya kutosha;

(iii) Kuendelea kuwekeza kwenye kiwanda cha Viuadudu Kibaha ili kiweze kuzalisha mbolea pamoja na viuatilifu, hadi hivi sasa Serikali imewekeza kiasi cha **Shilingi bilioni 83** na bado hiajaweza kupata manufaa yaliyotarajiwa.

### **3.1.11.4. Mitaji kwa ajili ya uendelezaji sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwekeza katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo TADB kwa kuweka mtaji wa kianzio kiasi cha **Shilingi bilioni 60** na hivi sasa imeshawekeza jumla ya **Shilingi bilioni 268** Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza mtaji katika Benki hii ili kuchochea uwekezaji na maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Ni vigumu kutegemea benki za biashara kukopesha sekta ya kilimo kwa sababu sekta hiyo ina vihatarishi vikubwa.

**7 NOVEMBA, 2022**

**Mheshimiwa Spika**, kupitia tangazo la Gavana wa Benki Kuu la tarehe 27 Julai, 2021 lililokuwa na kichwa cha habari *“policy measures to promote credit to private sector and lower interest rates”*. Tangazo hilo lilikuwa na lengo la kutumia nyenzo mbalimbali za benki kuu katika kusimamia sera ya fedha ili kuongeza ukwasi katika mablenki na mikopo kwa sekta binafsi katika kipindi cha janga la **UVIKO -19**. Aidha, Serikali ilianzisha mkopo maalum kwa mablenki wenye thamani ya **Shilingi trilioni 1** ili sekta ya kilimo ikopeshwe kwa **asilimia kati ya 3 hadi 10** ***“Introduction of a special Loan amounting to TZS 1.0 Trilioni to Bank and other financial instituion for on lending private sector”***. Pamoja na kwamba mazingira ya uchumi yamebadilika mahitaji ya mkopo huu bado hayajabadilika. Kamati inaishauri Serikali kupitia upya masharti ya mkopo huo ili yaendane na mazingira ya sasa, hatua hii itasababisha upatikanaji wa mikopo ya kilimo kwa riba nafuu.

### **3.1.11.5. Masoko ya Mazao ya Biashara**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuwezesha upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi. Aidha, Serikali ihakikishe miundombinu ya maghala yanayomilikiwa na Serikali katika mataifa ya DRC Congo na Sudani Kusini iunganishwe na wafanyabisahara wa ndani ili itumike kikamilifu sio kwa Taasisi za Serikali za (NFRA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania (CPB) tu.

**Mheshimiwa Spika**, Bei ya Korosho katika Soko la Dunia imeshuka, hii ni kutokana na ukweli kwamba mazao ya Kilimo ambayo hayajaongezwa thamani yana asili ya kuathiriwa na mabadiliko ya bei. Endapo kuna

mabadiliko madogo kwenye bei athari yake katika mahitaji ni kubwa (Elastic).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri masuala yafuatayo kuhusu masoko ya mazao ya biashara na chakula:

- i. Kuwepo na Mkakati wa kuongeza thamani ya mazao ya biashara na chakula ili yauzwe kwa bei ya soko;
- ii. Kuharakisha mchakato wa kuanzisha mfuko wa maendeleo ya kilimo ambao utatumika kuwezesha uhimilivu wa bei za mazao “Agricultural development Fund”
- iii. Mazao yote ya biashara na yale ambayo yapo chini ya Bodi mbalimbali yaingizwe kwenye mfumo wa soko la mazao (Tanzania Mercantile Exchange – TMX). Kwa sababu mazao yaliyopo kwenye soko la TMX yamefanikiwa kuuzwa kwa bei ya juu kuliko bei ya chini ambayo wakulima walikuwa tayari kuuza;
- iv. Serikali iendelee kuimarisha soko la TMX ili liweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa;
- v. Serikali iangalie uwezekano wa kuhamisha soko la TMX kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Kilimo ili liendeshe kwa tija katika kutafuta masoko ya mazao ya kilimo; na
- vi. Serikali iangalie upya mgawanyo wa majukumu ya kutafuta masoko kwa mazao ya kilimo baina ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

#### **3.1.11.6. Kilimo cha Pamba**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba pamba inayolimwa nchini **asilimia 70** inasafirishwa kwenda nje ya nchi na **asilimia 30** inabaki ndani ya nchi kwa matumizi ya viwanda vya nguo vya ndani ambayo haitoshelezi mahitaji. Na kwakuwa viwanda vingi vya nguo huagiza

pamba kutoka nje ya nchi wakati wa mavuno. Hivyo Kamati inaushauri kwamba ni vyema Bodi ya Pamba ikasimamia mikataba ya mauzo ya mbele *forward sales agreement* baina ya wakulima wa pamba nchini na viwanda vya nguo vya ndani.

### **3.1.11.7. Mashamba Makubwa (Block Farming)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuanzisha mashamba makubwa ya umwagiliaji **block farming** katika maeneo mbalimbali kama vile Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino (ekari 11,453), Halmashauri ya wilaya ya Bahi (ekari 3,560) na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya (ekari 65,000). Kamati imebaini kwamba asilimia kubwa ya mashamba haya yapo katika maeneo ambayo hayana vyanzo vya uhakika vya maji kama vile mito au maziwa, hivyo ni vyema Serikali ikaweka mkakati wa kuweka mashamba ya namna hii katika maeneo ambayo yana vyanzo vya uhakika vya maji ili kufanya kilimo cha umwagiliaji kiwe chenye tija kuliko kutegemea mvua. Vilevile, Kamati inaitaka Serikali kufufua na kuendeleza mashamba saba (7) makubwa ya Maua na Mbogamboga yaliyoko katika Wilaya ya Arumeru Mkoa wa Arusha. Aidha, inashauriwa kwamba mashamba yote makubwa yapate huduma ya miundombinu ya msingi kama vile maji, umeme na barabara ili yaweze kufanya uzalishaji kwa gharama nafuu.

### **3.1.11.8. Kilimo cha umwagiliaji na ujenzi wa mabwawa:**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania inajumla ya hekta 29,000,000 za kilimo ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Aidha, hadi kufikia mwaka 2021/22 kiwango cha Ardhi ambayo iko chini ya umwagiliaji ni

hekta 800,000 sawa na **asilimia 2.75** hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kujenga miundombinu ya umwagiliaji pamoja na mabwawa kama vile Bwawa la Kidunda na Farkwa ili kuwa na kilimo cha uhakika na chenye tija kuliko kutegemea mvua pekee. Hatua hii itasaidia kuwa na kilimo cha uhakika hasa kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi ambayo Taifa inakumbana nayo.

### **3.1.12. Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba Serikali iliingia mkataba na umoja wa watoa huduma wa mawasiliano ili kujenga mkongo wa mawasiliano katika maeneo yaliyokuwa hayajafikiwa na mkongo wa Taifa mwaka 2011. Utaratibu wa kutumia mikataba ni tofauti na utaratibu wa kutumia ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP). Ni vyema Serikali iangalie uwezekano wa kutumia mfumo wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi (PPP) kwa kufanya hivyo utawezesha mkongo kujengwa haraka zaidi na utafika maeneo mengi nchini. Vilevile, Serikali iwezeshe Shirika la Simu (TTCL) kukopa fedha kwa ajili ya kusambaza mkongo nchi nzima.

### **3.1.13. Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato katika Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudi za Serikali za kuwajengea uwezo watumishi kwenye Halmashauri mbalimbali nchini jinsi ya kuandaa maandiko ya miradi inayokidhi vigezo. Aidha, Kamati inatambua kwamba Serikali imeandaa mkakati wa ugharamiaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri kupitia vyanzo mbadala. Hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali bado hazibadilishi sera ya mradi huu kupelekwa kwenye Halmashauri zenye

uwezo wa kifedha na si zile zenye hali mbaya kiuchumi. Kamati inaona kuna haja ya Serikali kuangalia sera ya miradi hii ambayo inaelekeza fedha hizi kwenye Halmashauri za Miji na Majiji na hivyo Halmashauri ambazo zina hali mbaya na zinahitaji usaidizi wa fedha ili kuongeza mapato hazipati fursa hii. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kufanya mgawanyo wa fedha za uwekezaji kati ya zile zenye hali mbaya na Majiji na Miji ili kuzisaidia zote ziweze kuongeza mapato na kujitegemea. Pendekezo hili lina lengo la kuondoa utofauti wa mapato baina ya Halmashauri mbalimbali. Mfano mzuri kwa nchi jirani ya Kenya wana Mfuko unaoitwa *Equalization Fund* wenye lengo la kuondoa Tofauti za kimaendeleo baina ya county. Aidha, Halmashauri zinazoimarika zitolewe katika mradi huu.

### **3.1.14. Utoaji wa Mikopo ya Serikali kwa wajasiliamali**

**Mheshimiwa Spika**, kuna changamoto kubwa ya usimamizi na uratibu wa mikopo inayotolewa na Wizara, Idara, Wakala na Taasisi za Serikali. Mfano LGA's inatoa mikopo ya **asilimia 10**, Mikopo kwa Wachimbaji wadogo wa madini inatolewa na Wizara ya Nishati na kuna mikopo inatolewa na SELF, TADB, NEEC, hizi ni baadhi ya Taasisi za Serikali zinazotoa mikopo. Kamati inaishauri Serikali kufanya kwanza tathmini ya ufanisi wa mikopo hiyo na kufanya uratibu na usimamizi wa pamoja wa namna ya utoaji wa Mikopo Serikalini. Aidha, uangaliwe uwezekano wa kuunganisha mikopo hii ili kuwepo na Taasisi moja ya Serikali itakayokuwa na jukumu la kutoa mikopo kwa sekta mbalimbali kwa wajasiliamali na wafanyabiashara wadogo.

### 3.1.15. Usimamizi wa Maafa Nchini

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kifungu cha 35 cha Sheria ya Bajeti sura ya 439 inaelekeza kuanzishwa kwa mfuko wa dharura (Contingency Fund). Aidha, kifungu cha 36 cha sheria hiyo kinabainisha vyanzo vya mfuko huo, ili kupata fedha za kugharamia mahitaji mbalimbali pindi maafa yanapotokea. Serikali imekuwa ikitenga bajeti ya dharura kupitia fungu 21 kinyume na matakwa ya sheria. Kamati inaishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa Dharura (Contingency Fund) kama sheria inavyotaka.

### 3.1.16. Ushiriki wa Sekta Binafsi

**Mheshimiwa Spika**, Katika mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 Serikali ilibainisha kwamba Sekta Binafsi katika mwaka 2023/24 inatakiwa kuchangia jumla ya **Shilingi trilioni 9.08**, kati ya Fedha hizo Sekta Binafsi ya ndani ilitarajiwa kuchangia **Shilingi trilioni 5.17** na ya Nje **Shilingi trilioni 3.91**. Pamoja na kwamba Serikali imebainisha kuwa Sekta binafsi imeshirikishwa katika mchakato wa Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa mwaka 2023/24 bado mchango wake hauonekani katika utekelezaji wa Mpango. Kamati inashauri Serikali ni vyema Mpango wa mwaka 2023/24 ukaainisha maeneo hayo ya ushirikishwaji wa Sekta Binafsi na inatarajiwa kuchangia kiasi gani. Aidha, hatua hii iende sanjari na kuongeza kasi katika kuboresha mazingira ya biashara kupitia Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhhibiti wa Biashara (Blueprint) ili kuvutia uwekezaji wengi zaidi.

**3.1.17. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)**

**Mheshimiwa Spika**, ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni namna pekee ya kupunguza mzigo kwa Serikali kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo yenye sura ya kibiashara. Matumizi ya njia hii yanatoa unafuu kwenye mapato ya Serikali ili Serikali ijielekeze kwenye maeneo ambayo hayana mvuto wa Kibiashara. Pamoja na uwepo wa Sheria ya Ubia Sura ya 103 na kufanya mabadiliko makubwa mwaka 2018 bado chanzo hiki cha kugharamia miradi ya maendeleo hakijaleta manufaa yaliyokusudiwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

- (i) Muamko mdogo wa Sekta ya Umma kutekeleza miradi kwa njia ya ubia;
- (ii) Maandalizi duni au kutokufanya maandalizi kabisa kwa miradi ambayo inaweza kutekelezwa kwa njia ya Ubia PPP;
- (iii) Uwezo mdogo wa Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi za Serikali kuandaa maandiko ya miradi inayotekelezwa kwa njia ya ubia;
- (iv) Kiwango kikubwa cha Mtaji wa chini (Minimum Capital) cha dola za Marekani **milioni 20** ambayo ni sawa na **Shilingi bilioni takribani 46.3** ili mradi utekelezwe kwa njia ya Ubia; na
- (v) Masharti magumu ya kutekeleza miradi inayobuniwa na Sekta Binafsi ili itekelezwe kwa njia ya ubia *“unsolicited bids”*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kwamba, katika mwaka ujao wa **fedha** kufanyia kazi changamoto zilizodainishwa hapo juu ili miradi ya ubia ianze kutekelezwa. Aidha, Kamati imebaini kwamba miradi



iliyotajwa katika mpango kutekelezwa kwa njia ya ubia ni ile ile na imekuwa haitekelezwi. Vilevile, Kamati inaitaka Serikali katika mwaka ujao wa fedha kutoa maelekezo kwa maafisa masuuli kubuni, kuandaa na kutekeleza miradi kwa mfumo wa PPP hasa yenye sura ya kibiashara.

### **3.1.18. Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi katika kipindi cha Mwaka 2021/22**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba miradi iliyofanyiwa Ufuatiliaji na Tathmini (U&T) kwa mwaka 2021/22 ilikuwa ni **253** tu ukilinganisha na Jumla ya Miradi **2,034** iliyoko katika kitabu cha Miradi ya Maendeleo (Development Book) cha Bajeti ya mwaka 2021/22, hii ni sawa na **asilimia 12** ya miradi yote iliyotekelezwa katika mwaka wa Fedha 2021/22. Aidha, Kamati imebaini changamoto zifuatazo kwenye suala la ufuatiliaji na tathmini wa Miradi ya Maendeleo:-

- i. Miradi mingi kutokamilika kwa wakati kutokana na udhaifu katika mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini (U&T) kama vile mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (JNHP-Julius Nyerere Hydro Electric Power) na mingineyo;
- ii. Hakuna Sheria wala Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini (U&T) na badala yake Serikali inatumia muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini (U&T);
- iii. Gharama za ujenzi na ukamilishaji wa miradi zinaongezeka kutokana na udhaifu katika Ufuatiliaji na Tathmini (U&T); na
- iv. Mafungu mengi ya Serikali hayatengi fedha kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini. (U&T).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali ili kuondokana na changamoto hizi ni vyema kuhakikisha

katika mwaka wa fedha ujao inakamilisha Sera na Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini (U&T).

#### **4.0. MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2023/24**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/24 ni wa tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 ambao ni wa mwisho katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ndio msingi wa maandalizi wa Dira Mpya ya 2050. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa tathmini ya Dira ya 2025 bado haijafanyika ambapo Serikali ipo katika hatua ya kumpata Mtaalamu Elekezi. Suala hili limechelewa ambapo ilitarajiwa liwe limekamilika kwa ajili ya kuanza maandalizi ya Dira Mpya.

#### **4.1. Kuanza Maandalizi ya Dira Nyingine ya Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Maandalizi ya Tathmini ya Dira ya 2025 na Dira Mpya ya 2050 yapewe kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2023/24. Vilevile, ni vyema Serikali ijiwekee utaratibu wa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mipango yake ikiwa ni katika kujipima na kujua ni kwa kiasi gani imeweza kufikia malengo yake, yaliyo kwenye dira.

#### **4.2. Muda Maalum wa Ukamilishaji wa Miradi**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuwa na vipaumbele vingi na miradi kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi, utekelezaji wake na ukamilishaji umekuwa hauendani na matarajio. Miradi mingi imekuwa inachukua muda mrefu kutekelezwa, kukamilika na mingine kuishia njiani au kutokukamilika kabisa. Hali hii

haisababishia Serikali hasara ya kulipa riba zinazo tokana na hati za madai kutolipwa kwa wakati na pia kuwa na mitaji ambayo haizalishi kwa muda mrefu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi michache yenye tija na kwa wakati ili kuiepushia Serikali hasara au gharama kubwa ya miradi. Aidha, ni vyema vipaumbele vilivyobainishwa viainishe shughuli zitakazotekelezwa katika mwaka husika.

### **4.3. Dhahabu kuwa Sehemu ya Fedha za Kigeni (Monetary Gold)**

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2017, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria za uchimbaji madini iliyoipa Serikali mamlaka ya kisheria ya kuanzisha hazina ya Taifa ya madini ya dhahabu na vito ambapo Benki Kuu imepewa jukumu la kutunza na kulinda hazina hiyo. Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuvutia viwanda vya kuchenjua dhahabu nchini ili kuyaongezea madini yetu thamani kabla ya kusafirishwa nje ya nchi. Viwanda hivyo ni Mwanza Precious Metal Refinery, Geita Gold Refinery na Eyes of Africa Gold Refinery vyenye uwezo wa kusafisha dhahabu kwa ubora wa (purity) **asilimia 99.9** kama taratibu na miongozo ya Shirika la Fedha Duniani– IMF inavyoelekeza. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupitia Benki Kuu kuharakisha na kukamilisha maandalizi ya kuanza kutunza akiba ya fedha za kigeni kwa Dhahabu hasa ikizingatiwa kwamba dhahabu ni madini ambayo yamethibitika kuwa na uwezo wa kutunza thamani.

### **4.4. Vyanzo Mbadala na Bunifu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba vyanzo mbadala na bunifu vilivyobainishwa katika Mpango wa

Mwaka 2023/24 vimekuwa vikitajwa katika mipango ya maendeleo ya Serikali lakini havijaweza kutumika kugharamia miradi ya maendeleo. Kamati inashauri Serikali kuruhusu halmashauri zenye mapato ya ndani yanayoweza kulipia riba za Hati fungani za Manispaa (*municipal bonds*) ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Hatua hii itaziongezea halmashauri hizi mapato kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kimkakati katika maeneo yao.

#### **4.5. Kuiwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya jambo kubwa ambalo husababisha mfumuko wa bei nchini ni kupanda kwa bei za chakula. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuiwezesha NFRA ili iwe na uwezo wa kununua chakula cha kutosha katika kuendelea kuimarisha utoshelevu wa chakula nchini ili kukabiliana na athari za majanga ya asili mfano, mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la bei za mazao.

#### **5.0. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia **Shilingi trilioni 37.99** Aidha, Serikali iliweza kukusanya **Shilingi trilioni 36.92** ikiwa ni ufanisi wa **asilimia 97.2**. Mafanikio haya yamepatikana chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo anastahili pongezi. Kamati inathibitisha kwamba tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016 ikiwa ndio Kamati mama inayosimamia Serikali, haijawahi kuona ufanisi kama huu wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali hasa katika utoaji wa fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, mapato ya ndani yalifikia ufanisi wa **asilimia 95** ya lengo la mwaka. Ufanisi huu ulichangiwa na juhudi zinazoendelea kufanywa na Serikali kuhakikisha kuwa inapata mapato yake stahiki ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya mlipa kodi, kuimarisha mifumo ya TEHAMA, kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Biashara nchini na kusimamia vema sheria, kanuni na taratibu za kodi.

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine ni pamoja na mkopo wa **shilingi bilioni 1,310.65** kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa – IMF. Hili ni jambo jingine la kupongezwa kwa **Rais** wetu kuendelea kuipigania Tanzania katika kila fursa Kimataifa ili kuimarisha uchumi wa Tanzania na kusukuma gurudumu la maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2021/22, Serikali ilikopa zaidi ndani kwa **asilimia 18** ya lengo lilikuwa limewekwa, pamoja na kwamba mikopo ya ndani ni nafuu kwa sababu inalipwa kwa shilingi na kutokupatikana kwa mikopo ya kibiashara ya nje. Pamoja na faida za mikopo ya ndani athari inayoweza kujitokeza ni mabenki na Taasisi za Fedha kuvutiwa zaidi kuikopesha Serikali kuliko sekta Binafsi na hivyo kusababisha ukosefu wa Mikopo kwa Sekta binafsi. Kamati inaishauri Serikali kupitia Benki kuu kuhakikisha kwamba katika kipindi chote ukopaji wa Serikali hauathiri upatikanaji wa mikopo kwa Sekta Binafsi.

7 NOVEMBA, 2022

**Jedwali Na.2 Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2021/22  
Shilingi Bilioni**

<b>MAPATO/MATUMIZI</b>	<b>BAJETI</b>	<b>HALISI</b>	<b>ASILIMIA</b>
<b>Mapato ya Ndani</b>	<b>25,691.7</b>	<b>24,395.6</b>	<b>95.0</b>
Mapato ya Kodi (TRA)	20,283.4	20,029.3	98.7
Mapato Yasiyo ya Kodi (TRA)	1,494.7	902.0	60.3
Mapato Yasiyo ya Kodi	3,049.8	2,574.8	84.4
Mapato ya Halmashauri	863.9	889.5	103.0
<b>Misaada</b>	<b>1,138.1</b>	<b>708.5</b>	<b>62.3</b>
Misaada ya Kibajeti	-	<b>103.2</b>	
Misaada ya Maendeleo	915.5	519.3	56.7
Mifuko ya Kisekta	222.6	86.0	38.6
<b>Mikopo Nafuu</b>	<b>3,128.5</b>	<b>4,116.8</b>	<b>131.6</b>
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1,310.7	1,291.7	98.6
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,770.0	2,818.3	159.2
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	47.8	6.8	14.2
<b>Mikopo ya Kibiashara Kutoka Nje</b>	<b>3,045.1</b>	<b>1,809.5</b>	<b>59.4</b>
<b>Mikopo ya Kibiashara Kutoka Ndani</b>	<b>4,989.1</b>	<b>5,894.4</b>	<b>118.1</b>
Mikopo ya Kugharamia Miradi	1,838.8	2,850.0	155.0
Mikopo ya Kulipa Mtaji Deni la Ndani	3,150.3	3,044.4	96.6
<b>JUMLA YA MAPATO</b>	<b>37,992.5</b>	<b>36,924.8</b>	<b>97.2</b>
<b>Matumizi ya Kawaida</b>	<b>22,732.8</b>	<b>22,561.5</b>	<b>99.2</b>
Mishahara	8,136.5	8,087.4	99.4
Mfuko Mkuu wa Serikali (Deni)	8,756.8	8,756.8	100.0
Matumizi Mengineyo & CFS	5,839.5	5,717.3	97.9
<b>Matumizi ya Maendeleo</b>	<b>15,259.7</b>	<b>14,654.3</b>	<b>96.0</b>
Miradi ya Fedha za Ndani	11,591.1	11,554.6	99.7
Miradi ya Fedha za Nje	3,668.6	3,099.7	84.5
<b>JUMLA YA MATUMIZI</b>	<b>37,992.5</b>	<b>37,215.8</b>	<b>98.0</b>

**Chanzo:**Wizara ya Fedha na Mipango

## **6.0. UCHAMBUZI WA KAMATI KUHUSU MWONGOZO NA MAANDALIZI YA MPANGO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 NA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA 2023/24.**

### **6.1. Uchambuzi wa Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali imepanga kukukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 43.29** sawa na ongezeko la Bajeti la **asilimia 4.37** ukilinganisha na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2022/23.

#### **6.1.1. Mapato ya Ndani**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2023/24 mapato ya Serikali kwa ujumla yanatarajiwa kukua kwa **asilimia 4.37** ambapo mapato ya ndani yanatarajiwa kukua kwa **asilimia 10.77** ukilinganisha na mapato yaliyokusanywa kwa mwaka 2022/23. Aidha, kwa upande wa mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuwa na ukuaji wa **asilimia 13.01**. Ukuaji huu unaonyesha kwamba ukuaji halisi wa mapato ya Serikali ya ndani na yale ya Serikali za Mitaa ni zaidi ya mfumuko wa bei wa lengo la **asilimia 5** na ukuaji wa pato la Taifa unaotarajiwa wa **asilimia 4.7**. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha hizo ili kutekeleza miradi ya maendeleo yenye tija kwa Taifa. Vilevile, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kukusanya Mapato ya Serikali kwa ufanisi na weledi.

### 6.1.2. Mikopo na Misaada

**Mheshimiwa Spika**, misaada inatarajiwa kuongezeka kutoka **Shilingi trilioni 1.101** mwaka 2022/23 hadi **Shilingi trilioni 1.113** mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la **asilimia 0.94**. Aidha, misaada ya mifuko ya Kisekta imeongezeka kwa **asilimia 6.64**, ukilinganisha na misaada ya kibajeti iliyoongezeka kwa **asilimia 0.71**. Hali hii inamaanisha kwamba wafadhili wamehama kutoka kwenye Misaada ya Kibajeti na kujielekeza moja kwa moja kwenye miradi. Hivyo kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na tathmini ya ufuatiliaji ya miradi inayopata fedha moja kwa moja kutoka kwa wafadhili ili ilete matokeo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mikopo ya masharti nafuu imepungua kutoka **Shilingi trilioni 3.55** kwa mwaka 2022/23 hadi **Shilingi trilioni 3.4** kwa mwaka 2023/24, sawa na wastani wa **asilimia hasi 4.16**. Aidha, kwa upande wa mikopo nafuu ya miradi ya maendeleo imeongezeka kutoka **Shilingi trilioni 1.65** kwa mwaka 2022/23 hadi **Shilingi trilioni 2.23** kwa mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la **asilimia 34.73**. Ongezeko hili ni kutokana na mkopo wa ECF kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maendeleo iliyoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/23. Kamati inaishauri Serikali ifanye marejeo kwenye lengo la mkopo wa ECF ili shughuli zinazotekelezwa ziendane na mkopo huo.

### 6.1.3. Uchambuzi wa Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali imetenga jumla ya **Shilingi trilioni 43.29**, ambapo Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi trilioni 28.27** sawa na ongezeko la **asilimia 6.77** ukilinganisha na Shilingi trilioni



26.47 mwaka 2022/23, na Matumizi ya Maendeleo ni **Shilingi trilioni 15.03** sawa na ongezeko la **asilimia 0.15**, ukilinganisha na **Shilingi trilioni 15.01** kwa mwaka 2022/23.

#### **6.1.4. Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali inatarajia kutenga kiasi cha **Shilingi trilioni 28.27**. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yameongezeka kutoka **Shilingi trilioni 11.31** mwaka 2022/23 hadi **Shilingi 12.49** mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la **asilimia 10.44**. Ongezeko hilo linatokana na ulipaji wa deni la Serikali, ongezeko la mishahara (**asilimia 4.2**), ajira mpya katika Sekta za Afya na Elimu na upandishwaji wa madaraja. Kwa upande wa Matumizi mengineyo yameongezeka kwa **asilimia 3.6**, Ongezeko hilo limetokana na ugharamiaji wa uendeshaji wa miradi ya maendeleo iliyokamilika

#### **6.1.5. Matumizi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia kukamilika kwa miradi ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya elimu, afya na maji imesababisha matumizi kuongezeka kwa **asilimia 0.15**. Fedha za ndani zinazotarajia kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo zinatarajiwa kupungua kwa **asilimia 4.56**, kwa upande wa Fedha za nje yanatarajiwa kuongezeka wa **asilimia 21.6**. Hii inatokana na miradi iliyokuwepo ambayo inaendelea kutekelezwa kwa Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, mfumo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24 unaonyesha kwamba Serikali inakusudia kukusanya mapato ya ndani kiasi cha **Shilingi trilioni 31.03** sawa na ongezeko la **asilimia 10.77** ukilinganisha na mapato ya **Shilingi trilioni 28.02** yaliyokusanywa mwaka

## 7 NOVEMBA, 2022

2022/23. Kwa upande wa matumizi ya kawaida Serikali inakusudiwa kutumia **Shilingi trilioni 28.27** sawa na ongezeko la **asilimia 6.77** ukilinganisha na matumizi ya **Shilingi trilioni 26.47** mwaka 2022/23. Mizania hii inaonyesha kwamba mapato yetu ya ndani yana uwezo wa kugharamia matumizi yote ya Serikali na bado kukawa na ziada ya **asilimia 3.85** hatua hii ni ya kupongeza.

### Jedwali Na.3 Ulinganisho wa Bajeti ya Mwaka 2022/23 na Mwaka 2023/24

Chanzo cha Mapato	Bajeti Iliyoidhi nishwa 2022/23	Makadiri o ya Bajeti 2023/24	%
<b>Mapato ya Ndani</b>	<b>28,018</b>	<b>31,034.6</b>	<b>10.77%</b>
Mapato TRA (Kodi na yasiyo ya Kodi)	23,653	26,379.0	11.53%
Mapato yasiyo ya Kodi	3,353	3,511.7	4.73%
Mapato ya Halmashauri	1,012	1,143.9	13.03%
<b>Misaada</b>	<b>1,101</b>	<b>1,111.3</b>	<b>0.94%</b>
Misaada ya Kibajeti	56	56.4	0.71%
Misaada ya Miradi ya Maendeleo	924	924.8	0.09%
Misaada ya Mifuko ya Kisekta	122	130.1	6.64%
<b>Mikopo Nafuu</b>	<b>3,547</b>	<b>3,399.6</b>	<b>-4.16%</b>
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1894	1,172.5	-38.09%
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,653	2,227.1	34.73%
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	-	-	-
<b>Mikopo ya Ndani na Nje ya Masharti ya Kibiashara</b>	<b>8,814</b>	<b>7,749.1</b>	<b>-12.08%</b>
Mikopo ya Nje	3,034	2,110.6	-

## 7 NOVEMBA, 2022

Chanzo cha Mapato	Bajeti Iliyoidhi nishwa 2022/23	Makadiri o ya Bajeti 2023/24	%
			30.44%
Mikopo ya Ndani	2,480	2,096.4	- 15.47%
Mikopo ya Ndani Kulipia Mtaji wa Deni la Ndani	3,300	3,542.1	7.34%
<b>JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C)</b>	<b>41,481</b>	<b>43,294.6</b>	<b>4.37%</b>
<b>Matumizi ya Kawaida</b>	<b>26,474.6</b>	<b>28,266.6</b>	<b>6.77%</b>
Mfuko Mkuu wa Serikali	11,308	12,488.2	10.44%
Mishahara	9,831	10,251.3	4.28%
Matumizi Mengineyo	5,335	5,527.1	3.6%
<b>Matumizi ya Maendeleo</b>	<b>15,006.0</b>	<b>15,028.0</b>	<b>0.15%</b>
Fedha za Ndani	12,307	11,745.9	- 4.56%
Fedha za Nje	2,699	3,282.1	21.6%
<b>JUMLA MATUMIZI YOTE (E+F)</b>	<b>41,481</b>	<b>43,294.6</b>	<b>4.37%</b>

**Chanzo:**Wizara ya Fedha na Mipango

### 7.0. MAONI YA UJUMLA YA KAMATI

#### 7.1. Uratibu wa Shughuli za Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba kuna changamoto katika kuratibu Shughuli za Serikali. Mfano, katika uunganishaji wa umeme vijijini, Wakala wa umeme vijijini (REA) anaunganisha miundombinu ya Umeme, haunganishi shule zote zilizoko katika eneo husika, Taasisi mbalimbali za Serikali kutekeleza jukumu moja la utoaji mikopo kwa wajasiliamali wadogo, Taasisi za Umma moja kukwamisha nyingine kama vile wakala wa Mimitu (TFS) na

kuzuia Wakala wa Umeme Vijiji (REA) katika kupitisha miundombinu ya umeme mpaka walipie njia hiyo. Pamoja na Uwepo wa *Dash Board* ya uratibu wa Shughuli za Serikali chini Ofisi ya Waziri Mkuu bado tatizo hili limeendelea kuwepo kwa sababu baadhi ya Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali zinafanya kazi kwenye mfumo wa vihenge (silos). Hali hii inasababisha kutokuwa na ushirikiano baina ya Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali.

## **7.2. Kutotabirika kwa Sera za Kodi**

**Mheshimiwa Spika**, Moja ya changamoto inayoikabili nchi yetu katika eneo la uwekezaji ni pamoja na mabadiliko ya mara kwa mara ya sera za kodi na fedha, hivyo kuwafanya wawekezaji washindwe kufanya uwekezaji wenye tija nchini. Kwa msingi huo Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba sera za kodi na fedha hazibadiliki mara kwa mara na vilevile kodi ya makampuni (corporate tax) ifanyiwe mapitio ili kuondoa vikwazo katika uwekezaji.

## **7.3. Sheria Mpya ya Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa sheria mpya ya uwekezaji iliyopitishwa na Bunge inaweka misingi ya uwekezaji nchi nzima. Kamati inashauri Serikali kuangalia maeneo yafuatayo:-

- i. Sheria hii iendane na Sheria zingine za nchi, ili kuondoa ukinzani katika sheria nyingine;
- ii. Sheria iainishe maeneo ambayo nchi ina uhitaji wa uwekezaji na kuweka vivutio vya ziada ili wawekezaji waweze kuvutiwa zaidi kuwekeza. Hii itasaidia nchi kujitangaza katika maeneo husika;

- iii. Sheria imuangalie zaidi muwekezaji wa ndani kwa kumwezesha na kumuwekea mazingira mazuri ili kujenga uchumi jumuishi na shirikishi.

#### **7.4. Barabara zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kujenga barabara inayounganisha mipaka ya Tanzania na nchi ya Kenya hasa katika maeneo ya Mkinga, Lushoto, Same hadi Holili katika mkoa wa Kilimanjaro. Hii itasababisha kuwepo kwa njia rasmi ya kufikia mipaka hiyo na hivyo kuondoa changamoto ya biashara ya magendo katika mipaka hiyo na kuiongezea Serikali mapato yake.

#### **7.5. Kufanya Mapitio ya Sheria ya Manunuzi Sura 410**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria ya manunuzi sura 410. Kamati imebaini kwamba Sheria hii haijafanyiwa marejeo kwa muda mrefu na hivyo kuathiri sekta ya manunuzi nchini. Kwa mfano kwa mujibu wa sheria hiyo mchakato wa kumtafuta Mzabuni unahitajika kufanyika kwa muda wa siku tisini (90) isipokuwa kwa baadhi ya mazingira ambayo nayo ni magumu kuyakidhi. Siku hizi ni nyingi na zimekuwa ni moja ya sababu ya kuchelewa utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za Serikali. Vilevile, Sheria ya Ununuzi wa Umma inamtaka anayeshinda tenda za Serikali awe ni aliyetoa bei ya chini kuliko wazabuni wote (lowest bidder). Mara nyingi bei zinazotolewa na mzabuni huyu (lowest bidder price) haziakisi bei ya soko. Kamati inaamini kwamba endapo Sheria hii itafanyiwa marejeo itasaidia Serikali kuondoa ushawishi wa vitendo vya rushwa na ubadhirifu, kutopokea bidhaa au huduma zenye kiwango duni tofauti na inavyo-onyeshwa kwenye nyaraka za zabuni

na mikataba pamoja na kuhakikisha Serikali inapata thamani ya fedha (value for money) kutokana na manunuzi yanayofanyika.

### **7.6. Utekelezaji wa Miradi ya Maji**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya maji ni miongoni mwa sekta chache zilizokua kwa kasi katika mwaka wa fedha 2022/23, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba katika kipindi cha miaka mitano (2015-2020) jumla ya miradi ya maji 1,848 imetekelezwa nchini. Hata hivyo, sekta hii pamoja na kuwa na miradi mingi bado inakumbwa na changamoto mbalimbali kama vile; Wakandarasi wasiokuwa na uwezo wanaosababisha miradi ya maji nchini kutekelezwa chini ya kiwango, kucheleweshwa kwa manunuzi ya vifaa na malipo ya mkandarasi hali inayopelekea kuchelewa kukamilika kwa miradi mingi ya maji kwa wakati, miradi ya maji kutokuwa endelevu, kukauka kwa vyanzo vya maji mfano mto mkuu wa Ruaha ambao umekuwa ukikauka mara kwa mara. Kamati inaishauri Serikali kuongeza usimamizi katika utekelezaji wa miradi ya maji ili ilete tija inayotazamiwa kwa kujengwa kwa ubora na kwa kuzingatia thamani ya fedha.

### **7.7. Ujenzi wa Barabara kwa Mfumo wa Uandisi, Usanifu, Manunuzi, Ujenzi na Utafutaji wa Fedha (EPC+F-Engineering Procurement Construction and Financing)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23 Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi alitaarifu Bunge lako kwamba barabara katika mwaka huu wa fedha zitajengwa kwa kasi kwa kutumia mfumo wa EPC+F. Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipata fursa ya kukutana na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Ujenzi

na Uchukuzi na kubaini kwamba matumizi ya mfumo huo hayatakuwa na matokeo ya haraka kama ilivyokusudiwa kwa sababu kuu mbili. Moja mwenye Mamlaka ya Kukopa kwa Niaba ya Serikali ni Waziri wa Fedha na Mipango kwa Mujibu wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali Sura ya 134 na pili ujenzi wa namna hii una athari ya moja kwa moja kwenye Deni la Serikali. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuliko kutumia mfumo huu ambao utachukua muda ni vyema tukope kwenye masharti nafuu ili tutekeleze miradi ya kimkakati ambayo ina tija kwa Taifa. Kuliko kutumia mfumo huu ambao unaweza kuathiri deni la Serikali kwa namna ambayo inaweza isihimilike.

## **8.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yako iliyoiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake, aidha, napenda kumshukuru Mhe Mussa Azzan Zungu Mb, na Naibu Spika kwa ushirikiano wake kwa Kamati. Vilevile nimshukuru. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Ndg. Jenifa C. Omolo Naibu Katibu Mkuu Utawala na Huduma za Mfuko Mkuu kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2023/24 pamoja na Mwongozo wa uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mhe Omari Kigua Mb, na Makamu Mwenyekiti pamoja na wajumbe

## 7 NOVEMBA, 2022

wa Kamati hii kwa umakini na uweledi wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb Mjumbe
4. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb Mjumbe
5. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb Mjumbe
6. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb Mjumbe
7. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb Mjumbe
8. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb Mjumbe
9. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb Mjumbe
10. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb Mjumbe
11. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb Mjumbe
12. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb Mjumbe
13. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb Mjumbe
14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb Mjumbe
15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb Mjumbe
16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb Mjumbe
17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb Mjumbe
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb Mjumbe
19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb Mjumbe
20. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb Mjumbe
21. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb Mjumbe
22. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nanelwa Mwihambi, ndc kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi na Makatibu wa Kamati Ndg. Lilian



**7 NOVEMBA, 2022**

Masabala, Ndg. Wilfred Akasi, Ndg. Maombi Kakozi na Ndg. Trifina Tanzania kwa kuipatia ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

7 Novemba, 2022

*(Hoja iliyolewa lamuliwa)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti ahsante sana, kwa kuunga mkono hoja. Kabla hujatoka hapo, 3.115 ya taarifa ya Kamati, miradi ya Bandari. Umeshaiiona? Kwangu ni ukurasa wa 12 lakini kurasa zinaweza kutofautiana ni kwenye sekta ya miundombinu. Hii Bandari ya Tanga.

Wakati ukiendelea kutafuta taratibu, Waheshimiwa Wabunge Kamati inasema inaishauri Serikali kufanya maboresho ya bandari kwenye miundombinu, mitambo na vifaa ili kuvutia Meli na Shehena nyingi. Hii sehemu ya umbali wa Kilometa 1.7, ni hii ambayo CAG alikuwa anasema pesa zimelipwa kwenye mwaka wa fedha 2020/2021 ama siyo? Mwenyekiti wa Kamati ya PAC.

**MHE. NAGENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa bado naangalia ripoti

**7 NOVEMBA, 2022**

yetu kama ilikuwa ndiyo hiyo ama siyo. Labda nitatoa majibu baadae kidogo.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante. Hii sehemu nilitaka Mwenyekiti uione kwa sababu Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kwamba ifanye maboresho ya miundombinu kwenye Bandari ya Tanga. CAG ametoa taarifa kwamba Bandari ya Tanga ili kuongeza hiki kina zililipwa Shilingi Bilioni 104. Sasa sijaelewa pesa zile kama zilivyolipwa, halafu zile Shilingi Bilioni 40 zilivyotolewa kwa yule aliyekuwa *sub-contracted* ilikuwa ni kuchimba hiki kina au kufanya jambo tofauti? Kwa sababu pesa zilitolewa mwaka ule 2020/2021 ndiyo maana CAG ameulizia.

Sasa hapa tena inaonekana bado kuna changamoto Tanga hapo hapo tena na yenyewe inazungumzia kina, Meli kushindwa kufika kwenye Bandari umbali wa kilometa 1.7. Sasa Mwenyekiti wa PAC hajapaona bado anapatafuta. Upande wa Serikali, Waziri wa Ujenzi yuko kwenye changamoto kule Bukoba. Naibu Waziri ni hii sehemu au ni kitu kingine tofauti, kazi ile ilishafanyika halafu hili ni jambo lingine ambalo Kamati inapendekeza.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni eneo hilo hilo ambalo Bunge lilishaazimia siku ya Jumamosi, kwa sababu ni bandari hiyo hiyo moja kuongeza kina na kufanya *trenching*.

**MWENYEKITI:** Huyu Mkandarasi aliyelipwa zile Bilioni 40 hajafanya kazi kuanzia mwaka 2020/2021? Maana ndiyo kipindi alichopewa hizo pesa. Au kuna jambo mimi ndiyo sielewi? Haya tutapewa taarifa lakini hii taarifa iliyoandikwa hapa ama mapendekezo yaliyotolewa na

**7 NOVEMBA, 2022**

Kamati ya Bajeti, yanazungumzia kuongezwa kwa kina cha Bandari ya Tanga kwa hiyo kilometa 1.7. CAG anasema zilishalipwa Bilioni 104 kwa Kampuni sijui inaitwa *CHENG*, halafu *CHENG* akampa mwingine akajenga kwa Bilioni 40. Sasa kama tunazungumzia Bandari ile ile, pesa ililipwa, changamoto bado ipo, hebu ngoja mtafute hizo taarifa ili zitusaidie.

Naona Mheshimiwa amesimama kule anataka kusaidia. Haya Mheshimiwa Isack Kamwelwe.

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilometa 1.7 *dragging* imeshafanyika tayari, kwa hiyo Meli sasa hivi zinaingia. Mradi huu ulishakamilika.

**MWENYEKITI:** Haya, mradi ulishakamilika. Kamati yetu ya bajeti ambayo huwa inakutana na Serikali wote hawana taarifa. Haya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. DANIEL S. BARAN - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilifanya ziara katika Mkoa wa Tanga mwezi uliopita na kati ya changamoto iliyosemwa na watu wa Bandari ilikuwa ni hii, kwamba shehena inashindwa kuhimili kwa sababu gati ilipo na Meli inapotia nanga kuna umbali huo wa kilometa 1.7.(Kicheko)

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, Kamati yetu ya Bajeti inasema ilienda Tanga na watu wa Bandari wakasema kuna changamoto ya hii kilometa 1.7, meli zinaishia ndani kule baharini. Hapa aliyekuwa Waziri wakati huo anasema kazi ilishafanyika, sasa kwa nini Meli zinaishia kule na hii ni 2022?

## 7 NOVEMBA, 2022

Sasa hili itabidi litafutiwe majibu kama hakuna majibu itabidi tuyapate sawa sawa kwa sababu pesa ilishalipwa ndiyo maana CAG kazungumzia. Mazingira iliyolipwa ndiyo yale aliyaulizia CAG, lakini kwamba pesa ililipwa ndiyo ilishalipwa. Sisi tuliamini mwaka 2022 hiyo changamoto haipo. Kamati inasema huu ni mwezi wa Novemba, imeenda huko mwezi Oktoba na imekuta changamoto ipo. Nadhani tuwape muda kidogo Serikali ilete taarifa mahsus ambayo kama haitakuwa hivyo, basi itabidi ndani ya siku mbili, tatu hizi watu watumwe huko Tanga wakatazame, pamechimbwa au hapajachimbwa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana kwa taarifa yako. Mheshimiwa Waziri ulikuwa umesimama ama itaenda kutafutwa taarifa?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeshaliweka sawa tuta-network pamoja na watu wa bandari ili tujiridhishe aina ya changamoto kwa sababu kwenye bandari changamoto zinakuwa za aina tofauti tofauti. Tujiridhishe na tuoanisha na taarifa ya Kamati kama changamoto inayosemwa inahusiana na kilichoandikwa ama unaweza ukakamilisha kuchimba ukawa huna sets zingine za vitu vinavyohitajika ama mengine yanayohusiana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ulivyoelekeza ni vizuri, tunaomba tupate taarifa za ndani ya Wizara, eneo husika la bandarini pia tujiridhishe aina ya changamoto ambayo bandari walitaja kwa Kamati.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa ili tujielekeze vizuri, changamoto iliyotajwa hapa ni ya mizigo kuishia kilometa 1.7 baharini na kushindwa kufika kwenye gati ambayo

ipo. Kwa hiyo, mtuangelizie hiyo hapo pameishachimbwa au hapajachimbwa? Kwa sababu CAG taarifa yake ilikuwa inaelezea malipo kwa ajili ya jambo hilo na nafikiri hiyo taarifa tukiipata mapema itatusaidia sana ili wakati tunajadili huu mpango tuje tuendeleo kupendekeza kuhusu Bandari ya Tanga? Au hii changamoto Tanga haipo kwa hiyo tusonge mbele kwenye kupendekeza mambo mengine.

Mheshimiwa Kuchauka naona umesimama, wewe una majibu ya ziada yatakayotufanya tusiende Tanga siyo?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sisi tuko Kamati ya Miundombinu, tulitembelea Bandari ya Tanga na tulikuta kazi kule iko asilimia 80 kuisha na tukaishauri Serikali...

**MWENYEKITI:** Sogeza kisemeo.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Tulikwenda kutembelea Bandari ya Tanga na tulikuta kazi ipo asilimia 80 ya kazi hiyo ya *drainage* kukamilika...

**MWENYEKITI:** Ninyi mlienda lini?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda kabla ya Bunge lililopita...

**MWENYEKITI:** Hili la mwezi wa tisa au Bunge la Bajeti?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Bunge la mwezi wa tisa.

**7 NOVEMBA, 2022**

**MWENYEKITI:** Mlikuta asilimia 80 ya kuchimba si ndiyo?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuta zaidi ya asilimia 80 ya kuchimba imetumika. Changamoto ambayo tuliyoikuta pale wakasema kwamba itakapokamilika ina maana sasa mzigo utakuwa mwingi na lile *godown* ndiyo lilikuwa dogo. Wakaambiwa kwamba kuna mahali kunaitwa Mwambao wakachukue lile eneo kwa wananchi na Serikali ilipe ili kupanua lile eneo la kuweka *godown*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Hiyo taarifa inatusaidia lakini haituondoi kwenye changamoto iliyopo kwa sababu aliyekuwa Waziri anasema kazi ilishakamilika, wewe unasema imefikia asilimia 80, halafu taarifa nyingine hatuna hakika kama inazungumziwa hiyo kilometa 1.7 au jambo lingine?

Nadhani tuipe muda kwanza, mimi nipate taarifa kutoka upande wa Serikali, nikishaipata hiyo sasa ndiyo tutajua changamoto inayozungumziwa hapa. Hizi kilometa usikute zilikuwa zaidi ya hiyo, kwa hiyo, yule aliyechimba katoka huko mbali ndiyo kafikisha hapo kwenye 1.7, tutapata hayo majibu. Upande wa Serikali nadhani mkiweza kutusaidia hayo majibu yakipatikana leo itatusaidia sana ili kuweza kutusaidia kama Bunge wakati tunajadili haya mapendekezo ya Mpango tutaweza kuongozana vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda kwa hiyo nimwite Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI.**

**7 NOVEMBA, 2022**

*(Bunge lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani niongee nikiwa nimesimama kwa sababu nitasimama sasa hivi. Kwa sababu tumepata taarifa hii muda siyo mrefu, Waheshimiwa Wabunge inavyoonekana mnahitaji muda wa kwenda kuipitia pia kupitia na taarifa ya Kamati ili tuanze kuchangia. Katika mazingira hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Kamili Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.30 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 8 Novemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*

**7 NOVEMBA, 2022**